

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 7 Mei, 2021**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kikao cha Ishirini na Tano cha Mkutano wetu wa Tatu.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu, swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, tafadhali.

Na. 205

**Kukitumia Kikamilifu Kitengo cha Kukuza Tija Kilichopo Ofisi ya Waziri Mkuu**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukitumia kikamilifu Kitengo cha Kukuza Tija kilichopo Ofisi ya Waziri Mkuu ili

kuhakikisha utekelezaji wa miradi mikubwa nchini unakuwa wa tija na kuwanufaisha Watanzania?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Kapungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, CCM kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Kitengo hiki kinatekeleza majukumu yake kikamilifu, Serikali imepanga kutekeleza mipango ifuatayo:-

Moja, kuandaa Sera ya Taifa ya Tija na Ubunifu (*National Productivity and Innovation Policy*) ambayo itaweka mfumo thabiti wa kupima tija na ubunifu katika ngazi ya taasisi, sekta na Taifa ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya Kitaifa.

Pili, kuanzisha kanzidata ya makubaliano, matamko na taarifa za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kuhusu tija, ubunifu na ufanisi wa viwanda.

Tatu, kufanya tafiti ya tija katika viwanda vya mfano vilivyopo Mikoa ya Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani.

Nne, kuandaa na kuwezesha Wiki ya Tija na Ubunifu (*Productivity and Innovation Week*).

Tano, ni kuandaa na kuwezesha Mpango wa Kitaifa wa Tuzo za Tija na Ubunifu (*National Productivity and Innovation Award Schemes*).

Sita, kuna mpango wa kuendesha programu 24 za kuwajengea uwezo wadau juu ya dhana, kanuni na viwango

vipya vinavyotakiwa katika tija, ubunifu na ufanisi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa Tatu (*FYDP III*) katika kutekeleza katika sekta binafsi, imeelekeza pia sekta binafsi kushiriki katika miradi mikubwa ya Kitaifa kwa kushirikiana na taasisi nyingine ikiwemo Kitengo cha Ukuzaji Tija ili iweze kuboresha ufahamu wa sekta binafsi juu ya masuala ya ufanisi na ushindani na pia utoaji wa huduma zilizo na ubora katika jamii.

**SPIKA:** Dkt. Alice umeridhika?

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kwanza nisahihishe majibu ya Mheshimiwa Waziri. Jina langu siitwi Alice Kapungi, naitwa Alice Karungi. Baada ya hapo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kutokana na umuhimu wa Sera hii ya Taifa ya Tija: Je, ni lini sera hii itakuwa tayari ili iweze kutumika tena kukuza tija? (*Makofi*)

Swali la pili, kutokana na marekebisho ya sera, sheria na kanuni ndogo ndogo za uwekezaji kwa nia ya kukuza uwekezaji: Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kukishika kikamilifu kitengo hiki katika marekebisho haya ya sheria ili mwisho wa siku sheria hizi ziwe zenye kuleta tija? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, kwa kipindi chote amekuwa akitupa

ushirikiano mzuri sana katika kuhakikisha tunafanya maboresho kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye maeneo ya kazi, vijana na pia kwenye masuala mtambuka kama ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, swali lake la nyongeza, napenda kujibu kuhusu lini sera hii itakuwa tayari? Kwa hatua ya sasa tayari tumeshaanza kuchukua maoni kwa wadau. Bahati nzuri sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameliuliza swali hili, kuna uwezekano mkubwa kwamba ana ufahamu na uelewa mpana juu ya jambo hili. Namwomba pia awe sehemu ya hao wadau ambao tutawafikia kwa ajili ya kukusanya maoni hayo tukiwa tunaenda kukamilisha sera.

Mheshimiwa Spika, baada ya bajeti hii nina imani kwamba kwa mwaka huu 2021 tunaweza kwenda kukamilisha sasa uwepo wa sera na pia kuangalia mabadiliko ambayo tutayafanya katika sheria. Hili litatusaidia sana kwa sababu tumeliona kama Ofisi ya Waziri Mkuu litatusaidia kukuza tija na ubunifu katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, kwenye maeneo ya *Agro-industry, automobile industry, airspace industry, mechanical industry, petro-mechanical industry* na kwenye maeneo mbalimbali ambayo ni mtambuka.

Mheshimiwa Spika, viwanda vyetu na maeneo mengine hata ya kazi yamekuwa yakitengeneza bidhaa ambazo mwisho wa siku kunakuwa na uzalishaji mkubwa, lakini ubora unakuwa chini. Kwa hiyo, hili ni eneo muhimu sana ambalo Serikali tumeona tuliangazie pia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Dkt. Alice kuhusu kukamilisha utaratibu wote wa mchakato wa kisheria kuweza kuhakikisha suala hili nalo linakuwa na nguvu ya kisheria ukiacha hivi hivi; hilo litaenda sambamba pamoja na hatua ya sasa ya kukusanya maoni ambayo tumekwisha kuianza na tuna imani kubwa kwamba kufikia mwaka huu tutakuwa tumekamilisha zoezi hilo na kuweza kurasimisha ili kuleta mapendekezo ya mabadiliko ya sheria, sambamba na kuwa na sheria ambayo inaweza ikasimama hapo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Tunaendelea na *TAMISEMI* Waheshimiwa Wabunge. Swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, tafadhali.

Na. 206

### **Hitaji la Wafamasia katika Vituo vya Afya**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuajiri Wafamasia angalau katika kila Kituo cha Afya nchini ili kuimarisha usimamizi na mtiririko wa upatikanaji dawa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Festo John Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, *TAMISEMI*, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ikama wa watumishi wa afya, Mfamasia anapaswa kuwepo katika ngazi ya Hospitali. Kwenye ngazi ya Vituo vya Afya na Zahanati, ikama inaelekeza kuwepo kwa Mteknolojia wa Dawa au Mteknolojia Msaidizi wa Dawa. Kada hizi ni muhimu kuwepo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa bidhaa za afya.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mei, 2017 hadi Februari, 2021 Ofisi ya Rais, *TAMISEMI* imeajiri Wafamasia 79, Wateknolojia wa Dawa 313 na Wateknolojia wa Dawa Wasaidizi 160. Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa

Wataalam hawa, ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kuajiri watumishi 10,467 wakiwemo Wafamasia na Wateknolojia wa Dawa watakaopelekwa kwenye Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya pamoja na zahanati kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali la nyongeza. Wakati mwingine wananchi wetu wanakwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wanakosa dawa siyo kwa sababu dawa hiyo inakuwa haipo kwenye maghala ya *MSD*, bali ni matatizo ya uagizaji ambayo yanatokana na vituo vyetu vya kutolea huduma za afya kutokuwa na hawa watu muhimu wafamasia na wateknolojia dawa ambao wana utaalam wa kuratibu, *ku-forecast* na kujua kwamba kipindi hiki tuagize dawa gani, kipindi hiki kuna mlipuko wa magonjwa fulani, kuwe na dawa fulani. Sasa ili kuhakikisha kwamba watu hawa muhimu wanakuwepo muda wote katika vituo vya kutolea huduma za afya:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuruhusu *Ma-DMO* na Wakurugenzi wa Halmashauri zenye uwezo *ku-engage* watu hawa ili wawepo muda wote hata kwa mtindo wa *internship* au mikataba ya muda wakati tukisubiri hizi ajira?

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kimsingi tunafahamu kwamba katika vituo vyetu vya huduma za afya kama ambavyo nimetangulia kueleza kwenye jibu la msingi, tuna upungufu wa wataalam hawa wa teknolojia wa dawa na wateknolojia wasaidizi wa dawa. Ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge Zedi ameelezea, tunahitaji kuwa na wataalam hawa ili kuhakikisha vituo vyetu vinaweza kuweka maoteo mazuri ya dawa lakini

pia uagizaji kulingana na utaalim ili kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na jitihada hizi za Serikali, pia Serikali ilishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi, kwa Halmashauri zile ambazo zina uwezo wa mapato ya ndani ya kuwaajiri kwa mikataba wataalam hawa, waweze kuwaajiri na kuwasimamia kwa karibu chini ya *DMO* kuhakikisha huduma hizi za upatikanaji wa dawa katika vituo hivyo zinaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba jambo hilo lishafanyiwa kazi na Serikali na nitoe wito kwa Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kutumia fursa hiyo kwa wale ambao wana uwezo wa kuwaajiri ili tuboreshe huduma za afya kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, swali kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

Na. 207

### **Korongo Linalopita Katikati ya Mji wa Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza kingo za korongo linalopita katikati ya Mji wa Mpwapwa lisiendelee kutanuka ili kunusuru maisha na makazi ya wananchi wa maeneo hayo?

**SPIKA:** Ahsante sana, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa naomba kutoa maelezo yafuatayo kuhusu Korongo lililoko katikati ya Mji wa Mpwapwa:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mpwapwa umejengwa pembezoni mwa mto ambao ni maarufu kwa jina la Mto Shaaban Robert, ambao sasa unaonekana kama Korongo linalopita katikati ya Mji. Kutokana na wananchi kufanya shughuli zao mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwenye kingo za mto huo, kumekuwa na kubomoka kwa kingo hizo. Hali ambayo imeleta athari kubwa kwenye miundombinu na makazi ya watu walioko karibu na kingo za mto huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na uharibifu huo wa mazingira, Serikali imefanya upembuzi wa awali kwenye mto kiasi cha urefu upatao kilometa mbili ambazo ziko jirani na makazi ya watu ili kufahamu gharama za kudhibiti kingo zake. Katika upembuzi huo, inakadiriwa kwamba zinahitajika kiasi cha shilingi bilioni 2,170 kwa ajili ya ukarabati huo. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kufanya yafuatayo:-

(i) Kuweka gabioni kiasi cha mita za ujazo 8,870;

(ii) Kujenga vizuri mmomonyoko kwa zege kiasi cha mita za ujazo 52;

(iii) Kujaza udongo maeneo yote yaliyoporomoka kiasi cha mita za ujazo 9,000; na

(iv) Kurudisha mto kwenye mkondo wake wa asili ambapo kinahitajika kifusi kiasi cha mita za ujazo 6,000. Serikali imetenga fedha ili kuweza kutekeleza mradi huo.



Mheshimiwa Spika, pia, napenda kuchukua fursa hii kuwasihii wananchi kuacha shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira katika kingo za mito na badala yake wajitahidi kupanda miti, kupanda majani ambayo yatazuia mmomonyoko wa kingo hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Korongo hili kwa msimu wa mvua wa mwaka 2020 na mwaka 2021, nyumba 29 za wananchi zimechukuliwa na maji.

Je, Serikali ina mpango gani kupitia Mfuko wa Maafa kuwasaidia wananchi hawa ambao wameathirika kwa kuchukuliwa na nyumba zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ili kuona ukubwa wa tatizo hili, ni muhimu sana Waziri na timu yake ya wataalam wa mazingira kutembelea eneo hili ili kuona wenyewe uharibifu ambao umetokea pale: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana nami katika eneo lile ambalo imetokea shida hii ajjionee mwenyewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo muhimu. Korongo hili ni kubwa, linatakiwa hifadhi ya milima.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Malima kwa juhudi yake ya ufuatiliaji katika mto huo na Jimbo lake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pili, nampa pole Mheshimiwa Mbunge kwa maafa ambayo yametokea katika mvua zilizopita. Ni kawaida ya Serikali, inapotokea maafa katika sehemu yoyote kufuatilia, kufanya tathmini na kuwafariji watu hao ambao wamepata maafa katika sehemu mbalimbali.

Kwa hiyo, nimtoe shaka kwamba, Serikali itafuatilia na itakwenda kuwafariji watu waliopata maafa katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili. Mimi pamoja na timu yangu ya wataalam, niko tayari kabisa kufuatana na yeye baada ya *Eid El-Fitr* twende wote kuona hali ilivyo *Inshallah*. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, hapo ni *trip* tu ya kwenda na kurudi tu siku hiyo hiyo, kwa hiyo, siyo mbali sana. (Makofi)

Waheshimiwa, tuendeleo na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, uliza swali lako, tafadhali.

Na. 208

### **Kukamilika Ujenzi wa Barabara za Nyololo - Mtwango Mafinga - Mgololo**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Nyololo – Mtwango – Mafinga hadi Mgololo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyololo – Mtwango yenye urefu wa kilomita 40.4 na barabara ya Mafinga – Mgololo yenye urefu wa kilometa 81.14 zinasimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS). Barabara ya Nyololo – Mtwango ni barabara ya mkoa ya kiwango cha changarawe na barabara ya Mafinga – Mgololo ni barabara kuu ya kiwango cha changarawe na kiwango cha lami katika maeneo korofi. Barabara hizi zinapita katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya biashara na chakula na pia zinahudumia viwanda kadhaa ikiwa ni pamoja na Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hizi, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Nyololo – Mtwango kwa kiwango cha lami. Aidha, inaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mafinga – Mgololo kwa kiwango cha lami, ambapo kwa sasa kazi hii ipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zitaingizwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami, kwa sasa barabara hizi zinaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali kila mwaka ili kuhakikisha kuwa zinapitika katika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa David M. Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa majibu ambayo yametolewa kwa kuzingatia kwamba barabara hizi tumezipigia kelele kwa muda mrefu na tunategemea zitusaidie kutuvusha kwenda uchumi wa kati wa juu, kwa sababu ndizo zinakusanya viwanda vyote

kule ambapo tunakusanya zaidi bilioni 40 kwa mwaka na pengine kwa miaka kumi ni nusu trilioni. Fedha hizi zote zinakwenda kujenga maeneo mengine, pale wananchi wakitaabika na hivi ninavyozungumza magari hayapatiki.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la nyongeza; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alisema hapa Bungeni mwezi Februari, zingeingizwa kwenye mwaka wa fedha huu 2021/2022; na kwa kuwa amezungumza pia usanifu umekamilika wa barabara hii moja. Kwa nini sasa hii iliyokamilika ya kilomita 40 ya kutoka Nyololo mpaka Mtwango isianze kujengwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hii ya pili ambayo amesema usanifu unakamilika ni ipi *commitment* ya Serikali sasa, itaanza lini na itakamilika lini? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Tafadhali, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey K. Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa amesikiliza jibu la msingi, tunatambua kwamba mbao zote karibu tunazoziona zinatoka eneo la Mafinga zinapita huko, magogo ni mengi. Ndio maana katika jibu langu la msingi nimesema mwaka 2022/2023, Serikali inatoa *commitment* kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sababu ni barabara ambayo sasa zimekuwa ni changamoto kwetu kutokana na uzito mkubwa kwamba kwa uwezo wa changarawe barabara zinashindwa kuhimili uzito wa magari yanayopita hapo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mufindi Kusini kwamba *commitment* ya Serikali ni kama tulivyosema kwenye jibu la Msingi tutaanza kujenga 2022/2023. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace V. Tendega nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya kutoka Iringa Mjini kwenda Pawaga kilomita 76 ambazo zilikuwa ni ahadi ya hayati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mbaya mno na wakulima wa pale wanalima mpunga lakini wanashindwa kusafirisha. Je, ni lini Serikali itakwenda kujenga barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, barabara ya Pawaga, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Iringa Pawaga ni kama barabara zingine ambazo zimepata changamoto kubwa katika kipindi hiki cha mvua. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi zipo kwenye ahadi na zitategemea na upatikanaji wa fedha. Pale ambapo fedha zitapatikana barabara hizo zitajengwa na ndioyo azma ya Serikali lakini kinachotukwamisha ni uwezo wa bajeti yetu. Kwa hiyo nimhakikishie fedha zikipatikana barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mbunge wa Korogwe Mjini.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tuna Barabara yetu ya Korogwe Mjini ambayo inatokea *Old* Korogwe, Kwamndolwa, Magoma, Mashewa, Bombo Mtoni mpaka Mabokweni, ambayo ni ahadi ya Marehemu Rais Magufuli, Mama Samia na Waziri Mkuu. Je, ni lini Serikali itatekeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kutimiza ahadi ya viongozi wetu wa kitaifa?

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara alizoitaja Mheshimiwa Mbunge wa Korogwe zipo kwenye ahadi ya Rais na zipo kwenye llani na ni kati ya barabara ambazo zinakamilisha kilomita 6,006 ambazo zimeahidiwa kujengwa katika kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kadri fedha itakapopatikana barabara hizi ikiwemo na hii zitajengwa kwa awamu. Ahsante.

**SPIKA:** Bado tupo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Swali la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Hanang’.

Na. 209

### **Ujenzi wa Barabara ya Kondoa – Gisambalang - Nangwa**

**MHE. SAMWEL X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Kondoa – Gisambalang – Nangwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Waziri swali hili ulijibu kwa makini kwa sababu Waheshimiwa Madiwani wa Hanang’ wapo humu ndani wanasikiliza majibu hayo kwa hamu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Samwel Xaday Hhyuma, Mbunge wa Hanang’, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kondoa - Nunguri - Mtiriyangwe - Gisambalang - Nangwa yenye urefu wa kilometa 81.4 ni barabara inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini *TANROADS* baada ya kupanda hadhi mwaka 2010 kutoka barabara ya wilaya na kuwa barabara ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya ukarabati ili ipitike kwa mwaka mzima. Katika mwaka wa fedha huu 2020/2021, barabara hii ilitengewa jumla ya milioni 888.8 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali na ukarabati na Shilingi milioni 60 kwa ajili ya usanifu wa Daraja la Mungurwi. Serikali itaiweka barabara hii katika mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii kuhakikisha kuwa inapitika vizuri majira yote ya mwaka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Hanang' uliza swali lako, Mheshimiwa Hhayuma.

**MHE. SAMWEL X. HHAYUMA:** Ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali yenye kutia matumaini, nina maswali mawili madogo. Swali la kwanza; kwa kuwa barabara hii inategemewa na wananchi, upande wa Hanang' tu zaidi ya 100,000 wa Kata za Gisambalang, Bilmaa, Simbai, Isilo, Waretu na Nangwa yenyewe na kulikuwa na Daraja la Mungurwi B. Daraja lile limechukuliwa na mafuriko ya mvua iliyonyesha 2019/2020. Ni kwa nini Serikali daraja lile lilivyochukuliwa halikuwekwa kwenye mpango wa dharura wa kulirudishia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa daraja lile la Mto Bubu limekuwa likigharimu Maisha ya watu na kupoteza mali kwa kusombwa na maji. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura ili kuhakikisha wananchi wanaendelea na shughuli zao za kijamii pamoja na biashara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Samwel Hhayuma, Mbunge wa Hanang', kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba daraja la Mungurwi B lilisombwa na maji na ni daraja ambalo liko sehemu ya bonde ambapo baada ya kusombwa lilitengeneza umbali wa mita zaidi ya 200 na hivyo ilikuwa ni ngumu sana kulijenga kama lilivyokuwa na badala yake, daraja hili linafanyiwa usanifu kutoka ilipokuwa kupanda eneo la juu ambalo tunaamini litakuwa ni eneo fupi, lakini pia hakutakuwa na changamoto ya mafuriko. Kwa hiyo linafanyiwa usanifu na baada ya kukamilika tutaanza kulijenga daraja hilo. Hiyo ndio sababu kubwa ambayo hatukuweka daraja la dharura.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la huo Mto Bubu nadhani nimelijibu pamoja na swali la kwanza kwamba baada ya fedha kupatikana na baada ya usanifu kukamilika, basi hilo daraja litakamilika ili kuunganisha wasafiri kutoka upande wa Kondoa kwenda upande wa Mkoa wa Manyara. Kwa sasa tunawashauri wananchi waendeleo kupita kutoka Kondoa kupitia Babati kwenda Katesh na kutoka Sambalang kwenda Babati bila kupita kwenye huo mto. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa maswali ya barabara mbona ni mengi sana, lakini swali hili tulibakizie hukohuko Hanang' na Mbulu, Mheshimiwa Flatei G. Massay, tafadhali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Swali la msingi linafanana kabisa na Jimbo la Mbulu Vijijini na changamoto iliyopo Hanang' inafanana kwa sababu ilikuwa ni wilaya moja. Barabara ya kutoka Mugitu kuja Hydrom iliahidiwa na ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi na Mheshimiwa Naibu Waziri aliipita. Je, ni lini tunajengewa kwa kiwango cha lami?



**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatel Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mugitu - Hydrom imeshakamilishwa kufanywa usanifu wa kina na sasa hivi kinachosubiriwa ni upatikanaji wa fedha ili ianzwe kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mbulu kwamba kadri fedha zitakapopatikana barabara hii itajengwa pia na ndio maana tayari usanifu wa kina umeshafanyika ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukubali kwa sababu ya muda tuendeleo na swali la Mheshimiwa Dkt. Thea M. Ntara kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Dk. Ntara, tafadhali.

Na. 210

### **Kujenga Chuo Kikuu Kanda ya Kusini**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo Kikuu cha Taifa Kusini mwa Tanzania na Kanda nyingine ambazo hazina Vyuo Vikuu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la

Mheshimiwa Dkt. Thea M. Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za uanzishwaji wa Vyuo Vikuu vya Umma hazilengi kuanzisha Vyuo Vikuu vya Kikanda, Kimkoa au Kiwilaya. Vyuo Vikuu vilivyopo nchini, vikiwemo vya Serikali na Binafsi, vinapokea wanafunzi kutoka Kanda zote za Tanzania Bara na Visiwani; na kutoka nje ya nchi. Huu ndio utaratibu wa Vyuo Vikuu Duniani kote. Katika Kanda ya Kusini kuna vituo vitatu vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (*OUT*) vilivyopo katika Makao Makuu ya Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Aidha, kipo Chuo Kikuu Kishiriki cha Stella Maris *STeMMUCO* kilichopo Mkoa wa Mtwara na Taasisi ya Uhasibu Tanzania *TIA* Kampasi ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mpango wa Serikali ni kuboresha Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu zilizopo kwa kukarabati na kujenga miundombinu mipya pamoja na kuongeza vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia. Tunafanya hivyo ili kuongeza nafasi za udahili na ubora wa elimu itolewayo na hivyo kukidhi mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo yamenikatisha tamaa, nimechanganyikiwa, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Serikali ilianzisha Kitengo cha *SUA* huko Tunduru, Waziri anijibu, je, ni lini tawi hilo litaanza kufanya kazi kama Chuo Kikuu Kishiriki au *Centre* na twende wote huko tukaone?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Swali la pili, Vyuo Vikuu Vishiriki vya Taasisi ya Dini vilivyopo Kusini kama hicho alichokitaja, *Stella Maris* na kile kingine kipo pale Songea kinaitwa *AJUCO*, vimeendelea kuzorota na vingine

vimefungwa. Serikali ndio inatakiwa kusimamia hivyo vyuo ili viweze kusimama kwenye sehemu yake. Mheshimiwa Waziri ataniambia wanasaidiaje hivi vyuo ambavyo watoto wanaosoma ni Serikali hii hii ili viweze kusimama na kufanya kazi yake kikamilifu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Thea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Chuo chetu cha *SUA* kilikabidhiwa eneo katika majengo ambayo yalikuwa ya *camp* ya waliokuwa wanajenga barabara. Serikali imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli udahili katika chuo hiki cha Tunduru bado haujaanza na kinachokwamisha kuanza udahili pale ilikuwa bado kuna miundombinu ambayo siyo toshelezi. Bado hakuna mabweni pamoja na maabara katika eneo hili. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo chetu cha *SUA* kimepanga kuanza kutoa kozi fupi fupi pale katika eneo letu la Tunduru kwa wakulima wetu kwa lengo la kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao ya korosho, mihogo pamoja na ufuta.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika majengo yale yaliyopo kwa hivi sasa yanatumika kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa wanafunzi wetu wanaosoma Shahada ya Wanyamapori na Utalii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Chuo chetu cha *SUA* kinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutosheleza au kujenga miundombinu ili tuweze kuanza kutoa huduma pale mara tu majengo hayo yatakapokuwa yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, amezungumzia juu ya vyuo binafsi ambavyo vipo katika Kanda hiyo ya Kusini, naomba nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge Serikali imekuwa inafanya juhudi tofauti tofauti kuhakikisha vyuo hivi vinaendelea kutoa huduma. Serikali imekuwa ikifanya yafuatayo kupitia Tume ya Vyuo Vikuu:-

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kama vyuo hivi vinatoa huduma sawasawa na elimu Bora; Tume yetu imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam; na Tumeendelea kutoa mafunzo kwa viongozi pamoja na Wahadhiri wa vyuo hivi. Katika mwaka huu fedha, TCU imeendesha mafunzo ya Wahadhiri pamoja na wamiliki zaidi ya 218 kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinasimama sawasawa. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge. Swali la Mheshimiwa Esther L. Midimu.

Na 211

### **Utaratibu wa Kuwalipa Wakulima wa Pamba**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Ununuzi wa zao la pamba utanza mwezi Mei au Julai.

Je, Serikali inatarajia kuwalipa wakulima watakaouza pamba kwa utaratibu gani kabla ya kuanza kwa ununuzi wa zao hilo ifikapo Mwezi Mei – Julai, 2021?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu wakulima wa pamba wamekuwa wakilipwa fedha za mauzo ya pamba

kwa utaratibu wa fedha taslimu kwa maana ya *hard cash* kupitia Vyama vya Ushirika. Hata hivyo, mfumo huo umekuwa ukisababisha changamoto kwa wakulima ikiwemo wizi na ubadhirifu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya viongozi wa *AMCOS* kwa kutoroka na fedha za wakulima hasa katika msimu ambao ipo changamoto ya uuzaji wa ununuzi mfano msimu wa 2019/2020. Katika kutatua changamoto hizo, Serikali katika msimu wa 2020/2021, imeratibu kwa majaribio mfumo wa kulipa wakulima kupitia akaunti za benki na simu za mkononi (*mobile money*).

Mheshimiwa Spika, mfumo huo umeleta mafanikio ambapo baadhi ya benki ikiwemo *CRDB, NMB, Azania* na *NBC* zimewezesha wakulima kufungua akaunti za Benki bila malipo na baadhi ya akaunti za wakulima kufutiwa tozo ikiwemo tozo za *withdraw*. Aidha, pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto katika matumizi ya mfumo huo kutokana na kukosekana kwa matawi ya benki katika baadhi ya maeneo yaliyo karibu na wakulima. Taarifa za Benki na majina ya wakulima kutofautiana na hivyo kuchangia kukwamisha malipo ya wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta suluhu ya changamoto hizo msimu wa 2021/2022 fedha za wakulima zitalipwa katika kaunti za *AMCOS*, kwa maeneo ambayo hayana changamoto za ukosefu wa ukaribu wa matawi ya benki. Aidha, Serikali itaruhusu kutumia mifumo yote ya malipo ikiwemo mfumo wa malipo wa fedha taslim hususan pale ambapo mazingira hayaruhusu kufanya malipo kupitia benki na mitandao ya simu. Aidha, mfumo wa malipo ya fedha taslim utasimamiwa na *AMCOS* na mnunuzi ili kudhibiti ubadhilifu wowote unaoweza kujitokeza hususan pale ambapo malipo yanapokuwa zaidi ya shilingi 10,000.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza

kabisa nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kutoa pembejeo bure na mbegu bure za pamba. Imeleta motisha kwa wakulima. Hongera sana Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali ya nyongeza mawili. Kwa kuwa, mwaka jana *AMCOS* imechelewesha sana malipo ya wakulima na mpaka sasa...

**SPIKA:** Waheshimiwa, naomba sauti zenu mzipunguze tumsikilize Mbunge.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, niulize maswali mawili sasa. Kwa kuwa *AMCOS*, mwaka jana imechelewesha sana malipo ya wakulima na mpaka sasa kuna baadhi ya wakulima wanadai. Serikali haioni sasa umuhimu wa kuwarudisha wakulima kwenye soko huria ili wauze pamba walipwe *cash*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiwaruhusu wanunuzi ma-*dealers* kuingia sokoni moja kwa moja hiyo itasaidia wakulima kwenda kuuza pamba na kulipwa *cash* halafu itawasaidia vijana wengi kupata ajira kwa vile kuna ukosefu wa ajira. Je, ni nini tamko la Serikali kuhusu kuingia kwenye mfumo wa manunuzi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya hakika kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo. Muuliza swali ni mkulima mzuri wa pamba na ni mfanyabiashara wa pamba pia.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza mfumo wa ushirika ni takwa la Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Hii ni ahadi ambayo wananchi walikichagua Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba tunajenga ushirika. Hili ni jambo la kwanza. Jambo la pili, ushirika ndiyo njia sahihi ya wakulima wadogo wadogo kufanya *aggregation* na kwa kutumia ushirika kama alivyosema kwamba tumegawa dawa

bure, tumegawa pembejeo bure, tumetumia ushirika kufanya namna hiyo. Kwa hiyo, ziko changamoto kama alizosema Mheshimiwa Mbunge. Utafiti umeonesha kwamba kwenye Sekta ya Kilimo ambayo wakulima wake ni wadogo wadogo, tunapoondoa mfumo wa ushirika hasa katika haya mazao makubwa, mara nyingi wakulima hudhulumiwa na wanunuzi. Kwa hiyo, tutatatua changamoto zilizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *AMCOS* ambazo hazijalipa wakulima kama wapo tuletewe majina tuchukue hatua. Hili ni jambo la kwanza na kutokumlipa mkulima ni uhujumu uchumi, wako ambao tumeshawafunga. Kuhusu namna gani tunalipa, tumekaa kikao cha wadau wa pamba, tumekubaliana na nitumie Bunge lako kuagiza mambo yafuatayo kwa kuwa msimu wa pamba tunaanza sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, wanunuzi wanaruhusiwa kupeleka ma-*cashier* wao katika vyama vya msingi na waende na fedha wawalipe moja kwa moja wakulima pale pale kwenye chama cha msingi mahali ambapo hakuna mfumo wa kulipia benki. Hili la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, chama cha msingi ushuru wake utalipwa kupitia benki na wala hautaenda *cash* kwenye chama cha msingi. Lakini tunaruhusu mifumo yote mitatu. Mnunuzi anaruhusiwa kupeleka walipaji wake kwenye chama cha msingi. Kama chama cha msingi A, kuna makampuni matano, makampuni matano yapeleke ma-*cashier* wao pale pale ili mkulima anapofikisha pamba yake alipwe *cash* aondoke na fedha yake na pamba isiondoke kwenye chama cha msingi bila mkulima kupewa fedha yake.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuua mfumo wa ushirika katika hatua hii. Hili ni takwa la kikatiba na tuna sheria ya ushirika. Kama tuna nia ya kuufuta ushirika katika nchi iletwe sheria na Bunge hili hili likiifuta sisi wizara tutaufuta ushirika bila matatizo yoyote. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Hanang wanategemea sana kilimo katika masuala mazima ya uchumi. Lakini katika kilimo hiki tunategemea sana shamba letu kubwa, shamba la *NAFCO* ambalo kwa sasa lina mwekezaji. Shamba lile lina hekari takriban 40,000. Mwekezaji analima asilimia 20 na eneo analoliacha wazi anawanyanyasa sana wananchi. Je, Serikali inatuambia nini juu ya kurudisha shamba lile Serikalini au kuwagawia wananchi ili tuweze kuingiza kipato katika Serikali na kwa mwananchi mmoja mmoja. Ahsante sana kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu waziri Kilimo, tafadhali. Mheshimiwa Hussein Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Halamga na Mheshimiwa Mbunge wa Hanang kwa ufuatiliaji wa eneo ambalo lilibinafsishwa kwa Kampuni ya Ngano *Limited*. Lile eneo kwa mujibu wa sheria alibinafsishiwa huyu bwana na alilinunua. Sisi kama Wizara ya Kilimo pamoja na Waziri wa Kilimo tumekutana naye na wawakilishi wake na tumefanya nao mkutano. Tumewapa *ultimatum* ya mwaka mmoja na wao wanafahamu kwamba wasipotetekeleza makubaliano tuliyoifanya na wao, Serikali itachukua hatua ambazo tumekubaliana nao wao. Kwa hiyo, tuwaombe wananchi wa Wilaya ya Hanang kuweni na Subira. Tumeanza safari ya ngano pamoja na mmeona matokeo na sasa tuwaahidi, tatizo la ngano *limited* linaenda kuisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka nimekuona ulisimama. Swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.



Mheshimiwa Spika, swali lililoulizwa namba 211 linafanana kabisa na wakulima wa Mkoa wa Kagera wanaolima kahawa. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wanunuzi wanaotaka kununua Kahawa kwenye vyama vya msingi. Je, inaruhusiwa? Nilikuwa napenda tamko kutoka kwa Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo. Je, mambo haya yanaruhusiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, vile vile jambo hili limekuwa likifuatiliwa kwa karibu na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Innocent Bashungwa. Naomba nisitoe kauli na hii kauli vyama vya ushirika wa Mkoa wa Kagera kwa maana ya *KDCU* na *KCU*. Niseme tu kwamba wanunuzi binafsi, soko la kununua kahawa, soko la kununua mazao yaliyoko kwenye vyama vya ushirika ni masoko huria. Wanunuzi wanaruhusiwa kwenda kuingia mikataba na vyama vya msingi.

Mheshimiwa Spika, na nitumie kauli hii kuwaagiza *KDCU* na *KCU* wasimzuie mnunuzi yeyote anayetaka kununua kahawa moja kwa moja kwenye chama cha msingi na wala wasiwatishe viongozi wa vyama vya msingi kuwazuia kuingia mikataba na wanunuzi. Mnunuzi aseme bei anayonunulia na kiwango anachonunulia na wawaruhusu kushindania katika *AMCOS level* na wasiwachaji tozo zinazohusiana na *union* kama mnunuzi anaenda kununua kwenye chama cha msingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima. Mheshimiwa Sima Mbunge wa Singida Mjini uliza swali lako.

Na. 212

**Lugha ya Kiswahili Kuwa Bidhaa ya Kimataifa**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa ya kimataifa ili kuendeleza na kukuza utamaduni wetu Duniani.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Habari, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuwa, Serikali imeanzisha mipango kadhaa ya kimkakati ya kukifanya Kiswahili kuwa bidhaa ya Kimataifa. Tayari kanzidata ya wataalam wa Kiswahili imeanzishwa na wataalam 1318 wamesajaliwa. Pamoja na hayo, Serikali imenunua vifaa vya kisasa vya mafunzo ya ukalimani kwa vitendo na matumizi ya *TEHAMA* katika ukuzaji wa Kiswahili ambayo yametumia zaidi ya milioni 181.8.

Mheshimiwa Spika, tayari tunao mpango wa kufundisha Kiswahili kwa wageni kupitia balozi zetu nje ya nchi. Vile vile, Serikali imeboresha na kuimarisha mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni. Pamoja na kutoa machapisho ya Kiswahili rahisi kwa wataalam wetu, na pia kwa lengo la kusaidia nchi zilizoonesha nia ya kuingiza Kiswahili katika mitaala yao ya Elimu mfano Afrika Kusini, Namibia, Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Spika, afua ya hayo, mwaka 2019; wakati wa Mkutano wa 39 wa Wakuu na Viongozi wa Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika-*SADC* Serikali ilifanikiwa kukifanya Kiswahili kuwa moja ya Lugha nne rasmi zinazotumiwa wakati wa vikao na mikutano ya nchi hizo. Naombwa kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sima swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa nchi nyingi sana kama alivyooleza zimeamua kwa dhati kuwa na mtaala wa Kiswahili na ukizingatia pia tunao vijana wengi wabobezi kwenye eneo hili la Kiswahili. Serikali inaweka mkakati gani kuhakikisha vijana hawa wanapata ajira kwenye maeneo hayo ili tusije kuzidiwa na nchi zingine za Jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la misamiati ambayo inatokana na matukio mbalimbali na misamiati hii inaweza kuathiri lugha yetu ya Kiswahili. Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na ongezeko la misamiati hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge amehitaji kufahamu Serikali inajipanga vipi kuwasaidia vijana wetu wapate ajira kupitia lugha hii ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya awali nilieleza kwamba Serikali ilishaanza mazungumza na Balozi zetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje kuhakikisha kwamba hawa wataalam ambao wamezamishwa, wameeleweshwa lugha ya Kiswahili na namna gani wafundishe wageni waweze kushirikiana katika Balozi zetu na madawati hayo yaanzishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia BAKITA tunalifahamu jambo hili na nimesema kwamba tuna wataalam zaidi ya 1318 ambao wapo tayari na tumekuwa tukiwasaidia na wamekuwa wakiwasiliana na BAKITA kwa karibu waweze kupata ajira hizo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Mbunge alitaka kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali inaangalia misamiati inapokuwa imezalishwa ni kwa kiasi gani tunafuatilia kama kuna mabadiliko ya mazingira. Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba Serikali kupitia BAKITA tumekuwa makini sana. Panapotokea mabadiliko yoyote ya kimazingira, ya kieneo au mazingira ya matukio yoyote BAKITA wamekuwa wakitafuta misamiati mbalimbali na kuhakikisha kwamba tunasanifisha misamiati hiyo lakini pia tunachapisha.

Mheshimiwa Spika, mfano, hivi karibuni nchi yetu imekumbwa na ugonjwa wa *Covid* lakini BAKITA tumejidhatiti na tumeshasanifisha *covid – 19* inaitwaje kwa Kiswahili ambayo inaitwa UVIKO – 19. Nitoe rai kwa Watanzania kwasababu tunapenda lugha yetu tuhakikishe tunatumia lugha hii ya Kiswahili badala ya kusema *covid – 19* tunaweza tukasema UVIKO – 19. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa kwasababu ya muda. Mtaona muda uliobakia sio mwingi. Twende Wizara ya Nishati, swali la Mheshimiwa Mbunge wa Njombe Mjini Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika.

Mheshimiwa Deo Mwanyika.

Na. 213

### **Hitaji la Umeme Vijiji na Vitongoji Visivyo na Umeme Nchini**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, ni lini Vijiji na Vitongoji nchini ambavyo havijapatiwa umeme vitapatiwa huduma hiyo.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme nchini (TANESCO) inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini Awamu ya III mzunguko wa pili. Mradi huu unatarajiwa kufikisha miundombinu ya umeme katika vijiji vyote 1,974 ambavyo havijapata umeme kati ya vijiji 12,268 vya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, mradi huu pia utafikisha umeme katika vitongoji 1,474 ambavyo havijafikiwa na umeme. Mradi ulianza mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2022. Gharama ya mradi ni takriban bilioni 1,176.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vitongoji ni endelevu. Serikali kupitia REA na TANESCO itaendelea kupeleka umeme katika vitongoji vyote mwaka hadi mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Moja, baada ya ufuatiliaji wa karibu sana kwenye suala hili imedhihirika wazi kwamba kwa Jimbo la Njombe ni vijiji vinne tu, Mgala, Ngalanga, Mtila na Mbega ndivyo vilivyoingizwa kwenye Mpango ambao Mheshimiwa Naibu Waziri anauongelea. Kuna vijiji takriban 20 ambavyo vimesahaulika, vijiji hivyo ni Hungilo, Uliwa, Utengule, Diani, Makolo, Lugenge, Mpeto n.k. Naomba Serikali itoe kauli kuhusiana na suala hili na iwadhahirishie wananchi wa Njombe kama sasa baada ya maongezi kati yangu, Waziri na REA vijiji vilivyobaki vyote vimeingizwa katika Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Pamoja na vijiji vingi kuunganishwa na hasa kwenye Jimbo letu la Njombe Mjini bado tuna ukatikaji wa umeme mkubwa sana ambao

unaashiria kwamba pamoja na kuunganishwa, tatizo hili litaendelea kuwa kubwa. Tunaomba maelezo ya Wizara kuhusiana na ukatikaji wa umeme katika Mji wa Njombe ambao ni endelevu na hauishi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, zaidi ya vijiji 20 vya Njombe bado haviko katika *REA*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mara ya kwanza vilichukuliwa vijiji vinne lakini baada ya Mheshimiwa Mwanyika kuwasiliana na ofisi na tunamshukuru na kumpongeza kwa ufuatiliaji wake mkubwa, Wizara imeamua iongeze *scope* ya kazi ya awali na kuongeza vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi vilikuwa havikuachwa lakini vilikuwa vimebaki kwasababu viko katika eneo linalokaribiana na mji. Kwa hiyo, vilikuwa havikuingia kwenye mradi wa *REA* lakini tumevichukua tukivi-*treat* kama *peri-urban area*. Kwa hiyo, vijiji hivyo 20, nimhakikishie Mheshimiwa Deo Mwanyika kwamba vimeingia na vitafanyiwa kazi katika awamu hii ya kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, ni kweli. Maeneo ya Njombe yana tatizo kubwa sana la ukatikaji wa umeme. Naomba nitumie muda kidogo tu kukueleza tatizo kubwa tulilokuwa nalo Njombe na hatua taunazozichukua. Njombe inapata umeme kutoka katika kituo chetu cha kupooza umeme cha Makambako na kuna kilometa 60 kutoka pale Makambako mpaka Njombe, Njombe Mji na eneo kubwa la Mkoa. Sasa Njombe tunayo matatizo makubwa matatu.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la kwanza ni baraka ambazo Njombe imezipata ya kuwa na miti mingi sana. Ie miti, pamoja na sisi kufyeka ile *line* ya kupitisha umeme, lakini miti inayokuwa nje ya *line* yetu ya umeme baadaye inaangukia ndani ya *line* yetu kwa sababu inakuwa ni mirefu sana. Kwa hiyo, tumeendelea kufyeka na kuhamasisha wananchi basi hata watuongeze *line* ambayo iko nje zaidi

ya *line* yetu sisi ili tunapofyeka basi miti inayotokea nje ya *line* yao isije ikaleta shida kwenye eneo letu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo linatupa shida sana kwa Mkoa wa Njombe ni radi. Maeneo ya Njombe, kama nilivyowahi kusema hapa, Mkoa wa Kagera lakini pia Mbeya, tunayo matatizo makubwa sana ya radi ambazo zimekuwa zikileta shida kwenye miundombinu yetu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya kwa Mkoa wa Njombe kwa mfano kila tunapofunga *transformer* tunaifanyia *earthing system*. Ile *earthing system* inatakiwa uzamishe chini, lakini unapima udongo kuona *resistance value* ya udongo ni kiasi gani. Kama iko 0 - 60 inakuwa haina shida, kama iko zaidi ya 60 inabidi kutumia zile njia za kienyeji na za kitaalam za ku--*treat* udongo ili radi ikienda iweze kumezwa kule, tunatumia mbolea na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pengine tukifunga *transformer* tunachelewa kuiwasha kwa sababu tukipima *resistance value* ya udongo tunaona bado ina-*resist* sana radi, kwa hiyo, tunaamua kuiacha kwanza ili ipoe kidogo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. Naomba niruhusiwe kutoa nondo kama alizozitoa mwenzangu Ndaisaba jana kwa ajili ya uelewa mzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili tunafunga vifaa vya muhimu sana vinavyoitwa *surge arrester* and *combi unit* kuhakikisha kwamba *transformer* haiharibiki mara kwa mara. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Deo kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba...

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri.  
(Makofi)

Swali la mwisho kwa siku ya leo kwa sababu ya muda ni kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Halima James Mdee kwa niaba yake Mheshimiwa Felista Deogratius Njau.

Na. 214

### **Mkakati wa Mji Mpya – Kawe**

**MHE. FELISTA D. NJAU K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, nini kimepelekea mkwamo wa mkakati wa ujenzi wa Mji mpya wa Kawe kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na lini mradi huo utaendelea?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti, 2013, Baraza la Mawaziri kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, hususani thamani ile ya ardhi katika eneo la Kawe, ilitoa kibali kwa Shirika la Nyumba la Taifa ili eneo hilo ambalo lilikuwa eneo la Kiwanda cha *Tanganyika Packers* liendelezwe kuwa mji wa pembezoni (*satellite town*) na uendelezaji huo ufanyike kwa njia ya ubia kati ya *NHC* na Kampuni ya *Al Ghurair Investments*. Kazi zilizoanza kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa miradi miwili ya makazi na biashara yani *Golden Premier* na *Kawe 711* ambayo kwa sasa imesimama ikiwa imefikia asilimia 43 kwa *Golden Premier* pamoja na asilimia 38 kwa mradi wa *Seven Eleven (711)*.



Mheshimiwa Spika, mkwamo wa utekelezaji wa miradi ya *Golden Premier* pamoja na *Kawe Seven Eleven (711)* umesababishwa na uhaba wa fedha uliotokana na Shirika la Nyumba la Taifa kufikia kikomo cha idhini ya kukopa iliyotolewa na Serikali kabla ya mradi wake kukamilika. Hali hii ilitokana na Shirika kuwa na miradi mingi sana kwa wakati mmoja ambayo yote ilitegemea vyanzo vilevile vya mkopo kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, ili kuikwamua miradi hii, Shirika limefanya juhudi mbalimbali ili kupata fedha kupitia vyanzo vingine zaidi ya mikopo. Hata hivyo, Shirika tayari limeanza mpango huu wa kukwamua kwa kumaliza Mradi wa *Morocco Square*, ambao unakadiriwa kukamilika kufikia mwisho wa mwaka huu 2021. Ukamilishaji wa ujenzi wa mradi wa *Golden Premier* pamoja na *Kawe Seven Eleven (711)* unategemea kuanza katika mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Shirika la Nyumba la Taifa lengo lake kisheria ni kujenga nyumba za kupangisha na kuuza kwa wananchi wa kima cha chini na hii inasababisha wananchi wale kununua kwa bei rahisi. Hata hivyo, Shirika linashindwa kutekeleza jukumu hili kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ambayo inakuwa kwenye vifaa vya ujenzi. Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuondoa hii kodi katika vifaa vya ujenzi kwa shirika la nyumba la Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Ripoti ya *CAG* ya 2019/2020 ilionesha kwamba mradi huu usipokamilika mapema basi Serikali itaingia hasara kwa kulipa Shirika la Nyumba shilingi bilioni 100 na mpaka sasa wakandarasi wanalipwa. Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa

kutekeleza mradi huu ili kuepuka hasara hii ya Taifa ambayo inaenda kuingia?

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kuweza...

**SPIKA:** Aahaa, tayari maswali mawili. (*Kicheko*)

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu Naibu Waziri, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Angeline Mabula, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda hautoshi, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu sheria ilipitishwa Bungeni humu aangalie malengo mazima ya uanzishwaji wa Shirika la Nyumba. Mbali na hilo alilolisema, lakini kwa sasa Shirika la Nyumba halipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini na hivyo ni shirika linalojiendesha kibiashara. Kwa hiyo, katika miradi linayofanya kuna kujenga zile nyumba za gharama nafuu ambazo watu wananunua na wengine wanapanga, lakini pia linakuwa na miradi ya kibiashara ambayo inaliongezea pato Shirika ili kuweza kupanua miradi na kuweza kuongeza wigo wa kupata pesa kwa ajili ya kuendelea kujenga. Kama sasa hivi hapa Dodoma wana mradi wa nyumba 1,000 ambao wanaendelea kujenga nazo ziko katika viwango tofautitofauti.

Mheshimiwa Spika, ameongelea suala la kuondolewa kwa VAT kwa Shirika la Nyumba. Naomba niseme tu, katika suala zima la ujenzi ni mashirika mengi ambayo yanafanya kazi hizi za ujenzi ikiwemo *Watumishi Housing*. Kwa hiyo, unapozungumzia suala la kuondoa VAT, *Watumishi Housing* nao wanajenga nyumba kwa ajili ya wafanyakazi, sasa huwezi ukasema unaondoa VAT wakati haya mashirika yote yanafanya huduma ileile ya ujenzi wa nyumba kwa ajili ya

kuboresha makazi kwa watu wetu. Kwa hiyo, hili kama linaonekana kwamba ni tatizo basi nadhani ni jambo la kuangaliwa upya, lakini kwa sasa bado VAT itaendelea kutozwa kama ambavyo inaendelea, japokuwa kama Wizara tulikuwa na mpango awali wa kuangalia namna bora ya kuweza kuliwezesha Shirika kwa kuangalia pia katika suala hilo la VAT, lakini bado mchakato haujafikia mwisho wake kwa sababu ya hali halisi ya ushindani na mashirika yanavyofanya kazi kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, anaongelea suala la utekelezaji wa mradi ule kwamba unapata hasara na CAG ameonesha. Kwenye jibu langu la msingi nimesema ya kwamba kwa sasa tumepanga mradi huo utaendelea na ujenzi katika mwaka wa fedha huu 2020/2021 kwa sababu kubwa tu kwamba mradi wa *Morocco Square* ambao unaendelea mpaka sasa na tayari umefikia kwenye asilimia 92 ukikamilika ule tayari unaongeza vyanzo vya pesa kwa ajili ya ku-*subsidize* matumizi katika ujenzi ule. Pia tunayo *Victoria Palace* ambayo ina *unit* 88 lakini pale tayari 86 zimeshanunuliwa. Kwa maana hiyo ni pesa inayoingia kuliwezesha Shirika mbali na kutegemea mikopo basi pia kutoka katika vyanzo vya ndani vya miradi yake ya uwekezaji vitaenda kusaidia kuweza kukamilisha mradi ule ili kuweza kuboresha mji ule ambao uko katika eneo ambalo ni *very prime*.

**SPIKA:** Pamoja na muda kuwa kushoto lakini yuko Mbunge wa Jimbo la Kawe, Mheshimiwa *Bishop Gwajima*, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninalo swali kidogo la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kukamilika kwa Mji Mpya wa Kawe utaongeza shughuli za kijamii kwa wananchi wanaokaa kwenye eneo la Kawe, hasa Mzimuni, Ukwamani na maeneo mengine. Kukamilika kwa Mji Mpya wa Kawe ni kiashiria cha Kawe yetu ijayo kuwa wilaya. Je, ni lini hasa Mji Mpya wa Kawe utakamilika? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi sana, lini hasa Mji wa Kawe utakamilika? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumjibu Mheshimiwa Askofu Gwajima swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa sababu baada ya kuingia tu Bungeni amekuwa akifuatilia sana mradi ule ili kuweza kuona unakamilika lini ili uweze kupendezesha maeneo yale. Azma ya Serikali hata ilipohamishia Makao Makuu hapa Mji wa Dar es Salaam ulibaki kama mji wa kibiashara. Kwa hiyo, lengo letu kama Serikali pia ni kuhakikisha kwamba mradi ule unakamilika ili ile maana halisi ya kufanya Dar-es-Salaam kuwa mji wa kibiashara na Kawe kuonekana kama *satellite town* ambayo tumekusudia kuifanya hivyo tumesema mwaka wa fedha unaokuja mradi ule utakwenda kukamilishwa. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi Mheshimiwa Wizara iko makini katika hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Wakati huu wa bajeti muda wetu wa maswali ni saa moja tu, kwa hiyo, huwa tunapenda maswali mafupi, majibu mafupi, maswali ya nyongeza mafupi. Tunakuwa na maswali 10 kwa hiyo, katika muda wa saa moja inakuwa kidogo ni *pressure* kwa pande zote.

Sasa naomba niwatambue wageni wetu na matangazo mengine muhimu, kama ifuatavyo:-

Ninaye Dkt. Sam Atandi, *yes*. Huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, ni Mshauri Mwelekezi wa Masuala ya Fedha, Uwekezaji na Uwezeshaji kutoka Nairobi, nchini Kenya. Karibu sana jirani. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni tisa wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

kutoka *Tanzania Women Chamber of Commerce* wakiongozwa na Mwenyekiti Grace Oneya. Mnawaona wageni wetu, muendeleo kusimama kwanza kutoka *Tanzania Women Chamber of Commerce*, malkia wa nguvu ninyi, karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa watakuwepo nasi na siku ya Jumapili ni siku ya mwanamke mfanyabiashara. Watakuwa na shughuli maalum pale *Dodoma Hotel*, tunawaalika wanawake wote muweze kujiunga nao pale *Dodoma Hotel* kwa ajili ya event hiyo. (*Makofi*)

Najua wengi wenu mnafanya biashara na wale ambao hamfanyi biashara mna nia ya kufanya biashara. Biashara ndiyo hatima ndugu zangu au siyo? Kwa hiyo, nawaombeni siku ya Jumapili wale mtakaokuwa *Dodoma* basi mujiunge na *chamber* hii ya wanawake muweze kujifunza fursa mbalimbali na nini mnaweza mkafanya katika biashara. Wapo hapa kwa ajili yenu, karibuni sana wapendwa. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Deogratius Ndejemi, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambaye ni Rais wa Chama cha Wauza Viungo (*Spices*) *Tanzania*, sio viungo vingine, kutoka *TASPA* Jijini Dar Es Salaam, Ndugu Edward Rukaka. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jerry Slaa ni viongozi wa Bunge la Wanafunzi la Chuo cha *IFM* kutoka kule *IFM* Dar-Es-Salaam, Ndugu Ezekiel Mollel (Spika), Ndugu Lilian Simpson (Naibu Spika) na Ndugu Said Makala (Katibu wa Bunge). Karibuni sana, Spika Mollel yuko wapi, karibu sana mjengoni, lakini usiwe na tamaa sana bado nipo-nipo kwanza. Karibuni sana. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni kumi wa Mheshimiwa Omar Ali Omar ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha *Dodoma (UDOM)* wakiongozwa na Ndugu Rashid Ali Rashid. Karibuni wageni wa *UDOM*, karibuni sana wapendwa. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambaye ni mpiga kura wake kutoka kule Kilolo, Ndugu Santina Msungu. Karibu sana Santina. *(Makofi)*

Wageni 51 wa Mheshimiwa Samweli Xaday ambao ni Kamati ya Siasa ya Wilaya na Baraza la Madiwani kutoka Hanang, Mkoani Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya Mathew Darema. Wale wa Hanang, aah, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani wa Hanang na Mbunge wenu yupo anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Kipekee katika kundi hilo naomba niwatambue na wasimame, Mheshimiwa Thomas William na Mheshimiwa Isaya Mwashu. Hawa ni Madiwani wa kutoka CHADEMA ambao wanafanya kazi nzuri sana kule Hanang ya maendeleo, wao hawana siasa za kijingajinga, hongereni sana. Muendeleo kuchapa kazi nzuri ya kujenga nchi yenu, tunatambua mchango wenu, mnatoa mfano bora kabisa wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Simon Songe ana wageni wake ambao ni walimu kutoka Jimboni Busega, Ndugu Salige Benjamin, Ndugu Beatrice Gunje na Liberatus Ntilema. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ni wasanii wa filamu wakiongozwa na Ndugu Welu Sengo. Karibuni popote pale mlipo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ni Ndugu Daniel Muro ambaye ni ndugu yake kutoka Las Vegas Nevada, Marekani. Karibu sana pale ulipo. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wapiga kura wake kutoka VETA Dodoma, Ndugu Elibariki Njiku na Ndugu Michael Celestine. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*

wakiongozwa na Ndugu Bahati Daud. Wageni wa *UDOM*, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa John Pallangyo ambao ni wapiga kura wake kutoka Arumeru Mashariki wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Ndugu Jeremia Kishili. Karibuni sana kutoka Arumeru. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Noah Lemburis ambao ni wapiga kura wake kutoka Arumeru Magharibi, Ndugu Rsau Sikawa na Ndugu Naftal Sikawa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambao ni jamaa zake kutoka Mkoani Arusha wakiongozwa na Dkt. Kaanarli Ayo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Naomba niwatangazie Wabunge Wanawake (*TWPG*) wote kuwa tarehe 8 na 9 kuanzia Saa 03.00 asubuhi kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge wanawake wote Ukumbi wa Msekwa.

Sasa nina matangazo mengine mawili muhimu. Tangazo la kwanza ni kwamba, tuliagiza Ripoti ya *CAG* ianze kufanyiwa kazi na Kamati ya *LAAC* na Kamati ya *PAC* na ratiba yao itaendelea kama tulivyokubaliana nao, wao wanajua. Katika Taarifa ile ya *CAG* ya mwaka 2019/2020 yako mashirika ambayo hayakuwa yameandaa hesabu zozote kwa maana ya *CAG* kuzikagua hesabu hizo.

Kwa hiyo, hakuna Taarifa ya *CAG* inayokwenda kwenye Kamati ya *PAC* kutoka katika mashirika hayo. Sasa huu ni uzembe wa hali ya juu kwa shirika kukosa hesabu zinazokaguliwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naagiza Kamati ya *PAC* kuyaita mashirika haya kwa ratiba mtakayojiwekea haraka sana ili yaje yajieleze ni kwa nini hawakuwa kabisa na hesabu za kuweza kukaguliwa. Muwaite uongozi na Menejimenti, ikiwemo na

Wenyeviti wao wa Bodi, kama hawana sababu za maana tutatoa ushauri kwa Serikali ikiwezekana Bodi zao zivunjwe. *(Makofi)*

Mashirika hayo ni pamoja na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, hawakuwa na hesabu, MOI hawakuwa na hesabu za kukagulika. Cha ajabu kabisa *TANESCO*, shirika kubwa namba moja Tanzania nzima halina hesabu za kukagulika. Wengine ni *TMX, UTT, TFC (Fertilizer Company)*, Posta na kwa maajabu makubwa Shirika la Reli (*TRC*) na wapo wengine ambao sikuwataja. Kwa hiyo, muwaite haraka hawa waje wajieleze, ni hatari kabisa kwa mashirika makubwa kama haya yanakuwa shaghalabagala kiasi kwamba hawana hesabu zinazokagulika na *CAG*. *(Makofi)*

Natoa onyo kwa mashirika mengine yote wakati wa *CAG* kukagua hesabu zao baada ya Septemba ile Mosi, wawe tayari na hesabu zinazokagulika. Tunawalaumu sijui halmashauri, wenye vihesabu vyenye Hati zenye Mashaka na kadhalika wakati kuna mashirika makubwa hata hesabu hawana, sasa hiyo haiwezekani tukaenda namna hiyo. Kwa hiyo, *PAC* mfanye kazi hii na mtupe majibu ili tuweze kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

La pili, nilitoa ruling hapa naomba niirudie tena, maana wengine wanafikiri Spika akiongea hapa ni masihara. Spika anaongoza Bunge kwa kufuata kanuni, katiba, sheria, utaratibu, utamaduni na maamuzi ya Maspika wengine. Maamuzi ninayotoa hapa ni maamuzi ambayo yatumika nami na hata watakaofuata baada yangu. *(Makofi)*

*Ruling* niliyoitoa na ninairudia, maana wengine wanauliza Ndugai wewe ni nani? Suala siyo Ndugai, suala ni Spika. Narudia tena ili wanielewe vizuri, kwa sababu hivyo ndivyo itakavyokuwa. Hatulumbani hapa, siyo masuala ya kulumbana. Hii itatumika sasa na hata siku zijazo.

Kwa vyama vyovyote vyenye kufukuza Wabunge ambao ni wanachama wao kwa kutumia dirisha la uanachama wao; wanawafukuza watu ambao hao



wanaowafukuzwa ni Wabunge, wanapaswa wanapomwandikia barua Spika ambayo ni busara pia kumnakilia Msajili wa Vyama vya Siasa, lakini hata asipopoleka huko, siyo neno lakini ni busara kufanya hivyo, lazima barua hiyo iambatane na katiba yao, iambatane na muhtasari au mihtasari ya vikao vilivyohusika katika kuwafukuza Wabunge hao.

Kwa kufanya hivyo inarahisisha kazi yangu ya kutenda haki ili kuweza kuona: Je, kweli haki imetendeka? Kabla nami sijaweka baraka zangu, nisije nikawaonea watu kwa sababu ambazo hazina mbele wala nyuma. Katika kufanya hivyo, wajue lazima nitashirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa. Sasa kama sina hivyo viambatanisho, hivi mimi nitajuaje hiyo Kamati kuu ndiyo Kamati Kuu ya Chama fulani? Anayejua ni Msajili.

Sasa lazima nipate nakala zile niweze kuona ili niwaite na hao Wabunge husika niwaambie, jamani ninayo maandishi hapa yanayosema kuna hiki na hiki na hiki, mnasemaje? Ili nao wajitete mbele yangu, niweze kutoa uamuzi. (*Makofi*)

Vinginevyo haiwezekani tu kwa sababu eti fulani anataka jambo fulani halafu ikawa; haiendi hivyo, ni masuala ya haki. Masuala ya haki yanataka utaratibu ulionyooka. Hili litatumika kwangu na kwa Maspika wanaofuata. Anayeandika aambatanishe vitu hivyo. Katiba hizi zinabadilika badilika, unilettee katiba ambayo ndiyo inayofanya kazi wakati huo. Ndiyo maana nikasema ile ambayo ili-*prevail* uiambatanishe pale.

Kwa hiyo, wale wenye nia hizo, mnaogopa nini kuambatanisha hizo nakala za vikao vyenu? Kwa nini mnafichaficha? Kuna nini ndani yake? Mbona ni jambo rahisi tu! Mnanilettee, mimi nafanya kazi yangu, wala haina shida.

Baada ya matangazo hayo mawili, sasa Katibu tuendeleee.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA YA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI  
KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Leo ni Wizara ya Maji tunaendelea nayo ambayo pia tutaendelea nayo kwa siku ya tatu kwa sababu ya umuhimu wake, siku ya Jumatatu. Kwa sababu ya *nature* ya mambo yalivyo na hali halisi na kuna mambo mengi yanaendelea, nimeombwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi, tumalize saa saba kwa leo. Kwa hiyo, wale wa CCM tumekubaliana watachangia kwa dakika tano tano ili na wengine wapate nafasi siku ya Jumatatu. *(Makofi)*

Kwa mwongozo huo sasa, naendelea nanyi, naomba mchangiaji yeyote awepo kwa sababu nikitaja jina lako, haupo, sitahirudia tena, maana yake mpo wengi. Tunaanza na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake kuu. Pia nianze na nukuu, wakati nachangia Wizara hii ya Maji Maandiko Matakatifu ya *Quran* sura ya 21 aya ya 30 ambapo Mwenyezi Mungu anasema: *“Wajaalna minalmaa-i kulashai-in-hayaa.”* Tumejaalia kutokana na maji kuwa ndiyo chanzo cha uhai wa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maandiko haya matakatifu tafsiri yake ni kwamba Wizara ambayo anaisimamia Mheshimiwa Jumaa Aweso na timu yake ndiyo uhai wetu sisi na viumbe vingine. Kwa maana hiyo, ni Wizara ambayo ni tegemeo kubwa la maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa *spirit* hiyo hiyo, mimi binafsi sina shaka kabisa na kiongozi wa Wizara hii Mheshimiwa Jumaa Aweso, sina shaka kabisa na Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Eng. Maryprisca, sina shaka na Katibu Mkuu, ndugu yangu Eng. Sanga; Naibu Katibu Mkuu pamoja na timu yote ya Wizara, wapo sawa sawa. Hata meneja wangu wa *RUWASA* katika Wilaya ya Kilwa Eng. Ramadhani Mabula yupo sawa sawa na tunakwenda naye vema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa imani tuliyojenga kwenu Wizara ya Maji, nitumie fursa hii kutoa ushauri ufuatao: kwamba kama ilivyo katika umeme, Wizara ya Nishati imekuwa na jukumu na juhudi za kutafuta vyanzo vya umeme kila *angle* na maji kadhalika mtafute vyanzo vya maji kila *angle*; katika chemichemi, katika mito, mabwawa, maziwa, maji ya ardhi kwa maana ya *underground water* na maji ya vyanzo vya asili.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, niseme tu kwamba kuanzishwa kwa *RUWASA* miaka miwili iliyopita kumeleta matumaini makubwa kwa Watanzania, lakini ukiangalia mwenendo na utendaji kazi wa *RUWASA* ni kama vile unaleta tija zaidi kwenye miradi mikubwa mikubwa na hususan kwenye vyanzo vikubwa vya maji hasa Maziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule vijijini ambako hatutegemei sana kupata maji kutoka vyanzo vikuu, kidogo nitoe ushauri. Kuna Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa (*DDCA*), miaka miwili iliyopita nahisi ufanisi wake wa kazi umepungua. Nadhani kuanzishwa kwa *RUWASA* kumeifanya *DDCA* isiwe mamlaka kamili au wakala kamili, ni kama *unit* tu hivi ndani ya Wizara. Nashauri kupitia Bunge lako kwamba *DDCA* ipewe nguvu kamili. Ilikuwa na waatam wa kutosha, ilikuwa na mitambo ya kutosha. Tulikuwa tukiona magari yakipita na *ma-drill* yakipita na *ma-compressor* kwa ajili ya kwenda kuchimba visima vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Itilima atakuwa mfano moja wapo wa kutoa ushuhuda huo, kuna visima vingi

vimechimbwa na *DDCA* na ilikuwa na uwezo wa kuleta mapato takribani shilingi bilioni 12 kwa mwaka. Haya siyo mapato madogo. Tuitathmini miaka miwili iliyopita kwa mwaka 2021/2022 kiasi gani cha fedha kimepatikana kutoka wakala wa huu. Kimeweza kuchimba visima vingapi katika vijiji vyetu?

Mheshimiwa Spika, nashauri *DDCA* ipewe nguvu na mamlaka kamili, Wahandisi wale ambao walikuwa ni washauri wa kitaalam, wako wapi sasa hivi? Mitambo ile iko wapi na iko mingapi na inafanya kazi gani? Nitoe kama hadidu za rejea kwa Waziri akaifanyie kazi ikiwezekana aunde Tume au kikosi kazi mahsusi cha kutathmini utendaji kazi wa *DDCA* kama kuna upungufu uboreshwe kwa lengo la kusaidia hususan visima vijijini.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo nikumbushe Wizara ya Maji; katika Wilaya ya Kilwa hususan Jimbo la Kilwa Kusini, tarehe 15 Septemba, 2009 aliyekuwa Waziri ya Maji wakati huo Mheshimiwa Mwandosya aliahidi kuchimba bwawa katika Kijiji cha Limaliyao, ambapo bwawa lile lingechimbwa lingeweza kusaidia upatikanaji wa maji kwa watu takribani 15,000. Naikumbusha Wizara ikafanyie kazi. Tangu agizo lile la Waziri, hakuna ambacho kimefanyika mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Jumaa Aweso ndugu yangu, ninaimani na timu yake, atume wataalam wake wakafanyie kazi kutafuta eneo ambalo tunaweza tukapata bwawa kwa ajili ya maji ya Wana-Limaliyao, kwa sababu hawataweza kunufaika na mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo chochote cha mto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikishauri hivyo pia, niendeleo kuishukuru na kuipongeza Wizara. Nimeona kupitia kitabu cha bajeti kwamba katika vijiji vyangu kadhaa nitapata miradi ikiwepo Kilwa Kisiwani, nashukuru sana. Pia ikiwemo Likawage, nashukuru sana; pia ikiwemo na Kiu, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, ahadi yake ya kunisaidia kisima cha maji katika Kijiji cha Nainokwe, naomba itekelezwe kupitia mpango huu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, pia mpango ule wa miji 28, ukumbuke na Mji wa Kilwa Masoko na Mji wa Kilwa Kivinje.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinga. Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, nilishakutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Tunza na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ajiandae.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Maji. Kwanza kabisa nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni matumaini ya Watanzania. Mheshimiwa Aweso unafanya kazi nzuri pamoja na Naibu wako.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wangu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama. Haijawahi kutokea mwanamke kuwa Mwenyekiti wa Taifa. Wanawake tunajivunia hilo, Mheshimiwa Rais ametuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dharti ya kumtua mama ndoo kichwani, ni mwanamke mwenzetu, shida zote zitaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee mradi wa Ziwa Victoria. Toka mwaka 2010 tunaongelea mradi huu, tunaomba maji kutoka Ziwa Victoria, hatimaye Serikali yetu

sikivu ikatusikia, ikakubali kutuvutia maji kutoka Ziwa Victoria kuleta Mkoa Simiyu. Nilishawahi kusimama mwaka juzi kuuliza swali hapa kuhusu mradi huo utaanza lini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa kipindi kile alinipa majibu mazuri akasema mradi huo utaanza na Wilaya tatu; utaanza na Busega, Bariadi na Itilima, lakini hadi sasa hakuna kitu kinachoendelea. Baadaye wakati wa kampeni, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli wakati anafanya kampeni zake alisema Mkoa wa Simiyu tayari wameshatenga shilingi bilioni 800 kwa ajili ya kuvuta maji kuleta wapi Mkoa wa Simiyu kutoka ziwa Victoria, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

Naiomba Serikali yangu Sikivu, kwa vile inasema hizo fedha imetupa, itoe sasa mradi uendeleee. Mradi huo utainua uchumi wa Simiyu na Mikoa ambayo ni ya pembezoni mwa Simiyu. Kwa sababu wanawake wa Mkoa wa Simiyu ni wakulima wazuri, wachapakazi, tutalima kilimo cha umwagiliaji, tutalima mboga mboga na matunda, tutauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali ni kuwa na uwanja wa ndege kila Mkoa. Simiyu tumetenga tayari eneo la uwanja wa ndege, nina imani utajengwa na ndege zitatu, tutasafirishva mboga mboga kwenda nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maji waathirika wakubwa ni akina mama. wanaume muda mwingi nyie mmepumzika, mmelala tu, sisi tunakwenda kutafuta maji, tukirudi ndani tunapika. Ninaomba Serikali ibaini sasa maeneo ambayo yana shida na hali mbaya kabisa ya maji, ichimbe visima vidogo vidogo kwa sababu tunaoathirika ni sisi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleee kuishukuru Serikali yangu na kuipongeza kwa mradi mkubwa wa maji wa Lamadi ambao umejengwa kwa shilingi bilioni 12.8 na unahudumia vijiji vitatu; Kijiji cha Lamadi, Kijiji cha Lukungu na Kijiji cha Mwabayanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, bado kuna vijiji vingine vina uhitaji zaidi, hawana maji kabisa; Kijiji cha Mirambi na Mwanhari. Wilaya ya Meatu ina shida kubwa sana, haina maji kabisa na wanawake wa kule wanahangaika sana. Muda mwingi wanaupoteza kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. Halafu jiografia ya Meatu ni mbaya sana, maeneo yale yana ukame sana, hata kama maji yakichimbwa kule chini unakutana na magadi, unakutana na maji ambayo hayafai katika matumizi ya binadamu.

Naiomba Serikali ifanye utaratibu kila mwaka itenge fedha iwe inachimba hata mabwawa mawili mawili wapate maji watu wa Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna bwawa la Mwanjoro huko huko Meatu. Kipindi kile Mheshimiwa Rais wa sasa wa Awamu ya Sita alikuwa Makamu wa Rais, alikwenda kulizindua. Sasa hivi limejaa tope. Naiomba Serikali yangu itoe fedha hilo bwawa likarabatiwe, kwa sababu linahudumia vijiji vitano ili wanawake waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji Mkoa wa Simiyu asilimia 60.3 Wilaya ya Meatu, asilimia 62 Wilaya ya Maswa, asilimia 69.2 Wilaya ya Itilima na asilimia 50.8 Wilaya ya Busega. Upatikanaji wa maji bado upo chini, tunaomba Serikali itulettee fedha ili tuchimbe visima virefu viweze kusambaza maji. Bahati nzuri kwa Simiyu tuna Meneja mwana mama mchapakazi, anachapa kazi, ni mtu mzuri, yeye anasubiri fedha tu aweze kusambaza maji kila kona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, ubarikiwe sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Lukago Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Kama hakuna maji huko Simiyu, hamieni Dodoma. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sisi sote kuwa hai na kukutana kwenye Bunge hili leo. Maji ni uhai. Sisi watu wa Mtwara nafikiri katika mikoa ambayo inaongoza kutokuwa na maji ya uhakika ni pamoja na Mkoa wa Mtwara. Leo ninataka niongelee mambo muhimu matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, naishauri Serikali, sehemu ambapo maji yanaanzia au yanakotoka kama ni kisima, kama ni mto, kama ni bwawa muanze kuwapa huduma wale halafu yaendeleo sehemu nyingine. Kumekuwa na changamoto kubwa sana, unakuta chanzo cha maji kipo pale, wameweka mabomba lakini maji yanakwenda kupatikana sehemu nyingine na wale watu ambao wanaishi pale kwenye kile chanzo cha maji hawapati maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Manispaa ya Mtwara Mikindani, kuna Kata moja inaitwa Naliendele. Kuna mradi mmoja wa maji unaanzia Mtaa wa Mbawala chini, huko mbawala chini wenyewe wanaona mantenki, wanaona mabomba lakini hawapati maji. Ile inakatisha tamaa. Mradi ule pia nimeona umezungumzwa kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu unasuasua, tunaomba ukarekebishwe ufanya kazi vizuri kama alivyoandika kwenye hotuba yake ili kusudi wananchi wale wapate maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine huduma ya maji ni huduma lakini kwa wakati mwingine ni biashara. Kumekuwa na masuala ya kusuasua sana, wananchi wanalalamika sana, mtu anakwenda Idara ya Maji, wanamfanyia tathmini analipia, lakini kuja kuunganisha maji inachukua muda mrefu. Vifaa hakuna, mita hakuna, mabomba hakuna.



Mheshimiwa Spika, unapotaka kufanya biashara wakati unatoa huduma ni lazima ujidhatiti. Kwa hiyo, suala hili nalo pia katika Manispaa ya Mtwara Mikindani lipo, watu wanalipa lakini wanachelewa kuunganishiwa maji kwa sababu ya ukosefu wa vifaa. Tunaomba wenye mamlaka walifanyie kazi kwasababu tumeongea sana. Ukiona nakuja kuongea huku Bungeni, nimeanza kuongea kwenye Baraza la Madiwani. Tunaomba lifanyiwe kazi ili mtu akilipa fedha yake anataka huduma ya maji, basi apatiwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine la mwisho kubwa ninaliongelea ni mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma kuleta katika Manispaa ya Mtwara Mikindani, mradi huo ukipita katika baadhi ya Vijiji vya Jimbo la Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama unakumbuka nilikuwepo kwenye Bunge lililopita. Huu mradi kuandikwa kwenye hotuba za Waziri umeandikwa sana, lakini haujawahi kutekelezwa kwa hatua yoyote. Hata leo Mheshimiwa ameuandika, nimeuona na nimeusoma. Ameandika kwamba huu mradi umetengewa shilingi bilioni sita; shilingi bilioni moja kutoka Serikali yetu ya Tanzania na shilingi bilioni tano kutoka Benki ya Afrika. Ombi langu kubwa tunaomba sasa isiwe historia.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kubwa, tunaomba sasa isiwe maneno matupu, huu mradi uende ukafanyiwe kazi na sisi watu wa Mtwara tunatamani tupate maji safi ya baridi na salama. Kwa mfano sasa hivi ukija Manispaa ya Mtwara Mikindani maji tunapata hatuwezi kumkufuru Mungu tukasema maji hatupati, maji tunapata, lakini Mheshimiwa Waziri anayajua ladha ya yale maji, akasema ili tutatue tatizo la maji ni lazima huu Mradi wa Mto Ruvuma ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, huu Mradi wa Mto Ruvuma ni mradi mkubwa na naamini ukifanyiwa kazi utakwenda kutatua changamoto ya maji kwenye majimbo mbalimbali ya Mkoa wa Mtwara ikiwemo Mtwara Manispaa, Mtwara Vijijini, Nanyamba, Tandahimba na Newala kule Nanyumbu huu mradi utakwenda kufanya kazi kwa sababu wananchi

wa Mkoa wa Mtwara walio wengi ukiacha Mtwara Mjini na hizi sehemu kidogo za mjini hawajui kufungua maji bombani.

Mheshimiwa Spika, *RUWASA* wanasema maji bombani sisi kule kwetu tunasema maji ya kuokota. Mtu unasubiria mvua inyeshe yale yanayotiririka chini ndiyo yaingie kwenye kisima. Watu kila siku wanaumwa matumbo, watu wanaumwa *typhoid* kwa sababu ya maji ya kuokota. Sasa leo sitaki kuongea sana Mheshimiwa Waziri ameandika mradi huu na hii siyo mara ya kwanza kuandika, naomba kwa heshima na taadhima, mradi huu uende ukafanyiwe kazi. Ni bora afanye mradi mkubwa hata ikiwa kwa awamu, lakini ukiisha unakwenda kutatua changamoto kubwa ya maji ambayo inaukumba Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, naishi Mtwara na najua ukipita Mtwara unakuta mashimo yanayoitwa visima, kama mtu hujazoea unaweza ukashangaa. Tunataka nasi tuvute maji majumbani kwetu yaliyo safi na salama ili kusudi tuweze kuishi kama Watanzania wengine, tunalipa kodi kubwa sana kwa nchi hii, tunaongeza pato la Taifa kubwa sana kwa nchi hii kwa sababu sisi tunazalisha korosho ambayo ni *among of the big five cloves* zinazoleta pesa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naamini nimesikika na nimeeleza yale yaliyoko moyoni kwangu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Issa Malapo kwa kuleta hoja za kusini mwa nchi yetu. Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

**MHE. DKT STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mezani ya Wizara yetu ya Maji. Nitangulize kwanza pongezi zangu za dhati kwa Wizara hii kwa jinsi ambavyo wamedhihirisha kwa matendo uchapakazi wao katika kupunguza kero ya maji nchini. Kwa kweli

wamefanyakazi kubwa na nielekeze pongezi za kipekee kwa Waziri wetu Mheshimiwa Aweso pamoja na timu yake yote, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa sababu kwa kweli tumeona matokeo ya kazi yao. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu ya uhaba wa muda, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye baadhi ya dondoo nilizotoa katika hotuba yake. Ukiangalia kiambatisho namba moja miradi 355 ya maji vijijini ambayo imekamilika katika mwaka wa fedha unaoisha ambayo iko katika ukurasa wa 91, Wilaya ya Longido nayo imepata miradi miwili ambayo imekamilishwa. Moja uko Kijiji cha Noondoto na mwingine ulikuwa Kijiji cha Magadini. Naomba kwa hii miradi niishauri Serikali kwamba inapomaliza miradi na kuiachia jamii ambayo haijaelimishwa, Kamati za Maji hazijui wajibu wake hii miradi itarudi tu kuharibika na tutakuwa tumefanya kazi bure.

Mheshimiwa Spika, kwa huu wa Noondoto naomba niishauri Serikali kwamba kuna upungufu. Ule mradi wa kutoa maji juu ya Mlima Kitumbeine kupeleka mpaka Kitongoji cha Ordoko ulihitajika uwe pia na tenki la maji, hakuna tenki la maji pale. Kwa hiyo naomba huo upungufu ukazingatiwe. Naomba nishukuru kwa kule Magadini maji yaliyotoka juu ya Mlima Gilayi yamefika mpaka Shule ya Msingi ya Magadini na inaonekana kwamba ule mradi umekamilika kwa asilimia 100, naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, nilipoangalia kiambatisho namba tatu kwenye miradi 67 ya maji iliyokamilika katika maeneo ya mijini, ukurasa wa 130 nikaona kwamba Longido nayo ni miongoni mwa wilaya ambazo zimeguswa na hiyo miradi na ule mradi wa maji safi na salama kutoka Mlima Kilimanjaro uliogharimu zaidi ya bilioni 15, uliweza kusambazwa katika mji wetu wa Longido. Upungufu kidogo upo kwa sababu bado pia kuna nyumba nyingi hazijasambaziwa maji.

Mheshimiwa Spika, naomba pia katika kuendelea kusambaza maji majumbani hilo lizingatiwe maana pale Longido sasa hivi tukitaka kuoga baada ya *breakfast* wakati

wa *lunch* na wakati wa chakula cha jioni tunayo maji ya kutosha, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano na Awamu ya Sita kwa sababu Longido ni moja ya Wilaya kame nchini, lakini sasa shida hiyo imekuwa ya historia katika maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nipende pia kuishukuru Serikali kwa sababu mradi ule, yale maji ni mengi pale Longido, umeanza kuelekezwa Mji wa Mpakani Namanga na utakapofika Namanga tutakuwa tumetimiza ahadi ya Hayati ya Dkt. John Joseph Magufuli aliyotoa alipokuja kuzindua ule mpaka wa pamoja, akawaahidi watu wa Namanga kwamba maji ya Kilimanjaro lazima yafike mpaka Namanga. Napenda pia kutoa hizo shukrani.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia katika kiambatisho namba 4a, kipo katika ukurasa wa 132, maji vijijini mradi ambao utatekelezwa katika huu mwaka wa fedha tunaoadili bajeti yake. Naishukuru sana Serikali kwa sababu kuna miradi saba imeorodheshwa inaenda kugusa Wilaya yangu ya Longido na ambayo itatupatia jumla ya shilingi bilioni 2.08 ambayo naamini tukiisimamia vizuri Vijiji hivi vya Leremeta, Olmolog, Orkejuloongishu, Lopolosek, Ermanie na Vijiji vingine kama Kiseriani, Meirungoi, Elangadabash, Lerangwa na Olmolog watakwenda kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa sababu hivi vijiji vina shida kubwa ya maji, lakini niombe pia Serikali iangalie katika yale maeneo ambayo nilitaja jana kwenye swali langu...

**SPIKA:** Watu wangu wa *Hansard* sijui watapata hivi vijiji sawasawa? Endelea Mheshimiwa Kiruswa (*Kicheko*).

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Olmolog, Kijiji cha Orkejuloongishu, Lopolosek, Ermanie Kiseriani, Meirungoi, Elangadabash, Lerangwa na vijiji vingine vingi kuna zaidi ya shilingi bilioni mbili ambayo Serikali ya Awamu hii ya Sita imetutengea ili tukajaribu kupunguza kero ya maji.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishauri Serikali na kuiomba kwamba yale maji ya bomba la Mto Simba basi yakasambazwe nayo sasa yale matawi yafike Vijiji vya Tingatinga, Ngereiyani, Sinya na Elerai ambapo ndiyo kijiji cha kwanza ambacho kimeguswa, hasa na eneo la Motooni. Ila kuna vijiji vimesahaulika na vina shida kubwa ya maji sana. Namwomba Mheshimiwa azingatie Wosiwosi ndiyo mwisho wa Wilaya tunapopakana na Kenya karibu na Ziwa Natron. Maji ya chini yana chumvi, lakini kuna maji mengi na mazuri kule Ngaresero upande wa Ngorongoro, naomba mradi wa maji safi kwenda Wosiwosi uangaliwe na maji hayo yapitite Magadini yaongezee yale yaliyotoka Mlima Kilai tuweze kupata maji toshelevu na masafi kwa wananchi wa mwisho wa wilaya yangu upande wa magharibi.

Pia niiombe Serikali na kuishauri kwamba katika maeneo ambayo maji yameletwa na mita zinafungwa bei ya maji ya mifugo iangaliwe tofauti na *unit* zinazochajiwa kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kwa sababu muda umeisha naomba *maintenance*, mashine zinafungwa za ma-*borehole*, maji yanaharibika ndani ya mwaka mmoja, mashine inakufa watu hawajui, wekeni wataalamu wa maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla sijamwita Mheshimiwa Shally Raymond, Waheshimiwa tunaenda wikiendi ambayo inaungana na huko mbele kidogo tu ni masuala ya Eid nafikiri, wiki inayokuja si ndiyo jamani?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Sasa ninachowashauri Waheshimiwa usije ukaondoka jumla, ukaunganisha na *Eid*, hupo mnanisoma lakini?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mnielewe, usije ukaondoka jumla. Ukiondoka jumla basi shauri yako, Spika wenu si mnamwelewa lakini? *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya, uwepo wepo kwanza.

Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Hhayuma ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kipekee namshukuru Mungu wote kuwa hapa na pia nakupongeza kwa kuwa wa matokeo *Result Oriented Speaker*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kuna kila sababu ya wote tulio hapa tumshukuru Mungu kuzaliwa Tanzania, nchi ambayo imezungukwa na vyanzo vya maji kila upande, tuna *Lake Victoria, Lake Nyasa, Lake Tanganyika*, kuna Bahari ya Hindi lakini katikati ya Tanzania yetu kuna mabwawa mengi ya maji, kuna maeneo mengi ya milima. Vyote hivyo ni vyanzo vya maji na sioni kwa nini Watanzania miaka nenda rudi tunalalamika hatuna maji hatuna maji. Niseme tu kwa kifupi maji tunayozungumzia hapa ni maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma kwa wale ambao wana umri wangu au zaidi watoto walikuwa wanazaliwa wakikuwa wana meno ya *brown*, lakini sasa hivi kila mtanzania akikuchekea ana meno meupe kwa sababu maji hayo yametibiwa na Serikali yetu iliona ni vyema basi kupunguza ile *fluoride* ili watu wote wanywe maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna shida, wataalam wetu wako wapi pamoja na vyanzo vyote hivyo vya maji? Jangwani kwenyewe, mfano ukienda Dubai maji yapo, sasa Egypt maji yapo, sisi urafiki wetu na nchi hizo uko wapi? Kwa nini

tulalamike maji, maji na tutenge Mifuko ya Maji kila wakati tuje, hapa tu-*ring fence* hela. Naiomba Wizara hii akiwemo Mheshimiwa Awesu, kijana anayependa kumtua mama ndoo kichwani na anayezungumza sana nchi hii haina ukame, tuone sasa tumefikia muafaka.

Mheshimiwa Spika, nianze kushukuru kwa ule Mradi wa Maji wa Mwangi, Same mpaka Korogwe ambao sasa ikifika Desemba kila mahali patakuwa na maji. Hata hivyo, niseme wazi, nimetokea Kilimanjaro ambako tuna mlima mzuri unaotiririsha maji, wengi wanapenda kuolewa Kilimanjaro au kuoia Kilimanjaro kwa ajili ya yale maji. Tatizo ni tambarare ya Kilimanjaro hatuna maji, ukienda Rundugai hakuna maji, tambarare yote hiyo. Tunaomba sasa Waziri wetu aje atembelee maeneo hayo ili pia naye atupe *solution*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunazo *success stories* za Mamlaka ya Maji Safi na Salama, wewe ni shahidi ulikuwepo hapa miaka hiyo, mkipitisha Sheria za Mamlaka za Maji, tumeona kuna ushindani na tumeona mafanikio katika miji, maji ni salama, miji mingi tu ikiwemo Dar es Salaam, Moshi, Musoma kule Mara. Huko kote nilikozungumza hao Wakurugenzi walipita Moshi wakajifunza, wakaenda sasa kupeleka huo utaalam kwingine na unakunywa yale maji yakitoka kwenye bomba moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba umefika wakati, baada ya kupunguza kiwango kikubwa cha yale magonjwa ya maji ikiwemo *cholera* (kipindupindu), sasa tuone kwamba ni haki na siyo ombi tena Wizara hii ya Maji ijue kwamba mwanamke anatakiwa afungue bomba la maji ndani ya nyumba yake na siyo kumtua tu ndoo na kuanza kubeba kwa mkono, hapana kila nyumba iwe na maji safi na salama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba Wizara hii inapata hela nyingi sana na pia ina wakandarasi wazuri na kelele zinapigwa, lakini wewe ni shahidi kila anayesimama hapa anasema maji hayatoshi. Nataka atakapokuja kuhitimisha Waziri aseme, tumefikia kiwango gani siyo hiyo 95 kwa miji

na 75 kwa vijiji tu, kwa sababu maji yote yanaanzia vijijini, hakuna maji yanayoanzia mjini kwa nini kule vijijini asiagize *RUWASA* kila kijiji yanapoanzia maji lile bomba litoe kwanza maji vijijini halafu ndiyo litoe mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hainiingiii akilini maji yanaanzia kwangu halafu wanaofaidi ni mjini, ina maana wale watu wa mjini ndiyo wanayajua maji na ijulikane kwamba maji hayana mbadala, huwezi kuchukua soda, ukachukua *K-Vant* au ukachukua kinywaji chochote ukafulia nguo wala kuoga, maji hayana mbadala kabisa, kiu ya maji ni ya maji na matumizi ya maji ni ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme pia Serikali itoe elimu; maji haya safi na salama yanatibiwa kwa hela nyingi sana, lakini maji hayo hayo utayakuta ndiyo yanayoosha magari, maji hayo hayo ndiyo yanafanya kazi za hovyzo zile inamwagilia bustani na kadhalika. Kwa nini tusipige hatua maji ya kunywa na kupika yawe ni tofauti na maji ya matumizi mengine yawe ni tofauti. Wengi mmetoka nje kuna mabomba mawili bomba moja ni la kunywa tu lingine ni ya kuoga na mambo mengine yale yale yanazunguka na yanafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, naona wasomi wetu pia hawachangamshi akili vizuri. Kuna lile Mindu *Dam* Morogoro, limekuweco siku nyingi na lime-*solve* matatizo mengi, lakini ukija katika hii barabara kabla hujafika Kongwa pale Kibaigwa maji yanakata mpaka yanavunja barabara, kwa nini kusiwepo na *Dam* lingine likakinga maji hayo yanayotoka huku Simanjiro yakatengeneza *Dam* linguine, ina maana wazee wale wa zamani walikuwa na akili kuliko sisi? Wasomi hawa walikuwepo, kwa nini maji yaharibu barabara tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Shally Raymond na hasa jinsi unavyoona maji mengi kabisa yakipita kule



Kongwa, lakini hakuna bwawa, mwaka hadi mwaka mengi sana, sana.

Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na, nitakuwa naenda sasa kwa Mbunge mwanamume, Mbunge mwanamke, namna hiyo.

Mheshimiwa Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mama Samia kwa kuendelea kumwamini Waziri Awesu na kwa kweli naomba nimpongeze sana Waziri Awesu, kama kijana ameitendea haki Wizara, pamoja na Katibu Mkuu na wasaidizi wake. Niseme wazi kwamba mimi binafsi kama Mbunge wa Geita ninakufurahia sana kazi zako na tungependu na Mawaziri wengine wawe kama yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona Waziri Awesu anavyohangaika na anavyopangua na sisi wengine tumepita huko kwenye ukandarasi kandarasi, tunaona jinsi ambavyo anajaribu kurekebisha hata huko kwenye Wizara yake, kwa sababu wizi mkubwa naamini kabisa unaanzia kutoka Wizarani, unateremka kule chini. Nitoe mfano mmoja, kulikuwa na huu mradi nasoma hapa wa miji 16, lakini sijui wametumia *formula* gani kwa kweli nawapongeza sana mpaka wametoa miji 29, hizo ndiyo akili tunazitaka, wasomi wawe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, tunaona hata sisi tunachimba, lakini kwenye visima bado, Waziri atafute akili nyingine kwa sababu ukiangalia, leo mimi kama Musukuma nikitaka kuchimba maji kisima changu hapa Dodoma kwa kutumia mitambo ile ile na utaaalam ule ule, haiwezi kuzidi milioni tisa au milioni 10, lakini ukienda kwenye kisima kinachochimbwa na Serikali milioni 37, inakuwaje huo utaaalam? Kwa nini tusiende kwenye utaratibu mwingine, tukaweza hiyo milioni 33 mpaka 35

ikachimba visima vinne mpaka vitano. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kuona namna ya kuwabana wataalam wake waweze kurekebisha ili tuweze kupata maji kwa wingi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuniwekea mradi kwenye Jimbo langu nimeona ameweka Vijiji vya Nkome, Senga, Nzera, Rwezera, Idosero, Sungusira na Kakubiro, namshukuru sana, lakini kauli yake ni nzuri sana, hivyo Waziri asinizingue *term* hii kwa sababu bahati nzuri mradi huu ulikuja kubuniwa na Profesa Mkumbo akiwa Katibu Mkuu na Katibu Mkuu wa sasa Sanga ndiye alikuja kufanya upembuzi yakinifu. Sasa Mheshimiwa Waziri hii ni mara ya pili ananiahidi akinizingua bajeti ijayo nitamzingua mara mbili.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tutakapomaliza suala hili la bajeti hata katikati hapa tukimbie akaone jinsi sisi Wanajimbo la Geita tulivyo wavumilivu, asilimia 92 ya Jimbo langu ni ziwa, lakini sisi tunaugua kichocho tunachota maji machafu, halafu maji yamevutwa yanaletwa mpaka Dodoma. Sasa hivi vitu nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, *term* hii asinizingue, tumekuwa wavumilivu vya kutosha, aone namna yoyote ile, baada tu ya bajeti hii, naomba tufungue mradi wa maji kwenye vijiji ambavyo ameniahidi. Nami namwahidi nitampa ushirikiano wa kutosha na hata akitaka utalam wakati wa kuandaa *BOQ* aniite ili maji yatoke kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aendelee na moyo huu. Nimekuwa Mbunge kwa awamu ya pili, hii bajeti Mawaziri huwa wanaugua tumbo, bajeti ya Wizara ya Maji, lakini naona leo mishale ni michache sana. Hii ni ishara nzuri, anapoitwa anaitika na anapoitika anaenda anatoa *action* ndiyo maana watu wanamshauri na kumwambia aboreshe pale alipovuruga.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ningomba Mheshimiwa Waziri, kama hatakuwa na nafasi kwa muda wa karibu kutembelea Jimbo langu, basi namwomba

Mheshimiwa Waziri kwa sababu ametembea na Wabunge wengi huko, aje na Jimboni kwangu angalau nitembee naye aone hivyo vijiji ambavyo...

**SPIKA:** Unamwomba Naibu au unamwomba Waziri?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, namwomba Naibu Waziri anaweza ....

**SPIKA:** Marufuku. (*Kicheko*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma hiyo ruhusa haijatolewa na Spika. (*Kicheko*)

Tunaendelea, Mheshimiwa Hamida Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Hhayauma.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Wake na timu yake ya wizara yake kwa namna ambavyo wanachapa kazi, lakini kwa namna ambavyo wamejiandaa na bajeti hii ya 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imegusa kila eneo na imezingatia changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge tulikua tunampelekea Mheshimiwa Waziri hoja mbalimbali. Kwa hiyo, nimshukuru sana lakini nimtakie kila kheri katika utekelezaji wa kipindi hiki cha mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mbalimbali ambayo yako ndani ya mpango huu wa bajeti ambayo itatekelezwa katika kipindi hiki. Naomba nishauri tunamuomba Waziri wa Fedha ajitahidi sana kutoa fedha kwa wizara hii iweze kutekeleza mipango yake ambayo himo katika mpango huu wa mwaka 2021/2022 kwasababu kuna mambo mazuri yanayokwenda kupunguza kero mbalimbali ya changamoto

hii ya maji, sasa utekelezaji huu utazingatia upatikanaji wa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha kutoa fedha kwa wakati kuhakikisha kwamba Wizara ya Maji inapata fedha na inakwenda kuteleza miradi hii ya maji. Niishukuru Serikali kwasababu Lindi tulikuwa na changamoto kubwa ya maji katika eneo Kata ya Rasibula Mtwero, lakini tayari tuko katika mpango huo wa utekelezaji kikubwa ni upatikanaji wa fedha tukatekeleze huu mradi wa maji kuhakikisha kwamba Mitwero, Kikwetu na Mchinga changamoto ya maji inaondoka.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo Lindi Manispaa ni uwepo wa gari maji taka, lakini nimshukuru sana Waziri lakini niishukuru Serikali kwamba tayari tupo katika mpango wa utekelezaji wa ununuzi wa gari la maji taka ili kuhakikisha kwamba Lindi Mjini tunakuwa na gari la maji taka na kufanya utekelezaji wa maji taka ili kuweka mji wetu kuwa salama na wananchi wetu waendeleo kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba uwepo wa maji duniani ni jambo kubwa ni jambo jema kwasababu mtu unaweza ukose umeme lakini usikose maji, unaweza ukose barabara lakini usikose maji, kwa hiyo, tunajua kwamba katika matumizi makubwa ya binadamu na shughuli za binadamu zinategemea sana uwepo wa maji. kwa hiyo, niitakia kila kheri Serikali yetu kuhakikisha kwamba inapata fedha za kutosha na kuweza kwenda kuteleza miradi ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na miradi ya maji ambayo ndugu zetu hawa la LUWASA walitekeleza kuweka viura katika mitaa, lakini ninajua kwamba Serikali ina nia njema ya kumtaka kila mwananchi aweze kuvuta laini ya maji nyumbani kwake ili afanye matumizi yake mwenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni kwamba maeneo ambayo yamepita *mainline* za maji inakuwa na

umbali mkubwa kiasi kwamba mwananchi anashindwa kugharamia kuvuta maji kutoka kwenye *connection* mpaka nyumbani kwake gharama zinakuwa kubwa mno, lakini ukiangalia mabomba ambayo yanatoa huduma na wenyewe *LWASA* nayenyewe yanakuwa na gharama kubwa ukilinganisha na bei ya madukani kwa hiyo tuangalie katika eneo hili ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanaweza kumudu kuvuta *line* za maji manyumbani kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kwenda kuhakikisha kwamba hasa Waziri na Naibu wake na timu yake katika utoawaji wa majisafi na salama ambayo tunapata huduma kutoka kwenye viwanda mbalimbali, maji mengine yanakua na *chloride* nyingi sana kiasi kwamba ukunywa yanakuwa chungu, kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Waziri aende akakaguwe ili kuangalia viwango vya ubora wa maji haya na kuweka hali za wananchi wetu ziendeele kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niendeele kuishukuru sana Serikali lakini niendeele kuwatakia kila kheri ili mipango yetu iliyomo katika bajeti hii tuweze kutekeleza kwa kipindi hiki cha 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamida Mohamed, Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma nilishakutaja utafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kwa kunipa nafasi awali ya yote nichukuwe nafasi hii kwa falsafa ile ile kwamba mnyonge mnyongeni lakini haki mpatieni. Niipongeze sana Wizara ya Maji kwa kazi nzuri inayofanyika, nikupongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa timu yako yote kwa kazi nzuri inayofanyika kwenye sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze kwa kazi ambayo kwa kweli mnaifanya kwa uvumilivu mkubwa mara zote nikikufuata wizarani unanipa nafasi ya kunisikiliza na tunajadiliana majadiliano ambayo kwa kweli yanaonyesha dira kwamba wana Hanang wanaenda kupata maji maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukuwe nafasi hii kushukuru kwa bajeti hii kuonyesha maeneo ambayo kwa kweli yalikuwa na matatizo ya maji muda mrefu, kwamba mmetutengea fedha za utafiti wa kupata vyanzo vya maji kijiji cha Mberu, Diloda, Bassodesh, Sasemwega, Mwanga, Lalaji, Wakhama, Masaqa, na ukichukua eneo la Mberu kipindi kirefu wananchi wanaamka saa tisa wanarudi nyumbani saa sita mchana shughuli zingine zote zinasimama wanafuata maji.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi sana mradi wa maji Gehandu eneo lile lilikuwa na changamoto ya muda mrefu tulijadiliana kwa kina na Mheshimiwa Waziri, kisima kimeshachimbwa usanifu umefanyika, lakini kwenye maandiko hapa naona unakwenda Gehandu Ming'enyi na Mugucha nilishaongea na wataalamu kwamba ule mradi kwasababu maji ni mengi tutanuwe kidogo uwende Milongori, uende kijiji cha Gidabwanja, uwende kwenye kitongoji cha Mwanina na kitongoji Marega kwasababu ni maeneo yako karibu na kwenye mteremko ni rahisi kupeleka maji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia pale Lalaji tumejenga shule ya sekondari ya kisasa sana na tuna kituo kizuri cha afya na mmeweka angalau mpango wa kupeleka maji na eneo lile halikuwa na maji muda mrefu sana eneo hili nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuangalia na pia tuna mpango huo wa kutanua mtandao wa maji kwenye Kata za Dirima, Lalaji, Mberu pamoja na Hideti. Ni kazi kumbwa naamini kwamba maeneo haya kidogo yatajaribu kupunguza changamoto ya maji ambayo tulikuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na juhudi zote zinazofanyika ninaomba Mheshimiwa Waziri eneo la usimamizi wa utekelezaji wa miradi ili eneo liangaliwe kwa ukaribu, kuna wakati nilishawahi kusema hapa Bungeni tafadhali wasongeelee karibu wataalamu wako ili angalau watekeleze miradi hii kwa ufanishi, jana baadhi ya Wabunge walichangia kwamba miradi mingi inatekelezwa kwa njia ya *force account*, ni wazo nzuri kama tuna rasilmali watu ya kutosha na naamini kwamba ni njia ambayo iko tuseme inathamani ya fedha kwa kazi kutekelezwa tuangalie je, kweli tunao huo uwezo je, hatucheleweshi miradi kwa kufuata hiyo njia lakini pia tuangalie tukiwatumia wakandarasi kwa njia ambazo zimeshauriwa, kwamba wakandarasi wengine inawezekana hawana mitaji tuangalie namna ya ku-*manage* ili tuhakikishe kwamba miradi inatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lakini pia jinsi tunavyozisimamia mamlaka zetu za maji sitaki sana niwe mlalamishi kwenye eneo hilo, lakini kwenye maandiko ya wizara umesema kwa kiwango kikubwa maendeleo ya jamii yoyote inategemea uwepo wa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa. Sasa ukiangalia mji wetu wa Kateshi pale umejengwa mradi wa maji wa bilioni 2.5, mradi ule hauleti tija yoyote kwasababu mradi umekamilika kwa maana na umekabidhiwa kwa mamlaka ya maji, lakini uendeshwaji wa Mamlaka ya Maji kwa kipindi kirefu hakuna *board*, ukifuatilia ni *board* ni kazi ya mtu mmoja,

Mheshimiwa Spika, naomba zile mamlaka zisimamiwe vizuri lakini pale ambapo hakuna ufanisi, zile mamlaka wakati mwingine zinatungezea gharama ukiangalia Dar es Salaam na Pwani inasimamiwa na *DAWASA* na gharama za maji ni nafuu. Huku kwetu *unit* inaenda mpaka 2,500 tuangalie eneo hili la mamlaka za maji zinaleta gharama kubwa kwa watumiaji wa mwisho. Ninaomba sana eneo hili lisimamiwe vizuri ili kuhakikisha kwamba tunapata tija ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kumaliza miradi ya maji jaribu kuongea ndani ya Serikali na watu wa Nishati ili pale

ambapo kisima kinaenda kuchimbwa nao umeme uende ili maji yanapopatikana maji yale yaweze kusambazwa kwa watu ili yaweze kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache ninashukuru ninaunga mkono hoja ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge wa Hanang, sasa Mheshimiwa Janejelly James, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Chege. Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, Ahsante kwa kunipa nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kusimama hapa nami kutoa mchango wangu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wake jinsi mnavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nilianza kazi maji miaka ya 1987 ukilinganisha na leo kweli Serikali imefanya kazi kwenye maji haikuwa hivi. Lakini kwasababu watu wengi wameshaongelea maji, matatizo ya maji na kila kitu mimi naomba nijikite kwenye miundombinu na mapato ya mamlaka zetu za maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajua kuna nyumba za Serikali nyingi, Tanzania nzima nyumba hizi kwenye *bill* za maji huwa hazilipwi kule kwenye nyumba za Serikali kwenye *bill* zile. Sasa tuanze kuzifungia *prepaid* nyumba hizi kuokoa mapato ya Mamalaka za Maji yanayopotea kumekuwa na uzoefu baadhi ya watumishi wa Serikali au baadhi ya viongozi wanahama wanaacha *bill* kwenye nyumba zile bila *bill* zile kulipwa sasa hii inakuwa ni hasara kwa Mamlalaka za Maji, wakati mwingine inakuwa ni hasara kwa mtu anayeingia kwenye nyumba ile kuambiwa alipe zile *bill* ambazo ziliachwa kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapitisha bajeti ya kila taasisi hapa ikiwa na gharama za ulipaji umeme na maji, lakini nadhani kwasababu ni Serikali yenyewe kwa wenyewe Wizara ya Maji mnaona aibu kwenda kukata maji kule



kwenye zile Taasisi na hawachukuli umuhimu wa kulipa bill za maji. Sasa niwashauri nishauri Wizara ya Maji anzeni kufunga *prepaid* mita kwenye taasisi za Serikali ili kuokoa yale mapato, tukishafunga hizo *prepaid* watalipa kama inavyotakiwa na ukiangalia hata kwenye ripoti ya CAG mapato mengine ya maji yanapotea pale taasisi za Serikali azilipi ipasavyo bill za maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hebu twende tukafunge *prepaid* kwenye hizo taasisi za Serikali walipe kwasababu bajeti ipo, Mheshimiwa Spika unaipitisha hapa na Wabunge tunapitisha ulipaji wa gharama zozote za uendeshaji wa Ofisi za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nijikite tena kwenye miundombinu, Wizara ya Maji au Mamlaka za Maji wanapokuwa wanafunga yale mabomba ya maji watayapitisha kwenye barabara, ujenzi wa barabara ni gharama kubwa nayo kwa Serikali. Sasa niombe tu Wizara hizi mbili wakati mnapoanza ujenzi wa miundombinu mkae pamoja mshauriane kwamba ni wapi miundombinu itapita ili tupunguze gharama za utengenezaji wa barabara zinazobomolewa wakati wa kupitisha mabomba ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna miundombinu ya haya mabomba kuchakaa na kumwaga maji hasa kwa jiji la Dar es Salaam hiyo ndiyo ilikuwa kubwa sana maji yanamwangika hovy. Niombe tu Wizara ya Maji, tumesema chuo cha Maji sasa havi kinatowa wale vijana hawajapata kuzunguka na kuangalia yale mabomba ambapo maji yanapotea wakafanye kazi ya kuwa wanatoa taarifa mabomba yale yanafanyiwa matengenezo ili maji yasipotee na watumiaji wa maji wasipate bill kubwa.

Mheshimiwa Spika, ninachojua Wizara ya Maji Mamlaka zenu za Maji ni maji salama na safi na maji taka, sasa mnapokua kutengeneza ufungaji wa maji basi fanyeni na ufungaji wa mabomba ya maji taka viende pamoja ili kuweza kufanya hivi vyote vitu viwe pamoja kupunguza

gharama na kuweka na kuweka sehemu za miji kuwa salama zaidi

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo niongeze tu kama mtumishi wa wafanyakazi kuna wakurugenzi wengi sasa hivi wanakaimu, mnawatumishi wengi wanakaimu, kukaimu nafasi huwa kunapunguza ushujaa au *confidence* ya kufanya kazi, basi niombe wale ambao mnaona wamefanya vizuri tunajua sheria inasema akaimu miezi sita, kama unaona ajatosheleza basi mtowe weka mwingine, kama unaona amestahili na amefanya vizuri basi watumishi hawa ambao ni ma-*engineers* wapeni hizo *confirmation* ili wawe na uhakika wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono ahsanteni sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Janejelly James, nilikutaja Mheshimiwa Jafary Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa, Sophia Hebron Mwakagenda.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukuwe nafasi hii kwanza kukushukuru wewe mwenyewe binafsi na niseme tu niendeleo kukutia moyo niseme uendeleo kufanya kazi ukiamini Wabunge wengi wako nyumba yako wala usiwe na hofu na yoyote yanayoendelea mtaani au kwenye mitandao ya kijamii, tuko nyuma yako na tunaelewa nini unafanya kwa wakati huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuchangia wizara hii nichukuwe nafasi kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji Wizara nzima pamoja na wadendaji wa RUWASA, mheshimiwa Waziri pongezi zote tunazokupa tunakupa kwasababu unatimu nzuri kwa maana ya wizara nzima yenyewe namna ilivyofanya kuanzia Katibu Mkuu na watumishi wote, lakini na *RUWASA* kwa utekelezaji mzuri wanaoufanya hasa pale unapokuwa unapokuwa umetoa maagizo.

Mheshimiwa Spika, nichukuwe nafasi hii kukushukuru binafsi kwa miradi mbalimbali ambayo umenisaidia, mradi wa Shilati niliwahi kusema ulikuwa na Zaidi ya miaka 15 hauna maji, umefanya Ziara ya siku moja ukatamka neno hivi ninavyozungumza tayari wananchi wale wana maji, nikuombe sasa kwa sehemu iliyosalia ulimalizie fedha walioomba milioni 300 ili angalau maji yaweze kusambaa ndani ya kata yote, lakini ikibidi na kata vijiji jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukuhishia hapo uliweza kunisaidia pia kwenye vijiji vingine kwa mfano kijiji cha Mwame, Kata ya Komuge, umenisaidia Nyarombo, umenisaidia Sudi, umenisaidia Nyehara na vijiji vingine, niendeleo kusema kwa namna unavyokwenda sisi vijana tunafarijika sana. Sasa niseme tu usife moyo, ninachoweza kushauri kwa miaka hii inayokwenda ili angalau tuendeleo sisi kukuunga mkono na kwenda na wewe sambamba nitakuwa na ushauri kwa maeneo matatu.

Mheshimiwa Spika, moja nikuombe sana Mheshimiwa Waziri jitahidi sana kuboresha RUWASA kwa maana wakala ya maji vijijini, na katika kuboresha huko wajengee uwezo ili waweze kupata watumishi wa kutosha kwa sababu nilikuwa najaribu kuangalia hotuba yako, kwenye fedha za maelendeleo peke yake maji vijijini Tanzania nzima umetenga Zaidi ya bilioni 360, kwa Mkoa wangu wa Mara umeniwekea Zaidi ya bilioni 21, tazama halmashauri peke yangu Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini yako umenipa Zaidi ya bilioni 5.3 ambayo inatakiwa itekelezwe kwa mwaka mmoja wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha yote hii kama kuna mtumishi mmoja tu ndani ya halmshauri kwa maana ndiyo *engineer* utaona namna gani fedha bilioni 35.3 inakwenda kusimamiwa na mtumishi mmoja ambaye inakwenda kusimamiwa na mtumishi mmoja ambaye unaweza kusema ni *engineer* wa wilaya. Kesho yake naamini, Mheshimiwa Waziri kama usipo wapa uwezo hawa watu wakuongeza watumishi utapita kwenye ziara yawezekana huyu asiwe na wakati mzuri. Niombe sana tuwajengee uwezo watu wa

*RUWASA* ili waweze kuongeza watumishi wa kutosha waweze kukusaidia kusimamia fedha hizi nyingi ambazo mmezitenga kwa ajili kwenye upande wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili nikuombe sana fedha hizi ambazo zimetengwa ziende kwa wakati kwasababu leo nitaondoka naenda kusema na ninasema kwa uwazi kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri kupitia Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan wilaya yangu imepata bilioni 5.3 kwa ajili ya miradi ya maji, ikienda kwa wakati na ikafika sahihi hautakuwa na ugomvi wowote na Mamlaka za usimamizi wa Maji kote hata hao watu wa *RUWASA*, kwasababu zitakuwa zinakwenda kwa wakati na wanatimiza yale ambayo wananchi wanahitaji haya mawili, Mheshimiwa Waziri ukiyasimamia vizuri ni Imani yangu, pongezi zote wanazozitoa ndani ya Bunge hili utaendelea kupata kwa miaka yote, kwasababu utawajengea uwezo miradi itakwenda kwa usahihi na kwa muda ambao umepangwa, niamini sana niendeleo kukuomba sana fedha hizi ambazo zimetenga, hasa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Maji fedha hizi mtusaidie sana ambazo zimetengwa kwenye bajeti hii tutengeneze historia kwa mara ya kwanza kwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maji kwenda yote kwa asilimia 100 hasa kwenye miradi ya maji hasa mkizingatia Rais Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ni mama ambaye kimsingi na yeye angetamani wamama wote ndani na vijiji vyote ambao kimsingi wanateseka sana na kero ya maji kwa miaka hii michache waweze kuondokana na kero hii ningeshukuru sana kama haya na hii bajeti tuliyoitenga itakwenda kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nizungumzie sana hii miji 28. Mheshimiwa Waziri nikupongeza sana mwanzoni ilikuwa inazungumzwa 16 lakini leo ndani ya Bunge hili unazungumzia miji 28. Nikuombe usipunguze hata mji mmoja, nenda nayo miji 28 kama ilivyosema kwa sababu tayari ndani ya Bunge

hili tunaondoka tukijua miji 28 inakwenda kupata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya jimbo langu nina vijiji 87 lakini vijiji vyenye maji ni 12 peke yake. Vijiji ambavyo vina miradi ni 23; vijiji 52 ndani ya jimbo langu havina mradi wowote wa maji safi na salama. Kwa hiyo, mradi huu wa miji 28 leo hii ukipitisha bomba lile linalotoka Rorya kwenda Tarime maana yake zaidi ya kata 11 zinakwenda kunufanika na mradi huu. Ndiyo mradi ambao sisi watu wa Rorya tunategemea kwa muda mfupi utakuwa umetatua kero kubwa na kwa eneo kubwa. *Coverage* ya mradi huu ni kubwa sana kuliko hata ukichimba kisima kimoja kimoja kwenye kila Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye huu mradi wa miji hii, naomba Waziri uipe kipaumbele sana hasa Rorya na Tarime. Watu wa Tarime hawana ziwa, ili wapate maji wanategemea maji ya Ziwa Victoria ambayo kimsingi yanatokea Rorya, Kijiji cha Nyamagaro. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ukisimamia hili ni imani yangu kwa muda mfupi ndani ya miji hii miradi ya maji itakuwa mizuri na utakuwa umetatua kero kwa asilimia kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Waziri amesema kuna watu wanapita kukagua miradi iliyotekelezewa na Serikali kwa miaka mitano iliyopita kwa kutumia wakandarasi na inawezekana wasiwe wakandarasi lakini fedha zilizokwenda kwa ajili ya miradi ya maji haikutumika sawasawa. Naomba Waziri atilie mkazo suala hili kwa sababu kama fedha zinaendelea kwenda kulekule ambako hakujatengenezwa mfumo mzuri wa kusimamia miradi hii na kuna fedha ilikwenda haikutumika inavyotakiwa maana yake hata hii inayopelekwa yawezekana isitumike vizuri. Naomba sana ukamilishe suala hili ili kila kitu kiende sawasawa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari na kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Maji anafanya kazi nzuri sana pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu yaani timu nzima wamejipanga vizuri. (*Makofi*)

Eneo la kuliangalia sana ni la gharama za miradi ya maji. Serikali mnatoa hela nyingi kwenda kwenye miradi ya maji lakini gharama ni kubwa. Kwa mfano, sisi hapa Dodoma ni visima vichache sana ni *borehole* ambayo inakwenda ziadi ya mita 150, vingi ni 150,120, 90, 80, 60 unapata maji ya kutosha. Sasa tuchukue hicho cha mita 150 ukiwa unachimba binafsi na ikichimba Serikali; ukiwa unachimba binafsi *drilling* ni *average* ya shilingi laki moja kwa mita ambayo kwa mita 150 ni kama milioni 15 yaani hiyo ndiyo kiwango cha juu cha kuchimba. Ukiweka mabomba, tenki na kadhalika, weka milioni 15 nyingine, hata kama unafunga *solar* kama milioni 30 hivi unapata chanzo na tenki lake na vitu vingine. Kisima hiki kinaweza kutoa huduma ya maji kwenye *average* ya kijiji chenye kaya hata 750, 1,000 na kadhalika. Sasa hiko chanzo cha milioni 30 sikiliza Serikali ifanye milioni 250, milioni 300 kitu kilekile, kwenye eneo la gharama za miradi ya maji mkaliangalie kipekee sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Chege anasema wamepewa shilingi bilioni 5 yaani ukimpa Mheshimiwa Simbachawene hapo shilingi bilioni 5 kwenye jimbo lake ukamruhusu yeye afanye anavyoona yaani harudi kwako tena, amemaliza lakini ukiwapa wataalam wako ataandika bomba kilometa kwa kilometa, *pump* ambazo hata hazihitajiki, inakuwa shida sana. Eneo la gharama za miradi ya maji ni la kuliangalia sana, ni namna gani utaweza kupata *realistic cost* za miradi ya maji na kutoweka mitandao ambayo haina tija kihivyo. Eneo hilo mkiliweza litakuwa limetuvusha kiasi kikubwa, kwa sababu Serikali mnapeleka fedha nyingi sana kwenye maji.

Tunaendelea na Mheshimwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nikuunge mkono kwenye eneo la Wizara kusimamia gharama za uchimbaji au gharama za miradi. Mheshimiwa Waziri na timu yako kama walivyosema wenzangu mnafanya kazi nzuri sana, lakini kule wilayani na mikoani lazima timu yenu pia ishuke ihakikishe inasimamia miradi yote ambayo Serikali imetoa fedha. Tuna mradi wa maji Masukuru, tulilalamika tukasema kwamba mradi ule ulifanywa chini ya kiwango. Nasisitiza kiwango ni kitu cha muhimu sana kwa sababu pesa ikitolewa ni lazima ifanye kazi sawasawa na thamani ya pesa iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya Wizara hii hasa walipoanzisha Jumuiya ya Maziwa kwa maana ya Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na mengineyo mmefanya kitu kizuri. Mkoa wa Mbeya una vyanzo vingi vya maji lakini tukitumia Ziwa hili la Nyasa kama ambavyo mmefanya Ziwa Victoria mtakuwa mmetatua tatizo kubwa sana la maji katika Mkoa mzima wa Mbeya wenye majimbo saba. Nafahamu ni fedha nyingi lakini tutakuwa tumetatua tatizo la muda mrefu la wananchi wetu kukosa maji sehemu za Nyanda Juu Kusini na maeneo ya Mbeya jambo ambalo sio sahihi kabisa kwa sababu tayari tunavyo vyanzo vya maji vingi lakini mpaka leo miaka 59 ya Uhuru hatujapata maji ya bomba maeneo mengi sana.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwa weledi mlio nao msimamie fedha za Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Spika kwamba Wizara hii mnapata fedha za misaada na mikopo tatizo ni mipango na viapaumbele ambavyo ni vyema tukavisimamia.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika Wilaya ya Rungwe kuna maeneo ambayo kama nilivyosema yana vyanzo vingi vya maji lakini ukienda maeneo kama ya Kimbira hukuti maji, ukienda sehemu za masoko au sehemu za Buliaga ambako ni mjini kabisa utakuta maji ni shida. Si hivyo tu watu wengine wanapata maji lakini bili za maji zinapokuja pia ni tatanishi. Kuna wakati unaenda kulalamika kwa nini bili yangu mimi nalipa hela nyingi wanakuambia tumekosea, sasa hii ni kwa

wale ambao wana uwezo wa kwenda kufuatilia. Kwa hiyo, tunaomba wanaosimamia mambo ya bili na utoaji wa maji maeneo kama hayo uwe wa vigezo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kusema hapa Bungeni kwamba kuna maeneo yanakuwa ni vyanzo vya maji, kwa mfano kwa kule Rungwe sehemu za Mpumbuli na Kasyeto, wao wana chanzo cha maji lakini cha kushangaza mabomba yanapita kama alivyosema Mheshimiwa Tunza wao hawana maji yanaenda sehemu za Ushirika na sehemu zingine wale wenye chanzo cha maji hawapati maji. Nafikiri hatuwatendei haki Mheshimiwa Waziri, najua labda ulikuwa hauna taarifa nakutaarifa sasa kwamba tunahitaji watu wa Kasyeto na wao wapate maji maana chanzo cha maji kinatoka kwao.

Mheshimiwa Spika, suala la ukosefu wa watendaji kazi, nimeona hapa katika hotuba ya Waziri wana upungufu wa wafanyakazi 1,500 na kuendelea. Tunahitaji watu hawa wapate watenda kazi ili kusudi iwe rahisi kuwafikia watumiaji wa maji. Tunaona wakati mwingine hata bili zinachelewa kusomwa kwa sababu anayesoma bill labda ni mmoja kwa eneo kubwa la sehemu husika. Kwa hiyo, mtakapokwenda kuomba watumishi iwape kipaumbele ili kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli maji ni uhai na ukimtua mama ndoo kichwani unakuwa umesaidia uchumi wa Taifa kuongezeka. Muda mwingi wanawake wanautumia kwenda kufuata maji mbali na kupoteza muda wa kutafuta pesa kwa ajili ya familia. Kwa hiyo, tunaamini Mheshimiwa Aweso na timu yako mkifanikiwa kusaidia kutatua tatizo la maji mtakuwa mmesaidia Tanzania kuwa ni nchi ya kati katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba niendeleo kuipongeza timu nzima ya Wizara ya Maji lakini pamoja pamoja na pongezi nyingi tunataka mama atuliwe ndoo kichwani maisha yaendeleo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*



**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda. Nilishakutaja Mheshimiwa Miraji Mtaturu na utafuatiwa na Mheshimiwa Ghati Chomete. Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu ya Wizara yetu ya Maji. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya lakini kwa bajeti nzuri walivyotuwasilishia hapa mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kabisa Mheshimiwa Aweso toka akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii ali-*perform* vizuri sana na ndiyo maana Mheshimiwa Rais akaamua kumpa Uwaziri kamili. Tuendeleo kupongeza na niwatie moyo vijana wengine waendeleo kuiga mfano wa aina ya Mawaziri kama akina Aweso, unafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba Ilani yetu ya Uchaguzi, ukurasa ule wa 7, Ibara ya 9(d)(i) inaeleza wazi kwamba katika miaka mitano tutaongeza nguvu katika upatikanaji wa maji vijijini na mijini. Katika taarifa yake aliyotusomea hapa kwa sasa kwa vijijini tumefikia asilimia 85 na kwa mijini tumefikia asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, kasi inatakiwa iendeleo kuongezeka katika kuwekeza Zaidi, najua kazi kubwa imefanyika. Mimi nina ushahidi katika jimbo langu au Wilaya yetu ya Ikungi tuliweza kupata jumla ya shilingi bilioni 3.7 katika mwaka uliopita na hata sasa tumeangalia pale wametutengea fedha naona safari hii kidogo wametuminya sana kwa wilaya nzima kwa majimbo yote mawili tumepata shilingi bilioni 1.7. Kwa shida ya maji tuliyonayo katika wilaya yetu, bado tuko chini sana, naamini kunahitajika juhudi kubwa kuongeza fedha kwa ajili ya kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Spika, nipongeze kwamba katika shilingi bilioni mbili 2 ambazo tulipata tumeweza kupata maji katika Vijiji vya Kipumbuiko, Kinku pamoja na Lihwa, hivi

ninavyoongea wananchi wanapata maji. Hata hivyo, ndiyo kama wanavyosema wenyewe kwamba tuendelee kula mtori nyama iko chini basi tunaendelea kuamini kwamba katika muda ujao tutaendelea kupata zaidi kwa sababu Vijiji vile vya Mkunguwakiendo, Sakamwau navyo vitapata fedha kwa ajili ya kuongeza uwezekano wa upatikanaji wa maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni usimamizi wa miradi hii. Mradi hii tunawekeza fedha nyingi lakini tunaenda kuacha kwenye Kamati za Maji ambazo hazina uwezo kabisa wa kusimamia miradi. Unaenda kuwekeza zaidi ya shilingi milioni 700 kwenye mradi wa maji unakuta hawana uwezo kwa sababu hawana ujuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na upungufu mkubwa wa hawa mainjinia au ma-*technician* wanaosimamia miradi hii. Pia kumekuwa na urasimu, unakuta huyohuyo injinia au *technician* anaagizwa aje asaidie wananchi mradi, unaende pale wanaomba hela ya mafuta na kadhalika, ucheleweshaji ni mkubwa sana katika maeneo hayo. Kwa hiyo, unakuta mpaka wamefika mradi umeharibika kabisa. Kwa hiyo, niombe sana kufanyike marekebisho katika eneo hili. Kama tumewekeza fedha tujiandae kutunza miradi ambayo inapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naamini sheria iliyoanzisha Kamati za Maji ni jambo zuri la ushirikishaji lakini hawana uwezo, miradi mingi inakufa. Tunaweza kusema kwamba wanajipange kutengeneza koki tu lakini hata mhasibu tu hawana kwa sababu pale hakuna mtu mwenye *professional* ya *accounts*. Kuna mtu wa kawaida tu mama mmoja amewekwa pale ana mradi anausimamia wa shilingi bilioni 1 hana uwezo wa kuendesha mradi ule. Kwa hiyo, ombi langu kama Taifa tuangalie upya suala la usimamizi wa miradi ya maji ambayo tunawekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la Ikungi sisi tulikuwa tumeomba tuwe na Mamlaka ya Maji Mjini. Tunaamini tukiwa na Mamlaka hiyo itatusaidia sisi kuwa na

uwezo wa upatikanaji wa fedha zingine. Mchakato ulianza miaka miwili iliyopita, Waziri utakapokuja hapa uniambie ni lini sasa tutapata Mamlaka ya Maji Mjini Ikungi ili isaidie kuongeza uwezo wa kupata fedha kwa ajili kuongeza miradi hii. Hii itasaidia sana kuongeza kasi ya usimamizi wa maji.

Mheshimiwa Spika, mfano kama Wilaya ya Ikungi leo tunapata maji asilimia 52 tu maana yake tuko chini hata lengo la Ilani, hii ilikuwa kiwango cha mwaka 2000 leo ndiyo sisi tunakitaja kile kieneo pale, asilimia 52 kwa wilaya nzima kwa majimbo yote mawili. Maana yake ni kwamba tuko nyumba sana hata miaka mitano ikiisha kama hatutafanya juhudi za makusudi hatuwezi kuvuka. Maji ni muhimu na hayana mbadala, huwezi kunywa kitu kingine badala ya maji.

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana Waziri anapokuja kuhitimisha atuambie kuhusu suala hili. Tuna tatizo la maji katika Vijiji vya Ntuntu, Tunataru, Mboho, Mwahu, Mahambe, Choda, Manjaru, Tumaini na Matongo, Unyang'anya. Haya maeneo yote watu wanashiriki kunywa maji pamoja na mifugo, hii ni hatari sana hata kwenye afya zao. Kwa sababu Mheshimiwa Rais ana mpango wa kutua akina mama ndoo kichwani niombe sana juhudi ziongezeke katika eneo hili ili tusaidiane kuwasaidia wananachi hawa waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili yake ni kujenga mabwawa kwa ajili ya unyweshaji wa mifugo. Sisi kule ni wafugaji naomba tuongeze uwezo wa kuchimba mabwawa ili angalau yapunguze tatizo la maji katika maeneo yetu. Mabwawa haya yakichimbwa yatasaidia sana kupunguza tatizo la maji kwa ajili ya kufulia au kunywesha mifugo ili maji machache yanayopatika yawe kwa ajili ya kunywa tu. Hii itasaidia sana kuondoa tatizo la maji katika maeneo yetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, vinginevyo nirudie tena kukushushukuru sana, Wizara inafanya kazi nzuri lakini tunaomba tuongeze bidii katika maeneo haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu nakushukuru sana. Katika mchango wa Mheshimwa Mtaturu ametaja vijiji kadhaa ambavyo havina maji lakini baadhi ya maeneo wanakunywa maji ya madwimbwi wakiwa pamoja na mifugo. Katika vijiji hivyo ametaja Kijiji kimoja kinaitwa Mahambe, hicho kijiji ndiyo anachotoka Mheshimiwa Tundu Lissu, amekuwa Mbunge miaka kumi kijiji chake mwenyewe hata chanzo cha maji hakuna. Ndiyo muelewe haya mambo haya, unajishughulisha na mambo ambayo ni *very superficial* yale ambayo ni *real politic* maana maji ndiyo siasa yenyewe hushughuliki nayo. Hawa ndugu zangu bwana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete atafuatiwa na Hasunga.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maji. Kwanza kabisa nampongeza Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri aliyoitoa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ninampongeza kwa juhudi anazoendelea kuzifanya katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuhakikisha inaboresha miradi ya maji nchi. Nampongeza sana Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, nampongeza Naibu Waziri wa Maji Maryprisca kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo. Wamefanya kazi nzuri katika Manispaa ya Musoma kwani hivi sasa wananchi wanapata maji mazuri ya bomba kwa kiwango cha kuridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, Mkoa wa Mara ambao una wilaya nyingi sasa maji ni pungufu sana.

Naomba mradi wa kutoka Ziwa Victoria, ule ambao unaanzia Wilaya ya Rorya uhakikishe Wilaya ile ya Rorya pamoja na vijiji vyake vinapata maji. Hivyo hivyo, Wilaya ya Tarime pamoja na Vijiji vya Nyamwaga mpaka Nyamongo wahakikishe vinapata maji. Niombe Serikali ihakikishe mradi huo wa kutoka Ziwa Victoria unawasaidia wananchi wa Wilaya ya Tarime kwa sababu mpaka sasa wanateseka sana hawana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Musoma Vijijini, Butiama pamoja na vijiji vyote vinavyozunguka zile wilaya havina maji. Bunda kuna miradi ya maji mpaka sasa miradi ile inasuasua, niombe Serikali kupitia Wizara hii ya Maji iangalie miradi yote iliyoko Bunda inatekelezeka. Mfano Mwibara kuna mradi wa maji ulipelekewa shilingi milioni 510 wa kutoka Namuhura kuelekea Kwibara lakini unasuasua. Kuna mradi wa kutoka Buramba, Kibara mpaka Kisorya mpaka sasa miradi ile inasuasau. Niombe Serikali yangu sikivu kupitia Wizara hii ya Maji ihakikishe miradi ile inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya Serengeti kuna mradi wa chujio la maji katika bwawa Manchira. Mradi ule ukitekelezeka unasaidia sana Mji wa Mugumu pamoja na vijiji vile vinavyozunguka pale ili wananchi wa maeneo yale waweze kuondokana na kero hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna sera ya kusema kwamba tunamtua mama ndoo kichwani, niwaombe sana Wizara ya Maji wahakikishe wanatua ndoo kichwani wale wanawake wa Mkoa wa Mara maana wanateseka sana. Akina mama wa Mkoa wa Mara ni wachapa kazi, wanaamka asubuhi kwenda kutafuta maji. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu sikivu uangalie kwa jicho la pili Mkoa wa Mara ili kusudi tuweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rorya, Kata ya Komuge kuna mradi wa maji. Mradi ule ulishatengewa shilingi bilioni 1.3 lakini sasa toka umetengewa fedha hiyo ni miaka mitano sasa umepelekewa shilingi milioni 300 tu. Niombe Serikali ihakikishe mradi ule unatekelezeka. Nasisitiza Serikali ihakikishe

inapeleka pesa hizi kwa wakati lakini ihakikishe pia inatekeleza miradi yote iliyowekwa katika Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete. Nilikuwa sijamfahamu, sasa sijui ni katika Waanchari au Wanyichoka au Mkurya au Mjaluuo au Mngorebe au Msweta au... *(Kicheko)*

Kuna makabila bwana. *(Kicheko)*

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mtimbaru. Mkurya Mtimbaru.

**SPIKA:** Naam.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mimi ni Mkurya Mtimbaru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ghati. Waheshimiwa huko inabidi ujjipange, uwe unajua masumbwi, vinginevyo utatolewa meno. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Japhet Hasunga, halafu atafuata Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia hii nafasi. Jambo la kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu kwa ujumla kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya katika kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu upatikanaji wa maji safi na salama ni moja ya vipaumbele; na ni kipaumbele cha nne kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa na mwelekeo ambao ametupatia kwa kweli unatupa matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, napenda kushauri; kwa muda mrefu tumekuwa tunapitisha bajeti kwa *figures* kubwa sana, lakini upatikanaji wa hizo fedha kiuhalisia umekuwa ni mdogo sana. Ukiangalia katika miaka yote ambayo tumepitisha bajeti, ukija kusoma uhalisia wa fedha ambazo zimepatikana kwenda kutekeleza miradi ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, hata sasa hivi nimepitia ripoti ya Kamati nikaangalia ni kiasi gani cha fedha ambazo zimepatikana? Utakuta wanasema fedha zilizopatikana mpaka sasa hivi na ambazo zimekwenda ni shilingi bilioni 376.4, sawa na asilimia 53.3. Kwa hiyo, hii inatia wasiwasi kidogo. Miradi tunaipanga vizuri, kazi tunazipanga vizuri, lakini fedha zisipokwenda inakuwa ni vigumu sana kuweza kutekeleza hiyo miradi ambayo tumekusudia.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Vwawa kuna mradi mkubwa pale Makao Makuu ya Vwawa ambao ulikuwa unatekelezwa, tulipata shilingi bilioni 1,500 kutoka kwenye chanzo cha Mantengu kwa ajili ya kusambaza maji katika Mji wa Vwawa. Mradi huu ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na alipokuja kuzindua akatoa tena fedha shilingi milioni 100 ili kuhakikisha kwamba usambazaji wa maji unaenea katika ule Mji wa Vwawa.

Mheshimiwa Spika, pia Waziri aliyekuwepo alitoa fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima vitatu virefu ili visaidie katika kuongeza mtandao wa upatikanaji wa maji. Cha kushangaza, mpaka leo bado kuna shida kubwa ya maji katika Mji wa Vwawa na yale maji hayajasambazwa, zile fedha sielewi zimefanya nini? Vile visima toka vimechimbwa zaidi ya miaka karibu mitatu bado havijaanza kufanya kazi kwa kisingizio kwamba hakuna fedha za kuunganisha ili viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi nzuri anayoifanya, basi hebu akalimulike hilo ili vile visima ambavyo vimeshatumia fedha,

basi vikafanye kazi ili wananchi waweze kunufaika na upatikanaji wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kusema, kuna mradi wa maji wa pale Kata ya lhanda, ni wa muda mrefu sana, umekuwa na shida, ambao ungesambazwa katika vijiji mbalimbali pale lhanda. Ulikuwa na matatizo. Mmetoa shilingi milioni 200, bado maji hayajapatikana. Tumechimba kisima, mpaka sasa hivi bado ni shida. Hebu naomba mkalifuatilie mlifanyie kazi ili wananchi wa Kata ya lhanda na vijiji vyote vinavyozunguka eneo lile viweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, kuna Kata ya lpunga pale, kuna Vijiji vya Mpera, lpunga yenyewe, vinahitaji maji. Vinaweza kupata maji kutoka kwenye mto kwa njia ya mserereko, lakini mpaka sasa hivi bado kumekuwa na changamoto ule mradi haujaweza kutekelezwa. Hiyo imekuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna Vijiji cha Msiya, Weruwan, Iganduka na maeneo mengine ya Isararo yanayozunguka. Pale tungeweza kupata maji ambayo yangetoka; kuna mradi mkubwa ambao uliwahi kusanifiwa miaka ya nyuma kutoka Rukururu – Mlangali ambao ulikuwa ni wa vijiji 14. Ule mradi kama ungetekelezwa, ungeenda katika vijiji vingi sana na hivyo wananchi wa kule wangeweza kupata maji kutoka katika hayo maeneo. Mpaka Vijiji vya Ibembo vingeweza kupata maji, lakini mpaka sasa hivi ule mradi haujatekelezwa na mpaka sasa hivi kuna upungufu mkubwa sana wa maji katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hata takwimu mnazozisema kwamba upatikanaji wa maji vijijini umefika asilimia 80, sijui labda kwenye majimbo ya wenzangu, kwenye jimbo langu sidhani kwa sababu vijiji vingi bado havina maji safi na salama. Kwa hiyo, hizo takwimu labda pengine zina-*fit* zaidi kwenye maeneo mengine kuliko katika Jimbo la Vwawa.



Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa maji ambao ulitekelezwa kutoka kwenye Kijiji cha Idiwiri kwenda Iyura na ukaenda katika vijiji saba. Sasa kitu cha ajabu ni kwamba ule mradi yale maji yanatoka kwenye Kata ya Idiwiri, kwenye Kijiji chenyewe cha Idiwiri ambapo maji yanatoka hakikupata maji; Kijiji cha Iromba ambako maji yanatoka hakijapata maji; Vijiji vya Mafumba havina maji; vijiji vingine maji yanatoka pale yanaelekea kwenye vijiji vingine.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wa maeneo yale wamekuwa na malalamiko makubwa kwamba wanatakiwa kutunza vyanzo vya maji, wanatakiwa kuhakikisha maji yanakuwepo, lakini wao wenyewe hawajapatiwa maji. Namuomba Mheshimiwa Waziri, hebu lipe uzito, liangalie hilo eneo ili nao waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, kuna Kata ya Nanyara; kuna Vijiji vya Songwe, Songwe - Rusungu, Namronga na maeneo mengine. Kuna mradi wa maji wa mwaka 1972 ambao kwa kweli mabomba yamechakaa sana, umekuwa haufanyi kazi. Mpaka sasa hivi kumekuwa na shida sasa ya upatikanaji wa maji na kwa sababu wakati ule wana-*design* ule mradi wananchi walikuwa ni wachache, sasa hivi wamekuwa wengi, bado hakuna upatikanaji wa maji wa kuweza kutosha katika lile eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba katika miradi ambayo wanaenda kuitekeleza kwenye vijiji, basi wakaliangalie hilo eneo ili vijiji vile viweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kuna Kijiji cha Ihoa, Welutuu na Ruvumbila, naomba sana tukaviangalie.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Hii siri ya maji ni mtihani mkubwa. Mimi nilitegemea shida ya maji ni Dodoma tu, lakini nashangaa mpaka Tukuyu wanalalamika, mpaka Mbeya Vijijini kwenye mvua nyingi. Kwa hiyo, maji ni mtihani kwa kweli.

Mheshimiwa Agnes Hokororo kama yupo, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani.

Mheshimiwa Hokororo tafadhali.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Aweso na nina matumaini makubwa kwamba atafanya vizuri kwa sababu naye hakutoka Oysterbay wala Masaki na anajua taabu na shida za mama zake kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mashaka pia na Naibu wake, Mheshimiwa Eng. Maryprisca, kwa sababu ni mama. Kwa hiyo, hata Mheshimiwa Rais anapohimiza suala la kumtua mama ndoo, yeye ni mama. Kwa hiyo, wote kwa kweli tuna matumaini na ninyi na tunawaomba kwa Mwenyezi Mungu mwendelee kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia kwenye bajeti hii nimeona kuna miradi 84 na hiyo ni usanifu, ukarabati, uchimbaji wa visima katika Mkoa wa Mtwara, lakini naomba nijielekeze kwenye utekelezaji wa bajeti iliyopita 2020/2021. Kama ambavyo imeonekana kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, utekelezaji wake ni asilimia 54 tu. Mkoa wa Mtwara kulipangwa shilingi bilioni 21 na zikapatikana ama zilizotumika ni shilingi bilioni sita tu, sawa na asilimia 39. Kwa

hiyo, hapa changamoto kubwa ni suala la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwenye hili eneo. Kwa sababu kwa sasa Mfuko wa Maji ambao ndiyo Wabunge wote wanategemea na kila mmoja hapa kwenye eneo lake ana changamoto ya maji na fedha zile ambazo zinapelekwa ni shilingi 50/= ya mafuta, mimi naamini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunaona bado kuna kadhia kubwa ya uhitaji wa maji, pengine mfuko huu uongezewe uwezo. Kama kwa bajeti ya mwaka 2020 iliweza kutekelezeka kwa asilimia 54, hatutegemei miujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni 680 lakini kwa utaratibu huo huo kama fedha haitakwenda yote hatutegemei Mheshimiwa Aweso na wenzake kwamba watafanya miujiza kwa sababu hiyo iko kwenye imani zetu za kidini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uwekezaji mdogo katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu unachangiwa na ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, nadhani iko haja ya kuangalia vyanzo vingine ili sasa hili suala la maji litekelezeke kwa kipindi kifupi na Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kuongea habari nyingine.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze katika Mkoa wa Mtwara. Kama ambavyo nimetangulia kusema, kwamba upatikanaji wa fedha pia ndiyo ilikuwa changamoto, sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara, nikisema hapa habari ya kuokota, dada yangu, Mheshimiwa Tunza amesema, hamtuelewi. Maana yake, kwenye vile vyanzo vitatu vya chini ya ardhi na juu ya ardhi, sisi tunatumia kwa kiasi kikubwa maji yale mvua inaponyesha, iwe ni nyumba ya nyasi yale maji meusi au yale yanayotiririka juu ya ardhi, tunayakinga kwenye mashimo halafu wenye uwezo wanaweka shabu, tusio na uwezo tunayanywa vilevile. Ndiyo maana ya maji ya kuokota kaka yangu, Mheshimiwa Waziri Aweso. Hiyo inatusababisha kutumia pia fedha nyingi kwenye matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana, hii changamoto ya maji ya Mkoa wa Mtwara kwenye Wilaya za Tandahimba, Newala, Mtwara Vijijini, Masasi, Nanyumbu ndiyo mara 200, haitaweza kuondoka kama Serikali haitakuwa na dhamira ya dhati ya kuanza kutekeleza Mradi wa Maji wa Mto Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona huku kwenye bajeti iko ile shilingi bilioni sita, Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara Mikindani na vijiji vya jirani, vijiji 73 vya Jimbo la Nanyamba au Mtwara Vijijini, lakini bado kule Nanyumbu, Newala, Tandahimba, Masasi, Majimbo ya Lulindi na Ndanda kuna adha kubwa. Kila siku mama analazimika kwenda mtoni. Kama mto utakuwa umekauka, basi tufukue kisima tuweze kuchota maji. Hata ukiona hata rangi ya yale maji hutakunywa. Hutaweza, nina uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaishauri Serikali ianze kutekeleza Mradi wa Maji wa Mto Ruvuma. Wenzetu tunasikia; maji ya Ziwa Victoria, maji sijui ya nini, sisi chanzo cha uhakika tulichokuwa nacho ni Mto Ruvuma. Pamoja kwamba kuna mto wa pili ambao haukaushi maji, Mto Lukuledi, lakini bado pia huo utasaidia kwenye maeneo machache. Ili tunufaike wananchi wote wa Mkoa wa Mtwara, ni muhimu sana kuona mradi wa chanzo cha Mto Ruvuma unatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara una vijiji 809. Kwa sasa vijiji 450 ndiyo vinapata maji na siyo saa zote, yaani 450 ndiyo vinapata maji. Ndiyo hayo sasa ya mdundiko, ama ya kuchota angalau. Vijiji 359 havipati maji. Kwa hiyo, wakati llani inasema itakapofika 2025 vijijini ni asilimia 85, sisi hiyo ni ndoto, kwa sababu kwa sasa kwa upande wa vijijini ni asilimia hiyo ambayo tunasema ndiyo ya wataalam, inawezekana 58 au 59, hatuwezi tukafanya maajabu kwenye hii miaka mitano tukafika kwenye hiyo asilimia 85.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ukiniuliza kipaumbele cha kwanza kwa Mkoa wa Mtwara, ni maji; cha pili, changamoto ni maji; cha tatu changamoto ni maji.

Ttunaiomba sana Serikali yetu sikivu ya Chama cha Mapinduzi ijielekeze kwenye hilo eneo ili nasi tutuliwe ndoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes Hokororo.

Bado tuko Mtwara Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii kukushukuru kwanza wewe. Vile vile nisiwe mchoyo wa shukrani, nami nawashukuru sana Waziri wa Maji, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wa Maji pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa *RUWASA*. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana. Ni imani yangu kwa michango hii ya Wabunge, bajeti yenu itapitishwa bila mihemko yoyote kwa sababu mnafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara ya Fedha, tunakaa hapa Wabunge kwa sababu ni ukweli wa dhahiri kwamba tatizo la maji kwenye nchi yetu bado ni kubwa. Sasa ni vyema Wizara ya Fedha, hii bajeti ambayo Wabunge tunakaa kuwasifia Mawaziri wanafanya kazi kubwa, wanatembelea miradi, wanajua changamoto, kama hawakupewa fedha hizi sifa zote tunazowapa hazitakuwa na tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuchangia pale alipochangia dada yangu, Mheshimiwa Agnes Hokororo. Sisi watu wa Mtwara ukiangalia kwenye bajeti tunao mradi ule wa miji 28, nasi tupo kwenye mradi wa Makonde. Napata mashaka makubwa; mimi na Mheshimiwa Waziri tumeingia Bungeni pamoja mwaka 2015, mradi huu wa miji 28 mnaousema tumeanza kuimba nao mwaka 2015. Miaka mitano tumemaliza tunazungumzia habari ya mradi wa miji 28, fedha zinatoka India. Huu mradi hebu mtuambie ukweli wake. Maana tusije tukawa tunaimba ngonjera ambayo

tunajitekenya wenyewe, tunacheka wenyewe. Miaka mitano mradi huu wa miji 28, kila tunapokuja mnauzungumzia. Ukweli wa mradi huu uko wapi? Tusiwape matumaini wananchi.

Mheshimiwa Spika, 2017, Rais wa sasa, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan alikuja Tandahimba, akazungumzia mradi huu wa miji hii na akasema tunapata fedha kutoka *Exim Bank* ya India. Leo tunaingia miaka sita tunazungumza *story* ile ile, Watanzania wanataka maji.

Mheshimiwa Spika, Mtwara dada yangu amewaambia, tunao Mto Ruvuma. Jimbo langu mimi la Tandahimba kutoka Tandahimba Mjini kwenda Mto Ruvuma hazizidi kilometa 16, lakini watu wake hawana maji. Kama mmeweza kutoa maji Ziwa Victoria mkayatembeza zaidi ya kilometa 400 na uchafu, yanakwenda mpaka Tabora, yanakuja mpaka Dodoma, mnashindwaje kutengeneza mpango Mto Ruvuma ukatoa maji ukapeleka kilometa 16, 60, 70 hadi 100 Mkoa wa Mtwara tukawa tumemaliza kabisa tatizo la maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimegundua ninyi mna dhamira njema, lakini kule chini, alipokuja *DG* wa *RUWASA* Tandahimba, tumekwenda kwenye chanzo cha maji Mauta, kulikuwa na Mradi wa Maji Mkupete, maji yalikuwa hayatoki. Amekuja, baada ya siku tatu watu wale wameanza kupata maji. Kumbe hapa juu ninyi mko vizuri sana, hebu mulikeni kule chini. Tuleteeni wataalam ambao wataleta matokeo ya maji kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto ni ndogo, wataalam mliowaleta chini wengine wamezeeka, wapumzike. Lete damu mpya msogeze gurudumu watu wapate maji. Kama watu walikuwa wanakosa maji muda wote, *DG* kaja siku ya tatu maji yanatoka mpaka Maheha. Kumbe wakati mwingine changamoto ni watendaji hawa.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamechangia hapa kwamba watendaji wa *RUWASA* ni wachache. Kama ni wachache mwone namna ya kuajiri watu wengine kwa

sababu tunapozungumzia Jimbo kama Tandahimba lenye vijiji 147 na vitongoji 60 ukawa na wafanyakazi wanne, sidhani kama kukitokea changamoto Mkwiti kwenye mradi mkubwa wa maji wanaweza kuukimbilia kwa haraka kule.

Mheshimiwa Spika, pia watu hawa wa *RUWASA* hawana vitendea kazi, na lenyewe mliangalie. Sisi tunaokaa Wilaya ambazo zenyewe ziko *scattered*, yaani ukitoka Tandahimba unakwenda Jimbo la Mheshimiwa Nape, kilometa 61, una wafanyakazi watatu, wanajigawaje? Hawana pikipiki, hawana magari, hata ikitokea changamoto hawa watu wanakwenda kutatua tatizo Mkwiti kwa namna gani?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana, kwenye Mradi wangu wa Mkwiti kama mkiangalia kwenye maandiko yenu, ule mradi ulipaswa kukamilika mwaka 2018, lakini nimesoma kwenye bajeti bado fedha mliyotenga kwenye Mradi wa Maji wa Mkwiti haiendi kutatua tatizo la maji kwenye Kata zile ambazo kipindi cha mwezi Juni mwananchi ananunua maji shilingi 1,500 kwa ndoo. Ikifika mwezi Juni tu hapo, watu wa Mwangombya, Mkwiti, Likolombe, Namindondi, Ngunja, Mmeda, Litehu, wanapata shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna dhamira ya dhati ya kuona kwamba tunataka tukamilishe tatizo la maji, basi wekeni fedha inayojitosheleza. Kama mradi ulipaswa kukamilika 2018 haukukamilika, leo malizieni fedha ili watu wale wawe wamepata maji na tumtoe mzigo mama ambaye anakunywa maji ambayo siyo salama.

Mheshimiwa Spika, nikwambie tu, sisi wanadamu bahati tuliyokuwa nayo, katika matumbo yetu kuna zahanati. Maana maji wanayokunywa watu wetu, usiku wanakunywa mbweha, asubuhi wanakunywa binadamu. Mungu ametujalia kuwa na zahanati tu, tunajitibu wenyewe. Vinginevyo, matatizo yangekuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani.

Nilishakutaja Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

Mheshimiwa Yustina, kama hayupo Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameonyesha na wanaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze alipoanzia Mheshimiwa Katani, mimi ni sehemu ya majimbo ambayo yanatarajia kufaidika na Mradi wa Miji 28 na mji mmoja wa Zanzibar. Kwanza niseme, kama alivyosema kwamba tumekuwa kwenye matumaini tangu mwaka 2015 na nipongeze juhudi ambazo zimefanywa na Serikali, lakini nipongeze zaidi kwa taarifa ambazo ametupatia juzi Mheshimiwa Waziri kwamba sasa wamefikia sehemu, wamekamilisha taratibu zote za manunuzi na wanasubiri sasa fedha hizo ziweze kufika na waweze kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo tunasisitiza hapa, tuliahidiwa kwamba mradi huu utaanza kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha. Sasa juhudi hizo Serikali ndizo wajielekeze nazo kama unaanza mwezi huu, kama unaanza mwezi ujao tunataka kuona wakandarasi hawa wakiwepo *site*, wakiwepo kwenye maeneo husika ili tupunguze maneno ya kuzungumza kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kila mkutano unaokwenda unazungumzia pesa za miji 28 na kwa bahati mbaya sana tumeshawapa matumaini wananchi kiasi kwamba



wanapomwona mtu anachimba kisima wanashangaa kwa nini unachimba kisima wakati tunatarajia maji kutoka Ziwa Victoria. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri tumemwelewa sana, tuna imani kubwa naye, lakini jambo la msingi mradi huu uanze katika mwaka huu wa fedha kama ambavyo amekuwa akituahidi na ambavyo alituahidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la pili, mwaka jana tulikuwa, tulipewa pesa kwenye bajeti bilioni 1.1 za maendeleo. Mpaka tunaingia kwenye bajeti hii pesa hizo za maendeleo zilikuwa hazijafika. Mwaka huu pia ametoa fedha bilioni 1.1 za maendeleo, napata wasiwasi sasa kama tunatenga haziendi, tunatenga haziendi, usambazaji wa maji kwenye mji wangu unakuwa hauendi kwa kasi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nimsaidie Mheshimiwa Waziri, *GEUWASA* wapo pale Geita Mjini, wakati huo huo kuna *RUWASA*. Kwa hiyo matokeo yake kwenye kata moja kuna *GEUWASA*, kuna *RUWASA*. Unakuta mtaa huu *GEUWASA* wanapeleka bomba, mtaa huo huo na *RUWASA* anachimba kisima. Kwenye maeneo, Mitaa ya Manga kuna *RUWASA* wanachimba visima, *GEUWASA* amefanya *survey* ya kupeleka bomba.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri, kama *GEUWASA* Waziri anawaamini na wanafanya kazi vizuri sana, wametoka kwenye bilioni 50 wamefanya mradi kwa bilioni nne. Waziri awape kazi ya Geita Mjini wasimamie wao, hii *confusion* ya *RUWASA*, *GEUWASA* atashindwa ku-*coordinate* kwa sababu atakuta hizi pesa ndogo anazozipeleka zina *authorities* mbili za kusimamia. Kwenye kata moja una *RUWASA*, kwenye kata moja una *GEUWASA* sioni inawezekanaje kumaliza tatizo la maji kwa sababu kuna watu wawili wa kuuliza maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri awape *GEUWASA* wasimamie au awaondoe *GEUWASA* awalete *RUWASA* wafanye kazi pale Geita Mjini. Hii itamsaidia Waziri kuweza kujua *value for money* ya kazi anayoifanya, lakini kupunguza maswali. Natamani sana kuona *GEUWASA* wakipewa kazi ile kwa sababu jana amesifiwa mtu wa

*DAWASA* na mimi namsifia kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini wale *GEUWASA* katika kila pesa wanayofanya *saving* wamekuwa wakiongeza usambazaji wa maji pale mjini. Kila *saving* wanayoifanya wanaongeza usambazaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Kasamwa, ukienda kwenye kata za pale mjini zina uhaba mkubwa sana wa maji, wanaojua vizuri matatizo ya maji ni *GEUWASA*. Sasa kwenye hiyo hiyo unapeleka *RUWASA* kwenye kata hiyo hiyo unapeleka *GEUWASA*, utajikuta pesa ndogo za Serikali zinashindwa kutoa matunda yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, pale Geita Mjini ni kilometa kama tano kutoka ziwani, mradi mkubwa pekee wa maji ni Mradi wa *GGM* walioujenga kwa *CSR*. Kwa hiyo tuna visima visima vingi, usambazaji wa maji kwenye Mji wa Geita katika taasisi nyingi umekuwa ni mdogo sana. Kwenye Kata za Mtakuja tuna vituo viwili vya afya havina maji. Kwenye Kata ya Mtakuja kuna shule za sekondari mbili hazina maji, tunasomba maji kwa kutumia malori.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati tunasubiri huu mradi wa fedha za India naomba sana pesa za maendeleo za kusambaza maji kwenye kata hizi ziweze kutolewa ili hizi kata na Taasisi za Serikali ziache kupeleka maji kwa kutumia malori. Wanaposomba maji kwa kutumia malori inabidi wanafunzi waanze kutumia maji kwa mgao, lita tano kwa masaa 24. Mheshimiwa Waziri unajua wanahitaji kuoga, wanahitaji kufua, kwa hiyo, tunawafanya wanafunzi wetu kuwa wachafu, lakini tunawafanya pia kushindwa kuwasimamia.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Waziri, naamini kwamba Mfuko wa Maji kama alivyosema mchangiaji aliyetangulia ni mdogo na tumepiga kelele sana kwenye Bunge hili ili kuweza kuuongezea pesa, lakini hizi pesa zilizopo tuzigawe vizuri, tuzisimamie vizuri, kwa sababu zina uwezo wa kuleta matokeo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine Kanyasu. Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Pili, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Maji, kwa namna wanavyopambana kuona namna gani wanatatua changamoto ya maji kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu umuhimu wa maji kwenye jamii zetu. Tunafahamu kwamba kama tunataka jamii au nchi yenye watu wenye afya nzuri tunahitaji maji safi. Kama tunahitaji kuinua kiwango cha elimu wanafunzi wote wa kike na wakiume waweze kwenda kuhudhuria masomo vizuri tunahitaji maji.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa tunahitaji kuinua kiwango cha uchumi wa nchi yetu, kuzuia magonjwa yasiwasumbue watu na tukapoteza fedha nyingi kwenye kutibu magonjwa, tunahitaji maji safi.

Mheshimiwa Spika, nafahamu juhudi kubwa ambazo Serikali inazifanya kutatua changamoto ya maji na zipo takwimu zinazoonyesha kiwango gani cha maji kinapatikana sasa hivi, lakini kwa uhalisia zaidi ya asilimia 50 bado watu hawana *access* ya maji safi na salama. Ushauri wangu ni nini? Serikali inabidi sasa itoe kipaumbele kikubwa kwenye Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, *research* zinaonyesha kwamba kutatua changamoto ya maji, kuleta maji safi na salama si kwamba tu muhimu kwa afya, lakini pia tunaona zitanyanyua kiwango cha uchumi kama nilivyosema hapo mwanzo. Pia itasabisha kuwe na Taifa la watu wenye furaha kwa ajili tunapata maji safi, watu wanaoga vizuri kabla ya kwenda kazini asubuhi, kwa hiyo maji ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, *statistics* zinasema tuki-*invest* shilingi moja kwenye Sekta ya Maji pamoja na Usafi wa Mazingira inaweza kuletea ongezeko la uchumi kwa shilingi 12. *Investment* ya shilingi moja inaweza kuletea pato la Taifa ongezeko la shilingi 12. Kwa hiyo naomba tujitajidi kuongeza *investment* kwenye sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni huu; kama tulivyofanya *investment* kubwa kwenye *standard gauge*, tulivyofanya *investment* kubwa kwenye umeme, tunaona tunajenga bwawa la umeme, kwa nini sasa tusiwe na mradi mkubwa wa kimkakati nchi hii ili kutatua tatizo la Maji Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tusiwe na fedha za kufanya hivyo, lakini tunaweza tukakopa fedha nje ya nchi au ndani ya nchi kwenye vyanzo mbalimbali kama vile *Government Bond* tuka-*invest* kwenye changamoto ya maji ili tuweze kutatua tatizo la maji kwa sasa hivi na hata miaka hamsini ijayo. Halafu tutaendelea kulipa deni hilo pole pole lakini tukiwa na uhakika kwamba changamoto ya maji imekwisha kabisa kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mradi mkubwa ambao uta-*identify* tatizo la maji lipo kiasi gani nchi nzima. Mradi mkubwa ambao uta-*identify* vyanzo vya maji, tumetajiwa Ziwa Victoria, Tanganyika na Maziwa mengine, Mito na kila mahali. Mradi ambao utasambaza maji nchi nzima, tuji-*commit* sehemu hii tutaendelea kulipa deni lakini tukiwa tunajua kabisa changamoto ya maji imeisha kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi Jimboni kwangu Korogwe. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kaka yangu Aweso kwa *commitment* yake kubwa kuhakikisha anatusaidia kutatua changamoto ya maji pale Korogwe. Korogwe ina changamoto moja, changamoto iliyokuwepo Korogwe kwanza kuna mradi unaoitwa *HTM*, huu ni mradi wa miaka mingi, mradi huu unasabisha wakati wowote tunapoomba fedha kwa ajili ya maendeleo ya maji, kutatua changamoto ya maji, tunaambiwa mna Mradi wa *HTM*. Kwa hiyo,

tunaomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe anatuleta maji kwenye Mji wa Korogwe bila kuangalia hii *HTM. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Waziri kwa sababu kwenye bajeti hii angalau tumepewa hela kidogo, lakini tunaona itatutua angalau changamoto ya maji Korogwe. Nilimwomba milioni 700 kwa ajili ya Kata ya Bagamoyo lakini kwa mwanzo ameniletea milioni 200. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutumaliza hizo milioni zilizobaki ili kuweza kutatua changamoto ya Maji Korogwe. Tuna imani sana na Mheshimiwa Waziri, tunamwamini na tunajua atatatua changamoto ya maji Korogwe na Tanzania nzima. Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea. Mheshimiwa Francis Isack Mtega, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. FRANCIS I. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya uhai wa wananchi, suala la maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukomo wa bajeti nafahamu kwamba ipo miradi katika jimbo langu ambayo imeachwa kutokana na ukomo, ambayo ni miradi muhimu sana inayohudumia wananchi wengi, takribani wananchi 10,000,000. Mheshimiwa Waziri mfano wa miradi hiyo, mfano Mradi wa Mirade karibu milioni 500, Mradi wa Mbigigi milioni karibu 520, Mradi wa Ndala karibu milioni 350. Miradi hii yote imeachwa kutokana na ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba upo mpango wa Wizara hii kuongezwa fedha hasa kutokana na agizo la Mheshimiwa Rais kwamba Wizara hii anaingalia kwa makini sana na akamwambia Waziri akizingua na yeye atamzingua. Sasa pale pesa zitakapoongezwa, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri miradi hii irudi kwenye bajeti. Kwa sababu

ni miradi muhimu, wengine naona wanaongelea miradi ya miji yao kupata maji, lakini sisi wa vijijini na Wilaya yangu ya Mkalama ni wilaya mpya, haina vitendea kazi na shida ya maji ni kubwa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakapoongezwa pesa, miradi hii irudi ili wananchi hawa wa Mirade, Ndala na Mbigigi katika Wilaya ya Mkalama nao waweze ku-enjoy maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, pia Meneja wangu wa *RUWASA* pale Mkalama anafanya kazi nzuri sana *Engineer* Mark, ni msikivu, anafuatilia lakini tatizo kubwa hatuna vitendea kazi. Wilaya yetu iligawanywa kutoka Iramba na vitendea kazi vingi vilibaki kwenye Wilaya Mama. Hatuna gari, nimwombe Waziri katika bajeti zake atupatie Mkalama gari ili *Engineer* huyu na watu wake na Ofisi yake waweze kufanya kazi nzuri zaidi ya wanayoifanya sasa ya kuhudumia Wilaya yetu ya Mkalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea jimbo langu sasa nishauri pia Wizara hii kitaifa. Kwa kushirikiana Wizara ya Maji na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wanaweza kutengeneza sera ambayo itawafanya Watanzania wawe na tabia ya kuvuna maji ya mvua. Unajua kila Mtanzania mwenye nyumba ya bati tayari ana chanzo cha maji, kinachobaki ni *storage* tu. Kwa hivyo kama tutatengeneza sera vizuri ya kuwashawishi Watanzania, wakaweka umuhimu kwenye ramani zao za nyumba wanapojenga kuwe kuna *tank* angalau la lita 50,000 za maji.

Mheshimiwa Spika, ukiwa na lita 50,000 za maji una mapipa zaidi kama 250 hivi. Kwa mwananchi wa Tanzania akiwa anatumia pipa moja lenye ndoo 12 anaweza akatumia miezi nane ya kiangazi. Kwa hivyo kama Watanzania wenye nyumba za bati wakatambua kwamba tayari wana chanzo cha maji na hivyo wakatengeneza *storage tank*, tutatumia, tutapata maji ya mvua ya kutosha na tatizo hili tutalipunguza kama siyo kulimaliza katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ikiwepo sera maana yake kutakuwa na miongozo, kutakuwa kuna uhamasishaji

na mambo mengine na hii tabia itaingia taratibu kwa Watanzania kujua kwamba tayari wana chanzo cha maji na hivyo kinachobaki ni kutengeneza *storage tank* angalau ya lita 50,000 na kuendelea. Mimi hapa nina ma-*tank* zaidi ya matatu yenye lita laki 200, na-enjoy, kwa hiyo naamini hiki kitu kikienda kwa Watanzania wengi shida hii itapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, niombe pia Wizara, badala ya kusubiri kila wakati maji yazame kwanza ardhini halafu ndiyo tuyafuate, unajua maji haya ya visima ni maji ambayo ni ya mvua, yakishazama yanaenda kwenye miamba yanatuama ndiyo tunafanya kazi ya kuyafuata chini. Hebu tujielekeze zaidi kwenye mabwawa kwa sababu mabwawa maji yanakuwa bado yapo juu na tukiyatega mabwawa ya maji yanakuwa na faida zaidi ya kunywa maji peke yake, kwa sababu bwawa la maji utapata maji ya kunywa, tutapanda samaki, tutavua samaki lakini na sehemu nyingine pia itamwagilia hata mazao. Kwa hiyo bwawa hili linakuwa lina kazi zaidi ya moja kuliko kusubiri yaende chini ndiyo tuyafuate kwa gharama kubwa kuyaleta juu.

Mheshimiwa Spika, ipo mipango mikubwa ya mabwawa, mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Chemba, kuna mradi wa Farukwa pale umeoongelewa, ni mradi mkubwa ambao lengo lake lilikuwa ni kulisha Dodoma, sijaona kama umepewa kipaumbele kikubwa. Bwawa lile likijengwa linakuwa hadi na kisiwa ndani, sasa hatuoni kwamba mipango hii ya mabwawa ikifanywa vizuri italeta faida mara mbili, mara tatu zaidi ya kupata maji ya kunywa. Kwa hiyo niombe wizara ijielekeze zaidi kwenye mabwawa kwa sababu fedha nyingi na miradi hii itakuwa *multipurpose* itafanya kazi kubwa zaidi kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia ...

**SPIKA:** Ahsante sana muda wako umeisha.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, nilikuongezea kwa sababu ulikuwa unaongelea Bwawa la Farukwa.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Nikaona hapa umegusa penyewe kabisa. Mheshimiwa Husna Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Mbunge wa Chemba, Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia kwenye Wizara yetu hii maalum kabisa ambayo tunatarajia inakwenda kumkomboa mwanamke wa Kitanzania kwenye jambo hili la shida ya maji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mchango wangu nimpongeze sana kaka yangu Mheshiwa Jumaa Aweso kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye Wizara hii, hakika nchi yetu sasa imekuwa na matumaini makubwa ya kutatua kero ya maji, pamoja na Naibu wake dada yangu kipenzi kabisa *Engineer* Mahundi. Uwezo wao na namna ambavyo wanaongoza hiyo Wizara inatusaidia sana kuwasemea akinamama kwenye jambo hili la maji.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimpongeze sana dada yangu *Engineer* Upendo Omari Lugongo, Mhandisi Mkuu wa Maji, Mkoa wa Tanga. Anafanya kazi kubwa sana, lakini kazi hii anayoifanya itakuwa na tija kama mambo haya mawili ambayo natamani kuyazungumza yatafanyiwa kazi katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, shida ya maji ni kubwa, pamoja na jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Serikali lakini huwa tunapeleka fedha nyingi kwenye kuanzisha miradi mipya lakini tumekuwa tukiiacha miradi ya zamani bila ukarabati. Ukiangalia kwenye Idara zingine kwa mfano Idara ya barabara tukishajenga barabara tunakuwa na ruzuku ya ukarabati wa barabara. Tukijenga vituo vya afya tunakuwa



na bajeti kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya vivyo hivyo kwenye mashule na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha ambazo tunatenga kwa ajili ya ukarabati wa miradi ya maji ni ndogo sana, muda mwingine tunaziachia Jumuiya za Watumia Maji ambazo hazina uwezo. Hizi Jumuiya za Watumia Maji ambazo kwa utaratibu wa sasa tunajenga miradi kwa kutumia fedha nyingi, lakini tunawakabidhi wenzetu waweze kuisimamia na kutumia *charges* ndogo ndogo ambazo wanachangia wakati wa kuchota maji waweze kukarabati hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu ambao kwa kweli unaweza kutukwamisha katika kutatua tatizo hili la maji katika nchi yetu kwa sababu hizo jumuiya kwanza hazina elimu, hazijaelimishwa vya kutosha, lakini jumuiya hizo zina-charge hao tunaowaita Watanzania wanyonge, Watanzania wa hali ya chini, ukienda huko vijijini hao wanaoenda kuchota maji kwa shilingi 200, mia 300 mpaka 500 ndiyo wale wale ambao tumeona kwamba hawawezi kulipa ada tunawapa elimu bure. Ndiyo wale wale ambao tunawapelekea ruzuku ya *TASAF* kwa kushindwa kukimu miasha yao. Sasa bado tumewawekea huu mzigo wa kuwa wanachangishana fedha kupitia kwenye visima vya maji, lakini baadaye wakusanye kwa ajili ya kukarabati jambo ambalo tungelifanya sisi kama Serikali, lingekuwa na mantiki kubwa sana katika kutengeneza uendelevu, *(sustainability)* ya miradi ya maji vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niishauri sana Serikali ione namna gani sasa inaweka kusudi la dhati katika kukarabati miradi hii hasa visima vile vya vijijini kabisa, kuwapunguzia huu mzigo akina mama wa vijijini ambao wanashindwa kuoga, wanashindwa kunywa maji, wanashindwa kulea watoto wao vizuri. Utakutana nao barabarani wamebeba madumu ya maji kama watoto mgongoni, wanahemea maji mbali kwa kushindwa kulipia gharama za maji muda mwingine lakini kukosa maji maeneo ya Jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitamani kulizungumza ni ukarabati wa mabwawa. Kule Tanga hususani kwenye Wilaya ya Mkinga kuna bwawa pale Duga, kule Handeni kuna mabwawa ya Mandera, Masomanga na Gendagenda. Kule Kilindi kuna bwawa la Kwamaligwa, Kwadudu na Mkuyu, mabwawa haya ni ya siku nyingi yamejengwa takribani kipindi cha uongozi wa Mwalimu Nyerere. Ni mabwawa ambayo yalikuwa na uwezo wa kutoa maji kwenye jamii nyingi, lakini hayajawahi kukarabatiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo sasa wanashindwa kupata maji lakini haya ukijumlisha na ile miradi mikubwa kama Potwe kule Muheza, Maramba kule Mkinga, Magina na Kwesine kule Lushoto ikikarabatiwa hii miradi ya siku nyingi ambayo ilikuwa inazalisha maji na kuhudumia kwa watu wengi zaidi inaweza kutatua kwa sehemu kubwa sana tatizo hili la maji. Lakini kwa sababu, muda ni mfupi sana nimeipitia hiyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri *inshallah* Rais ajaye labda, lakini kuna hii miradi ya *payment for result P4R*. miko a nane haijaguswa na hii miradi ikiwemo Mkoa wa Tanga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini Mkoa wa Tanga ina vijiji 846 lakini kati ya hivyo ni 400 tu vina mtandao wa maji na angalau watu wanapata maji safi na salama. Zaidi ya vijiji 400 kwenye Mkoa wa Tanga hawapati maji kabisa vijiji hivyo havina miundombinu ya maji kabisa, hawapati maji safi na salama.

Sasa kwa nini tusipeleke huu mradi niombe Wizara ya Maji na Serikali ione umuhimu wa kupeleka hii miradi ya *P4R* kwenye Mkoa wa Tanga. Lakini mwisho kabisa gharama ya maji ni kubwa sana, maeneo mengine tunaona mvua zikinyesha watu wananyanyua mikono juu wanamshukuru Mungu na hapo hawachukui tena maji ya *RUWASA* wala ya *DAWASA* wanatumia maji ya mvua kwasababu ya kutafuta ahueni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Nilishakuita Mheshimiwa Mohamed Lujoo Moni, Mbunge wa Chemba, hayupo! Katibu wa CCM ni kawaida ya Moni kujiandikisha na haonekani kwa hiyo, jina lake msiwe mnaniletea hapa ni mara kadhaa nimesha-*note* hiki kitu. Mheshimiwa Florent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi na niungane na wenzangu kupongeza Wizara ya Maji chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Waziri Awesso, Mheshimiwa Naibu Waziri, Eng. Maryprisca lakini pia na Watendaji Wakuu, Katibu Mkuu Eng. Sanga na Naibu Katibu Mkuu mama yetu Nadhifa Kemikimba lakini pia na Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA na Mameneja wote wa Mikoa na Wilaya zetu kwa kazi nzuri ndani ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa binadamu asiyeshekuru kwa kidogo hata kikiwa kikubwa hawezi kushukuru. Nishukuru Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa miradi mikubwa ya maji ambayo wametupatia ndani ya Wilaya ya Misenyi, ambapo tunao mradi wa Gera milioni 570 ambao umekamilika katika vijiji vitatu na sasa hivi nikushukuru sana Waziri kwa kutupatia *extension* katika vijiji vingine viwili vya Kashaka na Kashekya. Kwa hiyo, maana yake katika eneo hilo vijiji vyote vitakuwa vimefikwa kwa kupata maji kutoka kwenye Mradi wa Gera.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, wananchi wa Misenyi wanakushukuru pia kwa mradi mkubwa wa maji wa Kyakabulanzi wa bilioni 15.1 ambao tumeendelea kufuatilia unavyoendelea kujengwa na upande wa mkandarasi hela zimeendelea kwenda kwa kiasi lakini pia na upande wa *force account* kutumia wataalam wetu nimeambiwa vifaa vimeendelea kupelekwa. Kwa hiyo, tukushukuru lakini tuombe basi uwezeshaji uendeleo ili uweze kukamilika wananchi wa Kyaka, Kasambya na majirani pale waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kushukuru kwa bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa miradi ambayo kutoka katika

wilaya yetu imeweza kupitishwa na Wizara. Na tunaona katika maeneo mbalimbali miradi ya mradi wa maji katika eneo la Kashenye na Bushago na Bukwali tumeweza kupata fedha kiasi kwa ajili ya kupata maji lakini tumeona mradi wa Kitobo Katolelwa, Byemagwe, Byeju na Byamtemba yote imeweza kupata lakini na uchimbaji wa visima saba katika vijiji mbalimbali na kutanua mradi wa Kashaba.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara ya Maji ni kuomba kwa kazi nzuri ambayo mmeshafanya tayari, kuna miradi ambayo katika mwaka huu wa bajeti ambao unaisha tarehe 30 Juni, ilikuwa aidha ipo kwenye *pipe line* au imeshafanyiwa hatua za awali. Kwa mfano, tukiangalia katika eneo la Rwamachu na Rutunga Wizara mmechimba visima na wananchi wameshangilia kuona maji mengi yanatoka. Kwa hiyo, ni matarajio yao kwamba baada ya vile visima kuchimbwa tulikuwa tunaona hatua ya pili sasa ni kupeleka maji yawafikie wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hii bajeti sasa 2021/2022 tunaona kwamba tumeacha nyuma. Niombe Mheshimiwa Waziri najua bajeti sio kubwa sana tunagawana kilichopo, lakini basi wananchi wa Rwamachu na Rutunga waweze kuona sasa mradi unawafikia. Lakini sambamba na hiyo, Wizara imechimba visima katika kijiji chetu cha Ruano na Nyalugongo na yenyewe visima tayari vimechimbwa. Kwa hiyo, tungefarijika kuona sasa baada ya uchimbaji na wananchi kujitoa kwa ajili ya kushirikiana na Wizara na kuona maji yanawafikia basi, ndani ya bajeti hii ya 2021/2022 na eneo hilo liweze kuwekewa umakini ili bajeti iweze kutengwa wananchi hawa wapate maji.

Mheshimiwa Spika, lakini niombe kumkumbusha pia Mheshimiwa Waziri katika Kijiji chetu cha Kashasha chanzo kipo ni mradi wa Mbale ni *extension* ya kujenga matenki na kusambaza maji wa mserereko kwa wananchi wa Kijiji hicho cha Kashasha ili waweze kupata maji. Na katika bajeti ya mwaka huu ambao unaisha tarehe 30 Juni ilikuwa imetengwa hela kadhaa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huo unafanikiwa. Kwa hiyo, nikuombe sana Wizara yetu ya Maji

uweze kutusaidia katika maeneo hayo kwa kiasi kikubwa naamini, kama miradi hii itatekelezwa ndani ya Wilaya ya Misenyi angalau upatikanaji wa maji utakuwa umefikia takribani asilimia 72 au 75.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaendelea kushukuru kwa kuanza maandalizi ya miradi mbalimbali katika Kata yetu ya Minziro kwa Vijiji vya Minziro, Kalagara na Kigazi. Naamini na wananchi hao baada sasa ya upembuzi ukikamilika na vijiji vingine vya Rwamashonga lakini tumeona Mwemage kote kazi inaendelea pamoja na Kyazi. Niombe sana kuungana na wenzangu suala ambalo limekuwa likitatiza kidogo kwenye miradi yetu ya maji na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuombe Wizara kwa juhudi kubwa ambazo imeendelea kufanya na sisi kama kuna vikwazo vingine basi, ni kuliambia Bunge Tukufu kusaidia hasa *cash flow* ya miradi ambayo tayari iko kwenye *pipe line* inaendelea. Naamini kama fedha zikiwa zinakuja kwa wakati ingesaidia sana Wilaya fulani haivuki ikiwa na miradi viporo kwenda katika mwaka wa fedha unaofuata. Ikishavuka miradi haijatekelezwa na ilikuwa kwenye bajeti iliyopita inakuwa ni shida kidogo, maana yake mwaka ujao tunategemea tupate sasa miradi mipya kuliko hii ya nyuma ambayo haikutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuombe sana kwa juhudi kubwa mnazozifanya tuna Imani na Wizara kwa utendaji kazi wa Waziri na Wasaidizi wako wote, tunaamini haya yote yataweza kutendeka na wananchi wataendelea kupata maji na tutafikia asilimia zile ambazo zinaendana na sera ya maji katika vijiji na miji na tupate maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya ya Misenyi niseme wananchi wanafarijika sana na kwasababu, vyanzo vya maji ni vingi tunaendelea kupata matumaini hayo.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Florent Kyombo. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatey Massay.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwanza naunga mkono hoja hii. Lakini pia naipongeza Wizara ya Maji, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika juhudi zao za kila siku za kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliona hili na dhamira yake ya dhati ya kumtua mwanamama ndoo kichwani. Ambapo ameahidi kwamba, atauongezea nguvu mfuko wa maji kwa kutafuta vyanzo vipya vya kuongeza nguvu katika mfuko huu wa maji. Napongeza sana juhudi za Wizara kwa kukamilisha utekelezaji wa miradi 422 ya maji mijini na vijijini, pamoja na kupunguza gharama za uwekezaji kwenye miundombinu ya maji. Naomba juhudi hizo ziendeleo ili kuokoa pesa nyingi za Serikali kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ina upungufu mkubwa wa wataalam wa maji, naishauri Serikali ione umuhimu wa kuajiri hawa wataalam wa maji, ili kwenda kusimamia miradi ya maji huko mijini na vijijini. Ikiwa pamoja na kuwatumia wataalam wetu waliobobea ambao kwa sasa wamestaafu, angalau wawatumie kwa kipindi kifupi cha mwaka au miaka miwili ili kuongeza nguvu katika kuwekeza huduma hii ya maji kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ni muhimu kwa wananchi kwa maana ya binadamu, maji yanahitajika kwa wanyama, maji yanahitajika pia kwa miti na mimea yetu. Kwa hivyo, suala la maji ni suala la msingi na ninaipongeza Serikali kwa juhudi hizo kwa kuona tunafikia ile asilimia tuliyojiwekea kwa upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini. Lakini pia,

napongeza juhudi za Serikali kwa maana ya Wizara ya Maji wameliona hilo sasa, kwa kuhifadhi au kuvuna maji ya mvua. Hili ni jambo jema ambalo litasaidia sasa kupunguza zile changamoto za maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua maji ya mvua ni maji mazuri na yenye rutuba kwa kilimo. Kwa hivyo, tukihifadhi na kuvuna maji haya ya mvua yatakwenda kusaidia sana kwenye sekta hii ya uwekezaji wa kilimo lakini pia kwa matumizi mengine ya binadamu. Uvunaji wa maji ya mvua ni jambo la msingi kwa kuzingatia kwamba tunapoteza maji mengi na yanaharibu miundombinu yetu. Kwa hivyo, tukiyavuna na kuyahifadhi kwa kuyatumia kwa mahitaji yetu yote kwa viumbe sisi binadamu na wanyama, na kwa matumizi mengine ya kijamii yakiwemo mambo kama mfano, wakivuna maji ya mvua watu wa magereji wanaotumia maji mengi sana katika ukoshaji wa magari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo tungeweka msisitizo pia kwa hawa wanaotumia mambo ya ukoshaji magari wakavuna maji ya mvua ili kusaidia kupunguza yale maji safi na salama kutumia kwa mambo ya magari na mambo mengine. Kuna madeni makubwa sana kwenye Wizara hii ya Maji, ni vyema sasa Wizara ya Fedha ikawakata moja kwa moja wale wadaiwa sugu maana kuna wadaiwa na wadaiwa sugu. Sasa wale wadaiwa sugu wale Serikali ikate moja kwa moja ili fedha zile zikasaidie kuhakikisha kwamba, miundombinu ya maji inakarabatiwa, tunadhibiti upotevu mkubwa wa maji ili sisi tunaopata maji ambao hatulipi basi zile fedha zisaidie kwenda kutengeneza miundombinu na wale wenzetu ambao hawapati maji waweze kupata maji tuwalipie hizi fedha Serikali ikate moja kwa moja hizi fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na pia, hawa wadaiwa sugu naiomba Wizara *prepaid meter* zianze huko kwao kwasababu, wameonesha kwamba wao hawalipi kwa hivyo zile *prepaid meter* zikaanze kwa wadaiwa sugu wa maji, ili tuweze kupata fedha zetu za maji tuwekeze zaidi kwa

wananchi wengine wapate maji. Nimalizie kwa *DDCA* - Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa. Naomba Serikali iwekeze pale kwasababu, sasa miundombinu waliyonayo ya vifaa ni hafifu haviwezi kuchimba kina kirefu cha maji. Visima virefu vya maji inahitaji tuagize mitambo na wataalam kutoka nje waje watusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiwekeza pale tukisomesha wataalam wetu tukawa nao sisi wenyewe na tukawekeza mitambo ya kutosha pale ya kuhimili kuchimba kina kirefu cha maji, tunaweza tukaokoa pesa nyingi za Serikali na kupunguza urasimu wa utendaji katika kufanya kazi hii ya *DDCA*. Naomba Uwakala huu uongezewe nguvu na uwezo na kuwekewa wataalam wazalendo ili tukafanye kazi ya kutafuta maji, kwenye ardhi kuna maji ya kutosha.. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Upande wa Waheshimiwa wanawake walioomba kuchangia wamekwisha sasa wanafuata wanaume watupu. Lakini kabla ya hapo itakapofika saa saba Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na wajumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa wakutane Msekwa pale kwa kazi maalum.

Utawala na Serikali za Mitaa, Ardhi, Maliasili na Utalii wakutane Msekwa saa saba tukiahirisha hapa. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea mchana huu wa leo. Kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Awesso na dada yangu Mheshimiwa Eng. Prisca kwa kazi wanazofanya kwenye Wizara hii. Ninakupongeza kwasababu ninajua jinsi ambavyo



umesumbuka na Wizara hii, tangu ukiwa Naibu Waziri na sasa Waziri. Nataka nikupe moyo najua kuna changamoto, Biblia inasema namna hii kwenye kitabu cha Mwanzo mstari wa 1 na nikuambie tu unashughulika na kazi ya uumbaji ujue hilo unapotafuta maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwanzo anasema kwenye mstari ule wa 1, hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi, nayo nchi ilikuwa tupu na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji, na roho ya Mungu ilitulia juu ya uso wa maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aweso jua unazungumza na unafanya kazi katika hali ya uumbaji. Nakumbuka unapotembea kutafuta maji, unaposaidia kuipa maji nchi ujue kwamba unasumbuka na kazi ambayo Mungu aliifaya hapo mwanzo. Na nikuombe Mungu akusaidie katika hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini sasa umekuja Mbulu Vijijini nakushukuru, sasa ujue hiyo kazi Mbulu Vijijini inahitajika sana hiyo ya uumbaji kutafutia watu maji na katika *slogan* zetu tumewahi kusema maji ni uhai. Kwa hiyo, bwana, tusaidie tupe uhai katika Mbulu Vijijini. Ninashukuru nimeona kwenye bajeti imetengwa bilioni 2,300,000,000/= hii ni wazi kwamba, tunafanya kazi hii na niishukuru sana Serikali umetusaidia sana kwenye visima vya pale Haydom. Sasa kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ameitoa pale Samia Suluhu Hassan ya kutoa maji katika Ziwa Madunga kuleta katika Mji wa Dongobesh. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri kiumla, hii kuchimba visima naomba Wizara iangalie Je. ni njia sahihi ya kuwapatia watu maji? Maana visima vidogo vidogo wanavyochimba ninahakika katika maeneo mengi visima vile vimekufa kwasababu, tu maji maeneo mengine yanachimbwa na wanakutana na mwamba basi hela inakuwa imetumika zaidi. Kwa nini Wizara isiende ikachukue maji kwenye sehemu yenye ziwa ikapeleke kwenye vijiji pakawa na usambazaji, kuliko kila mahali kuchimba visima ambavyo baadaye vinakauka na hali kadhalika Serikali inakuwa imeharibu hela pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe Wizara ione namna hii kwamba, tunapochimba visima hivi vinatusaidia sana? Au kuchukua maji kwenye Ziwa na kuyasambaza? Nadhani tukichukua maji kwenye maeneo yenye Ziwa tukasambaza maji, fedha ya Serikali itatumika na watu wengi watapata maji kwa maeneo mengi. Sasa niombe kwenye bajeti yetu naona kuna vijiji umeviweka vingine si vya Jimbo langu na nimeshakuambia tangu jana wataalam wako waangalie, waweke visima vilivyo na majina yaliyopo kwenye Jimbo langu la Mbulu Vijijini. Naomba nikutajie sina hakika kama *Hansard* itashika lakini najua tutaongea baadaye.

**SPIKA:** Haya mjiandae Waheshimiwa Wabunge anataja majina. (*Makofi*)

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kuna kisima cha Gembaku, kuna kisima Getanyamba, Qaloda, Edahagichani, Maheri, Maretadu, Endadubu, Galoda, Dotina, Labay, Ng'orati, Garbabi, Qatabela, Qheteshi, Endaanyawish na Endaharqadat. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ndugu yangu mpendwa hivi ndio vijiji vyangu, lakini vijiji ulivyoviweka sio vya kwangu kabisa, angalia kitabu chako cha bajeti. Wataalam waangalie vijiji walivyoweka si vya kwangu lakini waviweke basi hivi nilivyovitaja kwasababu, najua ndivyo vilivyoombwa katika bajeti toka Wilayani.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana naamini atakuwa amevishika na ndugu yangu Awesso ni kijana mzuri sana na *slogan* zako nazipenda. Bwana sikufichi na kule kwetu nawapongeza sana wataalam wa maji wamejitahidi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maji katika Mkoa wa Manyara kuna shida kubwa sana ni asilimia 53 kwa Mkoa wa Manyara unaopata maji. Kwa hiyo, ni chini ya asilimia ya nchi. Lakini pia, Jimbo la Mbulu Vijijini tuna asilimia 59 si mbaya sana lakini si nzuri sana. Lakini ukiangalia pale Haydom Mheshimiwa Aweso, uliahidi mwenyewe kisima kichimbwe mpaka leo

kisima hakijachimbwa bwana. Haydom pale tuna asilimia 52 tu ya wakazi wanapata maji basi nikuombe sana angalia maeneo hayo. Lakini Haydom na Dongobesh tumeomba mtusaidie tupatieni Mamlaka ya Maji kwasababu, kuna jumuiya ya watumia maji wana hela nyingi sana pale zaidi ya milioni 400, ukiwaacha wale wananchi watumie ile hali ya watumia maji hainogi sana kwa sababu pale hawana wataalam wanaofanya kazi hiyo sio wakuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, lakini Haydom na Dongobesh tumeomba mtusaidie tupatieni Mamlaka ya Maji kwa sababu kuna Jumuiya ya Watumia Maji wana hela nyingi sana pale zaidi ya shilingi milioni 400, ukiwaacha wale wananchi watumie utaratibu ule wa watumia maji hainogi sana. Nasema hivyo kwa sababu pale hawana mafundi na wataalam wanaofanya kazi hiyo sio wa kuajiriwa kwa hiyo kudhibiti ile fedha kwa kweli hali si njema. Nikuombe sana uone jambo hili kwa sababu ni mji mkubwa unakua na kuna hospitali kubwa ya Rufaa ya Haydom.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa zaidi ni *units* za maji, imekuwa kero sana katika Mji wa Haydom na Dongobesh, *unit* imekuwa Sh.2,000. Mheshimiwa Waziri utakapofikia hatua ya kupelekea *pre-paid machine* za kulipia maji, nikuombe kabisa anzia na hiyo miji ya Haydom, nafikiri mambo yatakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine *DDCA* wamechimba visima tisa hawajapeleka maji yaani wamechimba *pump* wakazifunika. Niombe wazipeleke zile *pump* ili watu wapate maji. Wananchi wanapoangalia *pump* inakuwa taabu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Flatei Massay. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani kwetu. Niungane na wenzangu kuwapongeza viongozi wa Wizara hii tukianza na Mheshimiwa Waziri Aweso na Naibu wake kwa kweli mnafanya kazi na mna kipaji cha kipekee cha kusikiliza watu na hiyo ndiyo sifa kubwa ambayo mnayo. Mnatenga muda kusikiliza watu badala ya ninyi kusema ili watu wawasikilize. Kwa hiyo, endeleeni na moyo kama huo ili mpate kushauriwa na ninyi muweza kuyatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, nimpongeze Katibu Mkuu, *Engineer* Sanga lakini kipekee nimpongeze Mtendaji Mkuu wa *RUWASA*, *Engineer* Kivegalo. Ni watendaji wachache sana ambao wakifanya ziara wanatenga muda wa kukutana na wanasiasa. *Engineer* Kivegalo alivyofanya ziara Mkoani Mtwara alitenga muda wa kukutana na Wabunge wote wa Mkoa wa Mtwara. Watendaji wengi wana kawaida ya kusema wanasiasa wana nini hao lakini huyu alitembelea miradi, akawasiliza watendaji, jioni akatenga muda kwamba nimewasikiliza watendaji sasa nataka niwasikilize ninyi wawakilishi wa wananchi. Hongera sana *Engineer* na endelea na tabia kama hiyo utafanikiwa, naona *future* yako ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wenzangu wa Mtwara waliochangia kuhusu suala la maji Mkoani Mtwara. Kwa kweli suala la maji Mkoani Mtwara ni tete na hata kikao cha Kamati ya Ushauri cha Mkoa kilichopita agenda ya maji iliwekwa pembeni kwamba tuwe na kikao maalum kwa ajili ya kuzungumzia maji Mkoa wa Mtwara. Mheshimiwa Aweso nakupongeza kwa sababu tulivyofika hapa tulikutana, tukafanya kikao cha Wabunge wa Mtwara ukatusikiliza na wewe umeanza kuyafanyia kazi. Ndio maana nikakwambia kwamba una sifa ya kusikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maombi yetu makubwa yalikuwa mawili na nikushukuru kwa yote umeshayafanyia kazi. Cha kwanza, tulikwambia kwamba Mradi wa Maji wa Makonde ambao kwa bahati mbaya uliondolewa kwenye Mradi wa Vijiji 28 umeurudisha tena kwenye orodha ile, tunakupongeza sana. Mradi wa Makonde unahudumia karibu asilimia 40 ya Mkoa wa Mtwara, unahudumia halmashauri nne, Newala Mjini, Newala Vijijini, Tandahimba na Nanyamba. Kwa hiyo, mradi huu ukitekelezwa ipasavyo tutakuwa tumepunguza tatizo la maji katika Mkoa wetu wa Mtwara. Nikuombe uskilize ushauri wetu kwamba mradi wa maji wa Makonde chanzo kikubwa cha Mitema kuna maji mengi sana. Kwa hiyo, tutumie chanzo cha Mitema kupeleka maji Tandahimba na Nanyamba mtakuwa mmetatua changamoto ya maji kwa kiasi kikubwa katika Mkoa wetu wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi letu la pili kwenye kikao kile tulikwambia muda umefika sasa tutumie maji ya Mto Ruvuma. Mimi Jimbo langu la Nanyamba, Mheshimiwa Katani amesema kwake ni kilometa nane tu mimi ni *zero distance*, kwa sababu wananchi wangu wakati ule walikuwa wanalala Tanzania wanafanya kazi Msumbiji wanavuka kwa miguu Mto Ruvuma, kabla ya matatizo yale ya Msumbiji hayajaanza.

Mheshimiwa Spika, kile chanzo cha maji cha mradi wa kupelekeza maji Manispaa ya Mtwara kipo Nanyamba na maji yapo ya kutosha. Nimeona hapa tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kuyatoa maji Maembe Chini kwenda Nanyamba kama nilivyoshauri siku ile. Hongera sana uendelee kusikiliza hivyo, mradi huu unagusa vijiji 74 na Kata zaidi ya 13 ambazo ni za Nanyamba, Mtwara Vijijini na inawezekana mradi huu ukavuka ukaingia Jimbo la Mtama kwa sababu tumepakana. Kwa hiyo, mradi huo ukitekelezwa utatatua changamoto nyingi sana si za Nanyamba tu na maeneo mengi ya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu kwamba muda umefika sasa kuanza utekelezaji wa mradi huu wa kutoa maji Mto Ruvuma na kupeleka Mtwara Manispaa. Nimeona shilingi bilioni sita zimetengwa maana

siku za nyuma ilikuwa mradi huu unazungumzia tutatoa fidia, tutafanya upembuzi yakinifu lakini leo nikupongeze Waziri kwamba umeanza kuweka fedha. Naomba wakati wa utoaji wa fedha basi hizi fedha zitolewe ili mradi huu mkubwa uanze kutekelezwa na Manispaa ya Mtwara tuwe na maji ya uhakika kiasi kwamba hata wawekezaji wakija wajue wanawekeza Mtwara ambayo ina maji na umeme wa uhakika ambao sasa hivi upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba imesajiliwa kama Halmashauri ya Mji na kwa Sheria ya Maji tuna uwezo wa kuwa na mamlaka yetu. Sasa hivi tunahudumiwa na Mamlaka ya Maji ya Mtwara *(MTUWASA)* katika kipindi hiki cha mpito.

Kwa hiyo, naomba na hili sasa Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi, sisi tuna hadhi ya kuwa na mamlaka ya kwetu na hakuna sababu ya kuitumia ile Mamlaka ya *MTUWASA*. Ni muda umefika sasa kufanya taratibu zinazotakiwa ili na sisi tuwe na Mamlaka ya Maji ya Mji wa Nanyamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa mwisho ni kuhusu *RUWASA*. *RUWASA* ni mtoto mchanga anafanya kazi vizuri lakini kama walivyosema Wabunge wengine ana changamoto hebu tuiwezeshe *RUWASA*. Tuiwezeshe kwa vitendea kazi na rasilimali watu. Wilaya nyingine zina halmashauri zaidi ya moja, kwa mfano mimi Meneja wangu wa *RUWASA* anashughulikia Mtwara Vijijini na Nanyamba, lakini ana watendaji wachache. Naomba tuongeze watumishi ili mamlaka hii ambayo imeanza kufanya kazi vizuri iendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Kipekee hizi pongezi sio za kubahatisha, Mheshimiwa Waziri unafanya kazi nzuri sana. Kitu kinachotia moyo ni namna ambavyo unawasilikiza Wabunge wanapoleta hoja zinazotoka kwenye majimbo yao. Mimi nikushukuru kwanza kwa miradi ambayo tumekaa pamoja na watendaji wenzako na nimeona kwenye bajeti umeiweka. Ni jambo zuri na mimi niseme kwa Kyerwa maeneo mengi kwa kweli hatuna maji safi na salama na wewe hili umeliunga mkono kwa kuweka vijiji vyote, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti tunaona mipango mizuri lakini jambo lingine hii fedha inaletwa? Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri ili kazi yako iendelee kuwa nzuri hizi fedha ziletwe. Kuna maeneo ambayo kwa kweli kwangu yana shida kubwa sana, ukienda kwenye Kata kama za Bugala, Businde, Murongo kwa kweli hali ni ngumu sana. Nishukuru nimeona vijiji vya Bugala na Businde kule mmetenga fedha kwa ajili ya kuchimba visima lakini maeneo mengine kama Kibale ule mradi wa Kigologolo kuuongezea uwezo ili uweze kusambaza maji kwenye vijiji vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tuliongelea mradi wa vijiji 57, mradi huu ni mzuri sana na ndio mkombozi kwa wananchi wa Kyerwa. Kwa hiyo, niombe sana fedha ambayo mmeitenga iwafikie ili wananchi wa Jimbo la Kyerwa waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, *RUWASA* bado ni wachanga na ukija kule kwangu hawana gari wala ofisi, hawa watu wanawezaje kufanya kazi? Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri waongezee uwezo ili waweze kufanya kazi nzuri. Mimi niseme kwa upande wa Kyerwa yule kijana ambaye mmeleta pale anafanya kazi nzuri lakini anafanya

kazi kwenye mazingira magumu. Kwa Kyerwa ni kipindi kirefu cha mvua hata kwa pikipiki huwezi kwenda kukagua miradi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii miradi tunayoitengea fedha kama haitapata usimamizi mzuri tutakuwa tunafanya kazi bure. Tutakuwa tunapeleka fedha nyingi lakini fedha ambayo hatuoni inachokifanya kwa sababu hakuna usimamizi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge hapa wamekuwa wakiongelea suala la kubambikiziwa bili. Hili lipo kila maeneo hata hapa Dodoma, mimi nimekutana na watu wengi pale ofisini kwa Waziri wanalalamika. Nimekwenda Karatu, kule ukitaka kuchota maji unaingiza kadi kama ulivyolipia ndivyo unavyopata maji. Naomba hili lifanyike nchi nzima ili tuondoe suala la kubambikizia watu bili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mama mmoja nilimkuta ofisini kwa Waziri wamemletea bili milioni 1 na hana hata biashara na hili limekuwa likifanyika maeneo mengi. Hata mimi nyumba ninayokaa hapa Dodoma wameleta bili ya ajabu kwelikweli tena kipindi ambacho sisi hatukuwepo...

## T A A R I F A

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, endelea nakuruhusu.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa tu ndugu yangu anayezungumza kwamba hata kwenye nyumba ya baba yangu mzazi Mzee Gwajima ambapo anaishi yeye mwenyewe bili inakuja shilingi 600,000 kila mwezi. Anachosema ni kweli na ni sahihi.

**SPIKA:** Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Bilakwate?



**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naipokea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima waje na mpango mtu analipia kutokana na matumizi yake, kama ilivyo *LUKU*, tutakuwa tumemaliza hili suala la kubambikizia watu bili. Sijui kuna nini kinaendelea pale, mpaka watu wengine wakawa wanasema wanakusanya fedha ili waweze kujlipa vizuri, suala hili linaichafua Wizara lazima Waziri aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la mwisho ambalo napenda kuchangia ni kuhusu *RUWASA*. *RUWASA* ni ofisi ambayo inajitegemea, kwa upande wa Kagera hakuna Bodi ya Manunuzi wanategemea *BUWASA*. Kwa hiyo, niombe sana suala hili liangaliwe wawezeshwe ili wawe na Bodi yao waweze kuwa manunuzi yao kuliko kutegemea ile ya Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Bilakwate kwa mchango wako. Kwa kweli nipigie tu mstari na mimi eneo la bili kuwa kubwa sana ni kero kubwa. Mimi nilitegemea Wabunge Wanawake ndiyo mngepigia mstari kweli kweli hapo. Bili kubwa jamani, bili kubwa kila mahali sijui kuna shida gani. Mheshimiwa Waziri liangalie hilo, watu wako sijui wana malengo makubwa ya kukusanya fedha kwa hiyo inabidi waweke bili kubwa sana. *(Makofi)*

La pili ni lile alilosema pia, tukiweza nchi nzima hata huko vijijini watu wakaweka kadi wakapata maji, tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana ya wizi, kwa sababu miradi ya maji ina fedha nyingi sana, hata Kijiji chochote kile Kamati ya Maji ndio tajiri kuliko kamati nyingine yoyote ile, kwa hiyo wana uwezo kabisa wa kufanya vitu mbalimbali. Hata hivyo mnakuta miundombinu inaharibika hawana hata shilingi moja kwenye akaunti kwa sababu ya fursa ya kaufujaji fulani ambako kapo katika miradi ya maji wakati ina uwezo kabisa

ya kujiendesha kwa sababu maji ni uhai lazima watu wapate maji ili waweze kuendelea.

Tunaendelea na Mheshimiwa Amandus Chinguile, Mbunge wa Nachingwea utumalie kwa mchana wa leo.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nami niwashukuru sana viongozi wetu wa Wizara, kwa kweli Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri vijana mnatuheshimisha sana kwa sababu mnachapa kazi nzuri. Kwa kweli hii inaonesha kwamba vijana wakipewa nafasi wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, yako maeneo ambayo na mimi nitayazungumzia kwa jimbo langu; kuna Vijiji vya Namanga, Rweje, Mchangani pamoja na Kiegei, Matekwe na Nakilimalono. Maeneo haya tayari upembuzi yakinifu ulishafanyika na vibali kwa ajili ya uendeshaji wa miradi ya maji kwenye maeneo haya tayari vilishatoka lakini kwa bahati mbaya sana maeneo haya hayajapelekewa fedha. Naomba sana wakati anahitimisha hotuba yake aseme lolote kwa ajili ya maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ukitoka Nachingwea Mjini kuelekea Liwale ni kilometa 5 tu, ukipita nyakati za usiku utakuta moto unawaka siyo wachawi, hawa ni kinamama ambao wanahangaika kuhamia maji, inasikitisha! Maeneo hayo sisi tunakua hali iko hivyo mpaka sasa hali iko hivyo.

**SPIKA:** Kuhamia maji ndio nini?

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, wanakwenda kwa ajili ya kusubiria maji kwenye vile visima vidogo vidogo. Sijui Kiswahili chake rahisi niseme nini lakini kwa kweli ni kuhemea lakini kwa kweli wana shida kwenye maeneo haya. Hata ukizungumzia kama kuna mafanikio ya maji yamepatikana maeneo haya ni lazima uangalie kushoto,

kulia maana hawatakualewa. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na juhudi zote ambazo amezifanya maeneo haya kwa kweli yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ya Matekwe yana mabwawa ambayo yalichimbwa maalum kabisa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji lakini mpaka leo kazi ile mahsusiliyokusudiwa kwenye mabwawa haya haijatekelezwa. Niishauri Wizara badala ya kusubiri mradi huu ambao hatujui utaanza lini wafikirie namna ya kutuma wataalam ili waone maji haya yanapoweza kutumika kwa matumizi ya kunywa kwenye maeneo husika. Maeneo haya ni mbali na maeneo ya mjini, kwa kweli sio tu wanakunywa maji machafu lakini wanakunywa maji ambayo mbuzi, ng'ombe, tembo na wanyama wengine wanatumia. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara ipigie mstari wa huruma kabisa kwenye maeneo haya ili wapiga kura wangu wa Jimbo lile la Nachingwea waweze kufaidika pia na miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa maji wa kutoka Masasi kuja Nachingwea lakini kupitia kwenye Kata ya Ndomoni, nashukuru Ndomoni maji yamefika. Hata hivyo, kwenye kata hiyo hiyo kuna eneo lingine ambalo lina watu wengi la Ndomondo na Makitikiti. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na mafanikio haya ya mradi huu kuufikisha hapa, aone namna ambavyo atawapelekea maji watu wa maeneo haya ya Ndomondo na Makitikiti. Kwa sasa wanakwenda kilometa nyingi kutafuta maji na hii sasa kwa wale ambao kwa kweli wameoa ni shida. Wapo watu ambao sasa wamekuwa na mapengo baada ya kupewa vipigo na wanaume zao maana anaondoka asubuhi anarudi saa 8 na hii si sawa.

Mheshimiwa Spika, uko mradi wa maji wa Mbwinji umefika Nachingwea, naishukuru sana Serikali lakini tunahitaji huu mradi utanuke kwenye baadhi ya maeneo. Najua Mheshimiwa Waziri anaufahamu vizuri hebu atusaidie ili watu wengi zaidi waweze kupata maji haya safi na salama kutoka kwenye mradi huu wa Mbwinji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, yako maeneo ambayo wenzetu wa *TASAF* walishachimba visima vya maji sasa yamebaki mashimo. Namwomba sana Waziri akipata muda twende Nachingwea tukaone maeneo haya, vile visima havijawahi kutoa maji hata siku moja. Tulichoshuhudia ni wale wataalam wa maji waliokuja kuchimba vile visima wametuachia mashimo lakini sio hivyo tu, wametuachia na wapwa zetu kule jimboni. Hatukuhitaji wapwa, sisi tumehitaji maji! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya nayazungumza kwa uchungu kwa sababu yako mashimo, unafika kijijini unakuta mashimo manne matano na yote hayajatoa maji. Hii ni hasara kwa Serikali. Waziri naomba twende kwa pamoja tujue ni nini kilichotokea maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, najua huu muda umenipa wa ziada lakini kwa kweli inasikitisha sana ningepata muda mrefu ningezungumza mambo mengi ungejiuliza haya mambo yanafanyika Tanzania au lah! Nimuombe Waziri tukiambatana pamoja na mimi kwa kweli atakwenda kujionea mwenyewe. Haya mambo yapo, pamoja na kuwasifu kwa kweli mnafanya kazi nzuri twende tukakamilishe kazi hii ambayo kwa kweli taifa linatutegemea sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chinguile, Mbunge wa Nachingwea.

Mheshimiwa Waziri kwa kweli na mimi nakuomba uende kutembelea Nachingwea maana Mheshimiwa Mbunge aliyoongea, lakini usiangalie maji tu, ukienda uone na hao wajomba ambao wametokana na miradi yako ya maji ya *TASAF* na mingine pia, uone utaratibu wa ruzuku kwa ajili ya wajomba hawa. Maendeleo, unajua haya mambo, posho za wajomba apelike kule. (*Makofi/Kicheko*)

Naomba niwatambulishe wale vijana kutoka Chuo Kikuu cha cha Ruaha, Iringa Mjini, wageni wa Mheshimiwa

Msambatavangu. Karibuni sana. Wanaongozwa na Waziri Mkuu, Bwana Moses Muya, ahsante sana. Hawa ni vijana wa Kitivo cha Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Ruaha. Nafikiri ndiyo maana wapo *smart* sana, unajua wanasheria bwana, hongereni sana, mjitahidi kwenye masomo, bahati mbaya leo Mwanasheria Mkuu hayupo lakini asubuhi kama vile nilimuona. Karibuni sana vijana wetu na Mbunge wenu wa Iringa anafanya kazi nzuri sana hapa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu; anachapa kazi kwelikweli siyo kama yule mliyekuwa naye wakati ule, alikuwa analala tu humu, lakini sasa mnacho chombo Iringa Mjini. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtandao wetu siku zote hizi ulikuwa kidogo hauko sawa sana, ni wa kubabaishababaisha, ukitumiwa picha au nini huwezi kuona, ukituma kitu fulani huwezi kuona lakini lakini tumesharekebisha hiyo hali hivi sasa ili *at least* kwenye ukumbi huu ni *full swing* na mkiona kuna shida basi muwe mnanijulisha ili kusiwe na *hindrance* ya mawasiliano. Kama Waziri yupo hapa anatumiwa *event* yenye picha kutoka mahali fulani au nini aweze kufungua na kuona papo hapo. Maana dunia sasa hivi ni *faster*, kufungafunga vitu kwa Waheshimiwa hawa haiwezekani lakini tumerekebisha hilo, mkiona kuna shida muendeleo kutushauri, tunawaahidi kuendelea kurekebisha kila kitu.

Kama tulivyokubaliana tutaendelea kuchangia Jumatatu, huenda Waziri akahitimisha Jumatatu asubuhi tu yaani *bysaa 7* tukawa tumemaliza, huenda ikawa hivyo kwa sababu tumeshachukua wachangiaji wengi sana, waliobaki wale wachache mtamalizia Jumatatu na kuhitimisha. Tukishindwa basi tutahitimisha jioni siku ya Jumatatu.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia ni muhimu sana, msikimbilie Eid kule ukaondokaondoka tu bila ya kuwa umemuaga Spika, ukikimbilia huko sawa pia lakini tusilaumiane.

Baada ya ushauri huo, sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi Siku ya Jumatatu itakuwa tarehe 10

Mei, 2021, Saa Tatu Kamili Asubuhi na kesho Yanga wajiandae kwa magoli mengi sana. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Simba mjiandae. *(Kicheko)*

*(Saa 7.04 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 10 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*